**3 FEBRUARI, 2026**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA PILI

### Kikao cha Sita – Tarehe 3 Februari, 2026

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

Kiapo cha Uaminifu na Ahadi ya Uzalendo kwa Wabunge.

**SPIKA:** Kiapo cha Uaminifu.

### KIAPO CHA UAMINIFU NA AHADI YA UZALENDO KWA WABUNGE

1. Mhe. Beng'i Mazana Issa

*(Mbunge aliyetajwa hapo juu aliapa Kiapo cha Uaminifu na kutamka Ahadi ya Uzalendo)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa ninamwita Mheshimiwa Paresso kuendelea na Shughuli za Bunge.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Cecilia D. Paresso) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**3 FEBRUARI, 2026**

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na maswali, Ofisi ya Waziri Mkuu, na sasa namwita Mheshimiwa Moses Charles Bujaga aulize swali.

Na. 89

**Ujenzi wa Vituo vya Afya Wilaya ya Kwimba**

**MHE. MOSES C. BUJAGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatimiza ahadi ya ujenzi wa Vituo vya Afya Walla, Mwambomba, Mwagi, Mhandi na Mwamala?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Moses Charles Bujaga, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi 2024/2025 Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya kwa ujenzi wa vituo vya afya katika kata za kimkakati kote nchini, zikiwemo Kata za Isunga, Kadashi, Kikubiji na Hungumalwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Disemba, 2025 Serikali ilikuwa imekamilisha ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya 898 ambavyo vinatoa huduma ngazi ya kituo cha afya ikiwa ni pamoja na huduma za upasuaji wa dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa kujenga vituo vya afya katika Kata za kimkakati ikiwemo Kata ya Walla ambayo imetengewa jumla ya shilingi milioni 250 katika mwaka wa fedha 2025/2026. Utekelezaji utaendelea kwenye Kata zitakazokidhi vigezo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba kadiri fedha zitakavyopatikana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Moses Charles Bujaga, swali la nyongeza.

**MHE. MOSES C. BUJAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, ningependa kuongeza maswali madogo mawili. Kituo cha Afya Budushi kina daktari mmoja, Kituo cha Afya Kadashi kina daktari mmoja, na Kituo cha Afya Isunga hakuna daktari. Ningependa kujua Serikali ina mpango gani wa dharura kuhakikisha kwamba tunapata watalamu katika vituo hivi vitatu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kituo cha Afya Budushi hakina gari la kubeba wagonjwa inapotokea dharura ya kupeleka wagonjwa hao kwenye Hospitali ya Wilaya iliyoko kilometa 33. Je, Serikali itatupatia lini gari la kubeba wagonjwa Kituo cha Afya Budushi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuuliza maswali mawili ya nyongeza na ninaomba niyajibu kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu upungufu wa madaktari na ndiyo maana tulipata vibali vya kuajiri madaktari 5,000 nchi nzima na baadhi ya madaktari wameshafika maeneo yao ya kazi. Ninawaomba madaktari waliopangiwa kwenda kwenye vituo vyetu vya afya ili wafike kwa wakati, lakini kama haitoshi nimwelekeze Mkurugenzi kuendelea kutoa ajira zile za lazima hasa kwenye maeneo ambayo tuna upungufu kama alivyoainisha Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu magari ya kubebea wagonjwa, tayari tulishapeleka magari zaidi ya 594 katika maeneo yetu kwa Halmashauri zote nchini, lakini pia tunaendelea kuomba magari. Kadiri tunavyoyapokea kutoka Wizara ya Afya, tutaendelea kuyaelekeza katika vituo vyetu vya afya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilikuona Mheshimiwa Sylvia Sigula, swali dogo la nyongeza.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Kata ya Ilemba iliyoko Wilaya ya *Sumbawanga DC* yenye wakazi zaidi ya 27,000 haina Kituo cha Afya, na nimekuwa nikiuliza swali hili, na majibu ya Serikali yamekuwa ni yale yale. *On a serious note,* ni lini hasa ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Ilemba utaanza? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge Sylvia kwa kuuliza swali hili la nyongeza. Nimhakikishie ya kwamba Wilaya ya *Sumbawanga DC* kwa kata aliyoiainisha Mheshimiwa Mbunge, nimhakikishie tunakwenda kujenga Kituo cha Afya na kitaanza kutoa huduma kwa watu wetu. Serikali ya awamu hii siyo ya *busness as usual,* tunakwenda kufanya hakika. Niwahakikishie wananchi wa Kata hii watapata huduma ya afya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Tinnar Chenge, swali la nyongeza.

**MHE. TINNAR A. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kuniona. Kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Simiyu, ninaomba kuulizwa swali la nyongeza. Ni lini Serikali ina mpango wa kujenga Kituo cha Afya cha Bunamhala Wilaya ya Bariadi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza kuhusu Kituo cha Afya Simiyu, Bariadi. Katika vile vituo vyetu vya kimkakati Majimbo 94 na yale Majimbo mapya pamoja na Halmashauri ya Wilaya Simiyu na wao ni wanufaika, watakwenda kupata kituo cha afya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru, nilikuona Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaishukuru sana Serikali kwa kutujengea Vituo vya Afya viwili; Kituo cha Afya cha Miamba na Kituo cha Afya cha Mtii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vituo hivyo vyote viwili hakuna hata kimoja chenye wodi za kulaza wagonjwa. Je, Serikali itaanza lini kutujengea wodi hizi kwa sababu vituo vya afya ni vikubwa, vina kila kitu lakini wagonjwa hawana mahali pa kulala?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vyote vya kimkakati vilipoanza kujengwa tulielekeza shilingi milioni 250 ambazo bado hazitoshi, na tayari tumeshawaelekeza Wakurugenzi kuanza kutenga fedha, mapato ya ndani kujenga wodi ambazo zinatakiwa kutoa huduma katika vituo vyetu vya afya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea. Sasa ninamwita Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo aulize swali lake.

Na. 90

**Hitaji la Gari la Wagonjwa Kituo cha Afya Nyakahura - Biharamulo**

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kupeleka gari la kubebea wagonjwa katika Kituo cha Afya cha Nyakahura Wilayani Biharamulo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Jimbo la Biharamulo Magharibi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi 2024/2025 imenunua jumla ya magari 594 zikiwemo *ambulance* 382 na magari ya usimamizi ufuatiliaji 212 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo imepokea gari moja la kubebea wagonjwa mwezi Novemba, 2023 na kupelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Biharamulo. Aidha, idadi hii inafanya Halmashauri ya Biharamulo kuwa na jumla ya magari matatu ya kubebea wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa magari ya wagonjwa kwa awamu kwa ajili ya vituo vya afya vyenye uhitaji kote nchini kikiwemo Kituo cha Afya Nyakahura. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali. Ninakiri kwamba tulipokea gari moja la wagonjwa, na gari moja la usimamizi, kama alivyosema kwenye jibu la msingi Tunaishukuru sana Serikali. Hata hivyo kwa jiografia ya Biharamulo, Wilaya ile ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoongelea Kituo cha Afya cha Nyakahura ni kilometa 82 kutoka Biharamulo Mjini, lakini Waziri Mkuu akiwa katika ziara Mkoa wa Kagera tarehe 21/09/2021 *specifically* alitoa ahadi ya *ambulance* kwa Kata ya Nyakahura kwa ajili ya hicho kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa kujua ahadi hiyo ya Waziri Mkuu ninayoiongelea ndiyo inayoelekea Nyakahura pale? Kwa hiyo, swali la kwanza, kwa sababu ni ahadi ya Waziri Mkuu, ni lini tutapa ile *ambulance* sawa na Waziri Mkuu alivyokuwa ameahidi kwa ajili ya wananchi wa Nyakahura? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kata ya Kabindi ni *center* kubwa sana ambayo inahudumia Kata karibu tano ukielekea njia ya Mwanza ambazo nyingine zinapatikana zaidi ya kilometa 70 mpaka 80 kutoka Biharamulo Mjini na *center* ile ni kubwa, lakini upande ule hatuna kabisa *ambulance* ambayo inaweza ikakaa pale kwa ajili ya kuhudumia hizo Kata tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na hii ya Nyakahura, ni lini sasa tutapata *ambulance* nyingine itakayokuwa inakaa Kabindi kwa ajili ya kuhudumia kata tano inapotokea dharura aidha waletwe Biharamulo Mjini au wapelekwe Mwanza kwa ajili ya kwenda kupata matibabu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kupata pia majibu ya Serikali kuhusu *issue* hiyo ya *ambulance* nyingine ya pili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ninakiri na kwenye kampeni nilifika katika Jimbo la Biharamulo Magharibi na anayoyazungumza Mheshimiwa Chiwelesa yako sahihi. Nimhakikishie ahadi za viongozi wetu wakuu wote nchini zinakwenda kutekelezwa kwa wakati, na tumeshaomba *ambulance* nyingine, zinakuja kutoka Wizara ya Afya. Zikifika tunakwenda kutekeleza ahadi hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la pili, tunalichukua kama Serikali ili kuangalia kulingana na idadi za *ambulance* tutakazokuwa tunazipata ili kuweza kuwaongezea. Ni kweli Jimbo hili kijiografia ni pana na lina idadi kubwa ya watu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Arif Premji, aulize swali dogo la nyongeza.

**MHE. ARIF S. PREMJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Je, ni lini Serikali itapeleka gari la kubebea wagonjwa Kituo cha Afya Kilambo, *Mtwara DC* ukizingatia kituo hicho kipo mpakani mwa Msumbiji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu magari ya kubebea wagonjwa, tuna maeneo yenye upungufu kweli, tunakiri, na tumeendelea kuyaomba magari haya pamoja na yale mengine ambayo tayari Serikali imeshayatoa katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, ombi lake tunalichukua kwa maana ya kwamba tunapoenda kuomba magari mengine na yeye awe mnufaika katika gari hili la *ambulance*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, nilikuona Mheshimiwa Joseph Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri, Halmashauri ya Wilaya ya Geita ina Majimbo matatu na ina hospitali mbili zenye hadhi ya Wilaya kikiwemo na kituo kikubwa cha afya kilichopo Nyarugusu kwenye Jimbo lake Mheshimiwa Waziri na magari tunayo mawili tu. Anapopatikana mgonjwa kutoka Nyarugusu inalazimika kutoa gari kilometa 100 kwenye Hospitali ya Wilaya Nzera au kilometa 80 kule Katoro. Je, ni lini Serikali itapeleka *ambulance* kwenye kituo kikubwa cha Nyarugusu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwape pole na kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Busanda, Majimbo yote matatu yaliyo katika Halmashauri ya Wilaya ya *Geita DC* kwanza kwa uvumilivu mkubwa na usikivu mkubwa na wanatuunga mkono viongozi wao. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Kasheku Musukuma, tutafanya namna ya kupeleka gari la *ambulance* ili kuokoa maisha ya wagonjwa wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuendelee kusubiri, Serikali tumeshaomba magari haya kutoka Wizara ya Afya. Hivyo, Jimbo la Busanda na lenyewe ni wanufaika katika kupata ambulance mpya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, nilikuona Mheshimiwa Regina Mikenze.

**MHE. REGINA H. MIKENZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninapenda kuuliza swali. Ni lini Kituo cha Afya cha Kata ya Rwamgasa kitakamilishwa na kuanza kutoa huduma? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifika katika Kituo cha Afya cha Rwamgasa na

kiukweli kimeanza kutoa huduma za *OPD* na kuna majengo yanazidi kuongezwa pale kupitia mbia wetu wa *Buckreef,* na majengo haya yanakwenda kukamilika ndani ya mwezi wa tatu na kuanza kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshatoa maelekezo mahususi kwa Mkurugenzi kufuatilia kwa ukaribu katika ujenzi wa majengo haya ili akina mama wetu wanaojifungua zaidi ya 200 mpaka 250 kwa mwezi waweze kupata huduma hii ya afya ya msingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea. Sasa ninamwita Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, Mbunge wa Segerea, aulize swali lake.

Na. 91

**Hitaji la Kituo cha Afya Kata ya Buguruni**

**MHE. AGNESTA L. KAIZA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya katika Kata ya Buguruni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, Mbunge wa Segerea, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuboresha huduma za afya ngazi ya msingi kwa kujenga vituo vya afya kwenye kata za kimkakati. Buguruni ni miongoni mwa kata zilizopo Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam yenye wakazi wapatao 47,278. Kwa sasa hii wanapata huduma za afya katika Kituo cha

Afya cha Buguruni na Zahanati ya Bungoni umbali usiozidi kilometa mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2023/2024 Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ilifanya uthamini na kulipa fidia nyumba tatu kiasi cha shilingi milioni 245 kwenye eneo lenye ukubwa wa takribani mita za mraba 900 kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, eneo hilo halitoshelezi ambapo mwaka 2026/2027 Serikali kupitia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imefanya tathmini na kulipa fidia takribani nyumba saba ili kuongeza ukubwa wa eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Buguruni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026 Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imetenga jumla ya shilingi bilioni nne kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya katika Kata ya Kisuru. Ujenzi huu ni wa ghorofa na Halmashauri ya Jiji ipo katika maandalizi na utaratibu wa manunuzi ya kumpata mzabuni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnesta Lambert. Ahsante.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika swali langu la msingi, niliuliza suala zima la ujenzi wa kituo ndani ya Kata ya Buguruni, lakini kwa masikitiko makubwa naona Serikali imejikita kunijibu kuhusiana na ujenzi wa Kituo cha Afya ndani ya Kata ya Kisukuru. Pamoja na yote, ninalo swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kata ya Buguruni ni kitovu cha uchumi ndani ya Jimbo la Segerea, na kwa sababu hiyo kuna mwingiliano wa watu wengi ukiachilia mbali na hao wakazi 47 *plus*, jambo linaloonyesha wingi wa wananchi au wanaodumu ndani ya ile kata kwamba ni wengi zaidi ya 47,000 ambayo Serikali imetaja, sasa kwa umuhimu, ningependa kufahamu kwa uhakika kabisa, Serikali imetenga kiasi cha shilingi ngapi kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya ndani ya Kata

Buguruni, na ni lini hasa ujenzi huo utaanza? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali nyongeza la Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, Mbunge wa Segerea, kama ifuatavyo: Tayari Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imetenga jumla ya shilingi bilioni nne, kwa maana ya; kwanza, kulipa fidia na kuongeza eneo; pia kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya cha Kisukuru kilichoko ndani ya Kata ya Buguruni.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Mheshimiwa Getere, swali la dogo nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua hatima yake, hapa sasa itafika wakati wananchi watawaogopa kwenye mambo haya. Vituo vya mkakati vya afya vinavyojengwa na Serikali, maana yake mlisema mtapeleka shilingi milioni 250 na baadaye shilingi milioni 250 nyingine zitafuata. Sasa kama Kituo cha Mkakati cha Mihingo kinajengwa kwa shilingi milioni 250 na Serikali, halafu tukapata majibu kwamba sasa halmashauri itenge fedha ya kujenga hayo majengo. Sasa hapa kuna mchanganyiko, tunataka tuelewe lipi? Serikali Kuu ndiyo itajenga hivyo vituo kwa maana iliahidi kutoa hiyo shilingi milioni 250 kwa milioni 250; au imeahirisha tena, Mkurugenzi ndio atoe fedha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Bunge lako Tukufu lilipitisha kujenga vituo vya kimkakati katika majimbo yote nchini. Tayari tumeshapeleka shilingi bilioni 30 kujenga vituo vya afya vya kimkakati katika majimbo 120 na tayari tumeshaomba fedha nyingine kwa ajili ya kujenga vituo vya afya hivi katika majimbo mengine 94 na yale mengine mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ya kwamba tayari tumezielekeza halmashauri kuendelea kujenga majengo ya kutoa huduma katika hospitali hizi zote, lakini kama haitoshi, tutaendelea kuainisha halmashauri zile zenye uwezo na zile ambazo hazina uwezo ili tuweze kutoa fedha Serikali Kuu.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Wilson Mahera.

**MHE. DKT. WILSON C. MAHERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Butiama ina kata 18, lakini kati ya hizo, kata tisa tu ndiyo zenye vituo vya afya. Pia kuna kata kubwa kama vile Buruma, Buiregi, Bumangi, hazina vituo vya afya. Je, Serikali ina mpango gani kujenga kituo cha afya angalau kwenye kata ya Buruma yenye vijiji sita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Serikali inapongeza kwa maana ya kwamba tayari ana vituo tisa ndani ya kata 18, wakati huo kuna baadhi ya kata 14 ina vituo viwili. Kwa hiyo, ni juhudi kubwa ambayo imefanyika na tunaendelea kushirikia na Mheshimiwa Mbunge kuona ya kwamba tunazidi kuongeza vituo vya afya katika jimbo hilo.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, nilikuona Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Mbali na mpango wa Serikali wa kujenga vituo vya afya na hospitali, mmekuwa na mpango wa ukarabati wa hospitali ambazo zimechakaa. Hospitali ya Manyamanyama iliyopo kwenye Jimbo la Bunda Mjini ni hospitali ambayo majengo yake ni chakavu sana na inatoa huduma katika wilaya za jirani. Ni lini sasa mtatukarabatia Hospitali ya Manyamanyama?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika zile fedha ambazo Serikali ilitenga shilingi bilioni 102.08 za ukarabati wa hospitali hizi na hospitali hii aliyoiainisha Mheshimiwa Mbunge imo katika ukarabati huo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Emmanuel Khambay.

**MHE. EMMANUEL J. KHAMBAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kituo cha Afya cha Nangara kimejengwa na nguvu za wananchi na ni jengo moja tu la *OPD*. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa fedha nyingine ili kuweza kumalizia majengo mengine ili wananchi hao ambao wanafuata huduma umbali mrefu waweze kupata huduma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo hiki cha afya, kwanza tunawashukuru sana wananchi kwa kutoa nguvu zao na kuweza kuunga mkono juhudi za Serikali, lakini pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nimeshaongea na Mkurugenzi, na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI niendelee kumwelekeza Mkurugenzi kutenga fedha za ndani ili kukamilisha baadhi ya majengo katika kituo hiki baada ya kutoa *OPD* waendelee kutoa na huduma nyingine ambazo zinatakiwa kwenye kituo cha afya. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Mama Salma Kikwete.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mchinga halina hospitali hata moja, na lina vituo vya afya viwili. Kwa kuwa jimbo hili halina hospitali, je, ni lini Kituo cha Afya cha Kitomanga kitapandishwa hadhi ya kuwa hospitali, na kwa sababu mchakato wake wa kupandishwa hadhi ni wa muda

mrefu, nilikuwa ninaomba majibu ya Serikal, lini kituo hiki kitapandishwa hadhi na kuwa hospitali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mama Salma kwa kufuatilia afya za wananchi wake katika Jimbo la Mchinga. Pili, tayari tumeshachukua maombi ya kupandisha Kituo cha Afya Kitomanga kuwa hospitali ili kiweze kutoa huduma katika eneo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshakaa na wataalamu, na nimhakikishie Mheshimiwa Mama Salma Kikwete kwamba ndani ya muda mfupi tathmini itatoka na kuanza ujenzi na kukipandisha kituo hiki kuwa hospitali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tunaendelea. Sasa namwita Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge wa Kalenga aulize swali lake. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Mariam Kisangi.

Na. 92

**Ujenzi wa Barabara ya Tosamaganga – Igwachanya**

**MHE. MARIAM N. KISANGI K.n.y. MHE. JACKSON G. KISWAGA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa kipande cha barabara kutoka Tosamaganga hadi Igwachanya kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, Mbunge wa Kalenga, ambalo limeulizwa na Mbunge wa Temeke, Mheshimiwa Mariam Kisangi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Tosamaganga – Igwachanya ni moja kati ya barabara muhimu inayounganisha barabara kuu ya *TANZAM* na barabara ya Mkoa ya Iringa hadi Msembe yenye urefu wa kilometa 11. Mpaka sasa jumla ya kilometa 10.1 zimeshajengwa kwa kiwango cha lami na kilometa 0.9 iliyosalia inatarajia kujengwa katika mwaka 2025/2026 kupitia Wizara ya Ujenzi chini ya usimamizi wa *TANROADS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mkandarasi atakayetekeleza kazi hiyo ni *Plan Engineering Company* na mradi utatekelezwa kwa gharama ya shilingi milioni 829.88.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuuliza swali la nyongeza. Swali la kwanza, kwa kuwa changamoto ya wananchi wa Kalenga ni ukamilishwaji wa barabara hiyo. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha wanatafuta mpango wa muda ili barabara hiyo iweze kupitika na wananchi wa Kalenga waweze kufanya shughuli zao za kiuchumi kwa vizuri zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Changamoto inayowakuta Kalenga inalikuta pia Jimbo la Temeke katika eneo la Buza, barabara ya kutoka kwa Mama Kibonge, Mashine ya Maji mpaka Azimio. Barabara hiyo imekuwa ni changamoto, kwani unafika mahali magari hayapiti, wananchi wanashindwa kwenda hata kwenye kituo cha afya.

Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha wanatengeneza utaratibu wa muda ili barabara hiyo ipitike,

wananchi waendelee na shughuli za kiuchumi wakati tukimsubiri mkandarasi aingie na kutengeneza barabara hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, ukamilishwaji wa kipande cha barabara kilichobaki cha kilometa 0.9 unakwenda kufanyika kwenye mwaka huu wa fedha 2025/2026, na Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imetenga fedha, shilingi milioni 829 kwa ajili ya kazi hiyo na ujenzi utakwenda kuanza mara moja, kwa sababu fedha hiyo ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la nyongeza ambalo limegusa Wilaya ya Temeke, ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam na kwenye wilaya zote tano za Mkoa wa Dar es Salaam, Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inatekeleza Mradi wa *DMDP*2. Imetenga milioni 438 Dola za Kimarekani kwa ajili ya kuendeleza miundombinu yote ya msingi ikiwemo barabara aliyoitaja ndani ya Wilaya hiyo ya Temeke, na hivi sasa tuko kwenye hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo barabara ambazo tumeshawapa wakandarasi waendelee na kazi na zipo barabara ambazo tunaendelea na usanifu kwa ajili ya kutangaza zabuni na kuanza kazi mara moja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Geogrey Timoth, Mbunge wa Kawe, nilikuona.

**MHE. TIMOTH G. ANYOSISYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi, Jimbo la Kawe changamoto yetu kubwa ni miundombinu ya barabara. Barabara ya Ukwamani - Kwa Mapupu - Kanisani KKKT, Kata ya Kawe, lakini pia barabara ya Kwa Shokoronda na Mongela inayounganisha kata mbili; Kata ya Makongo na Mbezi Juu, na pia barabara inayotoka Bunju A inayopita Kata ya Mabwepande pamoja na Bunju ambayo inaenda hadi Kata ya Wazo pamoja na Kata ya Goba

zimekuwepo kwenye mpango wa kujengwa muda mrefu, lakini zimekuwa zikiahirishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanakawe wanataka kujua je, ni lini barabara hizi zitajengwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zote ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam likiwemo Jimbo la Kawe, barabara za Mheshimiwa Timoth ambazo ameziongelea miundombinu yote hii tutaitekeleza chini ya Mradi wa *DMDP2*. Tulianza na *DMDP1* tukajenga barabara nyingi sana, na hivi sasa tunakwenda kujenga mtandao wa barabara wa karibia kilometa 257 chini ya Mradi huu wa *DMDP2* na barabara hizo anazotaja kwa hakika zitafikiwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI. Sasa tunahamia Wizara ya Maji. Naomba nimwite Mheshimiwa Patrick Mwalunenge aulize swali lake. Kwa niaba yake namwita Mheshimiwa Ester Bulaya.

Na. 93

**Mradi wa Maji Mto Kiwira – Mbeya**

**MHE. ESTER A. BULAYA K.n.y. MHE. PATRICK A. MWALUNENGE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha Mradi mkubwa wa Maji kutoka chanzo cha Mto Kiwira ili kukomesha tatizo la maji Mbeya Mjini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

## TAARIFA

**MHE. SILVERY L. SALVATORY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. Mwuliza swali nipo. Ameitwa Patrick Mwalunenge, mimi ni Silvery Luboja Salvatory.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Misungwi...

**MWENYEKITI:** Sijakuruhusu Mheshimiwa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Hapana Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Patrick Mwalunenge, Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kutoa maji Mto Kiwira kwenda Jijini Mbeya. Miongoni mwa kazi zinazotekelezwa kupitia mradi huo ni pamoja na ujenzi wa dakio *(intake)* na mtambo wa kutibu maji lita milioni 117 kwa siku, ujenzi wa matanki mawili yenye uwezo wa kuhifadhi maji lita milioni 10 sambamba na ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 37.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa 48% na kwa mujibu wa mkataba unatarajiwa kukamilika mwezi Disemba, 2026 ambapo utanufaisha zaidi ya wakazi 890,000 wa Jiji la Mbeya na Mji wa Mbalizi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum Mbeya.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hiyo. Hili swali linahusu

wananchi wa Mkoa wa Mbeya. Ninashukuru sana kwa majibu ya Serikali. Huo Mradi wa Mbeya unasubiriwa na kutegemewa sana na wananchi. Nimekuwa nikiulizia mara nyingi sana hapa, ninategemea sana mimi pamoja na wananchi wa Mkoa wa Mbeya kwamba majibu hayo yatakuwa ni sahihi na watakwenda kupata mradi huo wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la nyongeza. Kwa kuwa mradi wa maji ambao ni mkubwa sana kwenye Wilaya ya Kyela unategemewa sana, lakini mpaka sasa hivi haujakamilika, je, tenki hilo litakamilika lini? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali nchini, na katika awamu iliyopita, zaidi ya miradi 3,714 yenye gharama ya shilingi trilioni 1.8 imekamilika, na sasa tunayo miradi 778 yenye gharama ya shilingi trilioni 1.3 inaendelea kutekelezwa ukiwemo mradi wa Kyela kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa nitaelekeza mamlaka husika wanaosimamia mradi huu kuhakikisha kwamba wanashirikiana na mkandarasi ili mradi huu uweze kukamilika kwa wakati, lakini pia Serikali tutaendelea kupeleka fedha kwa ajili ya mkandarasi kutokwama kwa namna yoyote ile ili lengo ni kwamba, wananchi wa Mkoa wa Mbeya na Kyela waweze kupata huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Mkoa wa Mbeya upatikanaji wa maji ni zaidi ya 90% na miradi inayoendelea ni zaidi ya shilingi bilioni 128 katika Mkoa wa Mbeya. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Waitara, nilikuona.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuruku sana. Kwa kuwa sasa hivi Wizara ya Maji ina

mitambo ya kuchimba visima, na kuna kata kama zile za Pemba, Mbogi, Gwitiryo na maeneo mengine hayana maji. Ni lini Serikali itapeleka wataalam wakatafiti kwenye vijiji katika Jimbo la Tarime Vijijini ili pale yanapopatikana maji chini ya ardhi watu wapate maji ya kunywa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wizara ya Maji tunampongeza sana, na kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Baada ya kununua mitambo ya kuchimba maji ndani ya kipindi cha miaka mitatu, tumeweza kuchimba visima 1,956. Hii ni rekodi ambayo haijawahi kutokea tangu tulivyoanza kuchimba visima 1,930 pale Mtukula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mheshimiwa Mbunge tutapeleka wataalamu wetu wa bonde, wataenda kufanya utafiti na baada ya hapo mitambo yetu ambayo ilinunuliwa na Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wataenda kutekeleza mradi huo ili wananchi wa Mheshimiwa Mbunge waweze kupata huduma ya majisafi na salama.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Nilikuona Mheshimiwa Dickson Villa.

**MHE. DICKSON N. LUTEVELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali. Kwanza kabisa niishukuru Serikali kwamba Halmashauri ya Mji wa Mafinga ni moja kati ya miji ambayo ilipata Mradi wa Maji wa Miji 28 na mradi huu ilikuwa ukamilike mwezi Juni mwaka uliopita, lakini mpaka sasa hivi mradi huu uko 28% tu ya utekelezaji wake. Ninaomba kauli ya Serikali, je, ni lini mradi huu utakamilika ili wananchi wa Mafinga waweze kupata maji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana kaka yangu Mwenezi wa Wilaya na Mbunge

wa Jimbo hilo ambaye ameanza kwa kasi kubwa sana, na mwezi mmoja tu uliopita nilikuwa naye kwenye ziara katika jimbo lake, na tulipitia baadhi ya miradi, na mradi ambao ameuongelea ni mradi unaotekelezwa na *Jandu Plumber*s ambapo ni kweli ulikuwa unasuasua, lakini tuliwaita wakandarasi tukakaa tukakubaliana warudi *site* waweze kuendelea kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaamini kwamba kwa kadiri fedha ambavyo zitakuwa zinapatikana tutahakikisha tunamwezesha mkandarasi aweze kukamilisha huu mradi kwa wakati. Ninashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Devotha Daniel, swali dogo la nyongeza.

**MHE. DEVOTHA D. MBURARUGABA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Ni lini Wilaya ya Kyerwa itaweza kupata maji ya uhakika? Kwani mradi ambao uko Wilaya ya Kyerwa unatekelezwa kwa kusuasua. Nilitaka kujua shida ni mkandarasi au kuna mkakati mwingine?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kuna baadhi ya miradi ambayo inaendelea kutekelezwa lakini kuna mingine ambayo inasuasua. Nimwelekeze *RM* Mkoa wa Kagera aende Kyerwa leo akafanye tathmini na kujiridhisha kuna changamoto gani, ili atuletee kwa ajili ya kuchukua hatua stahiki kulingana na uzembe ambao unaweza ukasababishwa na wakandarasi, na kama siyo mkandarasi, tujue kwamba tatizo liko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea, sasa ninamwita Mheshimiwa Salvatory Silvery Luboja, Mbunge wa Misungwi, aulize swali lake.

Na. 94

**Ujenzi wa Mradi wa Maji Ilujamate-Buhingo**

**MHE. SILVERY L. SALVATORY** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza Mradi wa Maji Bonde la Lujamate – Buhingo ambao umesimama kwa muda mrefu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Silvery Luboja Salvatory, Mbunge wa Jimbo la Misungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maji wa Ilujamate – Buhingo uliopo Wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza unahusisha ujenzi wa matanki matatu yenye uwezo wa kuhifadhi maji lita 800,000, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 67, sambamba na ujenzi wa vituo 60 vya kuchotea maji. Utekelezaji wa Mradi huo umefikia wastani wa 40% na unalenga kunufaisha zaidi ya wananchi 84,000 waishio kwenye vijiji 16 vya Wilaya ya Misungwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha miradi hiyo inayotekelezwa kwa kupelekewa fedha kadiri zinavyopatikana katika mwaka huu wa fedha 2025/2026 ili ikamilike na kuanza kutoa huduma iliyokusudiwa ukiwemo Mradi wa Maji Ilujamate – Buhingo.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Silvery Luboja.

**MHE. SILVERY L. SALVATORY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa wananchi wa vijiji 16 vya Gukwa Buhunda, Mwagimagi, Kifune, Busongo, Nyambiti, Kabale, Buhingo, Seke, Songiwe, Mwasagela, Mbalama, Nyamayinza, Gulumungu, Ng'hamve pamoja na Itogwang'holo viko kwenye

Mradi wa Maji wa Ihelele unaopeleka maji Mikoa ya Shinyanga na Tabora, na unaanzia kilometa *zero* kutoka kwenye chanzo cha maji; Tangu uzinduliwe mwezi Juni, 2009 wananchi hawa hawajawahi kupata maji ilhali maji yananyewa Sikonge. Je, sasa Serikali haioni ni wakati umefika wananchi hawa na wao waweze kupewa maji kwa haraka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa maji ni uhai, je, Serikali ina mkakati gani wa dharura wa kuwapatia wananchi hawa maji kwa haraka ili kuokoa afya zao? Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salvatory, Mbunge wa Misungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kwenye upande wa Misungwi Serikali imefanya kazi kubwa sana. Upatikanaji wa maji wa sasa wa Misungwi ni 68%, lakini Serikali imetekeleza zaidi ya miradi 15 na yenye gharama ya shilingi bilioni 15.6, lakini miradi inayoendelea kwa sasa ni nane yenye gharama ya shilingi bilioni 69. Hii ni kazi kubwa inayofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Jimbo la Misungwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kwamba kazi ya Serikali ni kuhakikisha kwamba vijiji vyote vinapata huduma ya majisafi na salama, lakini kati vijiji 94 vyote tayari vina maji na vijiji vinane ndivyo ambavyo bado tunahakikisha kwamba mradi huu unaoendelea utakapokamilika pamoja na vile vijiji 16 vyote vitapata huduma ya majisafi na salama. Tunafahamu kwamba maji ni uhai, lakini maji ni uchumi. Tunafahamu kwa kuwawezesha wananchi wa Misungwi wataweza kufanya shughuli zao za kiuchumi, lakini pia wataweza kutumia majisafi na salama kwa ajili ya kunywa, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Olelekaita.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi. Mheshimiwa Naibu Waziri Mradi wa Nchinilai – Engusero umechukua muda mrefu sana na unasuasua sana. Ni lini Naibu Waziri yuko tayari, kwa siku ambazo siyo nyingi sana tutembelee mradi huu ili tupate majibu ya uhakika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Olelekaita, na hakika tunapokuwa katika ziara jimboni kwake anatupatia ushirikiano mzuri sana, na pia tunapohitaji taarifa za maendeleo ya miradi yetu ndani ya jimbo lake anatupatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hivyo, nipo tayari kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji kwenda kutembelea mradi huu na kuupa *push* ili uweze kukamilika na wananchi wake wa Kiteto wapate huduma ya majisafi na salama, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Bakari Shingo, swali dogo la nyongeza.

**MHE. BAKARI B. SHINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo langu la Ukonga kuna Mradi wa Yangeyange, ambao ni mategemeo makubwa kwa wananchi wa Kata ya Pugu, Buyuni, Chanika na Zingiziwa, na pia ni mradi ambao unaonekana umekamilika, lakini hatujawahi kunufaika nao kwa sababu mara nyingi unaripotiwa kuwa na *breakdown*. Ninaomba nitambue shida ni viwango vya mabomba vilivyotumika pale viko chini, ama utalaamu ni mdogo, ama ni nini? Maana nilikuwa ziarani hata jana, bado tuna shida na tulikuwa tunaambiwa mradi ule una tatizo. Ninaomba nipate ufafanuzi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Bakari, kwa muda mfupi amekaa jimboni kwake, lakini ameshabaini baadhi ya changamoto hasa zinazolenga akina mama. Sisi kama Serikali tutaendelea kufanya kazi na Waheshimiwa Wabunge ili kuendelea kutatua changamoto za wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kupokea changamoto hii, na pia ninamwelekeza Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji atume timu iende kuukagua mradi huo, ije na tathmini ya nini kimefanyika, na wapi kuna tatizo? Kama kuna tatizo katika utekelezaji wa mradi, tuchukue hatua kulingana na changamoto ambazo zitabainika baada ya timu hiyo kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo ninakuhakikishia kwamba tutampatia jibu Mheshimiwa Mbunge kulingana na taarifa itakayopatikana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, sasa ninamwita Mheshimiwa Dkt. Wilson Mahera Charles, Mbunge wa Butiama, aulize swali lake.

Na. 95

**Uhitaji wa Maji Katika Kata za Jimbo la Butiama**

**MHE. DKT. WILSON C. MAHERA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha kusambaza maji Kata za Bisumwa, Bukabwa, Nyankanga, Butuguri, Bwiregi, Buruma, Kyanyari, Buhemba, Mirwa na Kikirango?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Wilson Mahera Charles, Mbunge wa Jimbo la Butiama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha ujenzi wa Mradi mkubwa wa Maji ya Ziwa Victoria wa Mugango – Kiabakari - Butiama uliogharimu zaidi ya shilingi bilioni 70 na unanufaisha wananchi kwenye Kata za Wilaya za Butiama na baadhi ya maeneo ya Wilaya za Bunda pamoja na Musoma Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa mradi huo umeanza kutoa huduma kwenye vijiji 22 vinavyopatikana kwenye kata saba za Wilaya za Butiama na Musoma Vijijini. Aidha, kazi ya upanuzi wa mradi huo inaendelea kwa awamu kadiri fedha zinavyopatikana ili kuweza kufikisha huduma ya majisafi na salama kwenye maeneo ambayo hayajafikiwa na huduma hiyo ikiwemo baadhi ya vijiji vya Kata za Bisumwa, Bukabwa, Nyankanga, Butuguri, Bwiregi, Buruma, Kyanyari, Buhemba, Mirwa pamoja na Kikirango.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Wilson Mahera Charles, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. WILSON C. MAHERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kutuletea mradi mkubwa wa maji wenye uwezo mkubwa sana wa kuweza kuzalisha lita milioni 35 kwa siku, lakini kwa sasa ni lita milioni 17. 5 kwa siku, ila mradi huo kwa sasa unatoa lita milioni tatu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili kuweza kusambaza maji katika vijiji ambavyo vinausubiri kwa hamu kubwa, kuna miradi miwili ambayo iko Wizarani ya *4.8 billion* na *3.5 billion.* Je, ni lini Wizara itatoa kibali ili miradi hiyo iweze kutangazwa wakandarasi wapatikane? Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa vile mradi huu ni mkubwa sana na utafika kwenye Kata ya Mirwa, tunayo Kata ya jirani ya Sirorisimba ambayo iko karibu na Wilaya ya Serengeti na Kijiji cha Baranga Kata ya Buswahili hawana mradi wa maji. Je, Wizara ina mkakati gani wa kuanza kuandaa mradi ili vijiji hivyo navyo vipate maji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge, nilipata ziara katika Jimbo lake na alikuwa kwenye safari zake, lakini aliamua kuahirisha na kurudi jimboni kwake ili tuweze kufanya ziara kwa pamoja. Ninampongeza sana kwa namna ambavyo anaendelea kuguswa na changamoto za wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa maji ndani ya Jimbo lake ni 78%, lakini tunayo miradi miwili inayoendelea yenye gharama ya shilingi bilioni tano lakini vilevile, mradi huu ambao Mheshimiwa ameongelea, ni mradi ambao unatokana na ahadi za Viongozi wa Kitaifa. Ni mradi ambao sisi kama Serikali na sekta ya maji ni lazima mradi huu utekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mradi huu ninaufahamu vizuri kwa sababu nina picha nzima ya Butiama. Kikubwa tu ni kwamba ile taarifa ambayo amesema, ilishafika Wizarani, ninaomba nimhakikishie kwamba haijafika mpaka sasa, lakini tumeshawasiliana na watu wetu ili waweze kuileta kwa haraka ili tuhakikishe kwamba tunachukua hatua za haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi huu wa Buhemba utakapotangazwa, utafika mpaka katika eneo la Sirorisimba ambapo utaenda mpaka kwenye Kata ya Mirwa kule. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge aondoe shaka, Serikali itakapotoa kibali na mradi ukatekelezwa maeneo yote hayo yatapata huduma ya majisafi na salama. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante, nilikuona Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Wananchi wa Mji wa Tarime wana adha kubwa sana ya maji, na tegemeo lao kubwa; na wanaishukuru Serikali kwa Mradi mkubwa wa Maji Ziwa Victoria wa shilingi bilioni 134 lakini mradi huu ulianza mwaka 2022 na unatarajiwa kukamilika Septemba mwaka huu. *So far* wamepeleka shilingi bilioni 24 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kujua mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba hizi shilingi bilioni 110 zinaenda ili mradi huu ukamilike ndani ya muda na kuweza kupunguza adha ya maji kwenye Mji wa Tarime? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kabisa kwamba Mheshimiwa Esther Matiko ameendelea kupigania sana wananchi wake wa Tarime Mjini, na pia ameendelea kuhakikisha kwamba mradi huu anausukuma ili uweze kupata fedha na uweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba mradi huu unaenda kuwa mwarobaini, lakini mkakati wa Serikali sasa wa namna gani mradi huu unaenda kukamilika, ni kupunguza utitiri wa kutangaza miradi mingi wakati tuna miradi ambayo bado haijakamilika na haijaanza kutoa matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa tunaenda kuhakikisha kwamba badala ya kutangaza miradi mingi na kuzigawanya fedha ambazo zingeenda kukamilisha miradi kama hii, sasa tunaenda kuweka hitimisho katika utaratibu wa namna hiyo, na mkakati wetu ni kumaliza miradi viporo. Tukishamaliza baadaye tutaendelea na miradi mingine ambayo tutaweza kuifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, mradi huu ni kipaumbele kwa Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, na tuna uhakika mradi huu utakamilika na wewe mwaka 2030 utarudi, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Phillipo Mulugo.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri wa Maji alifanya ziara kwenye Mkoa wetu wa Songwe na alipofika pale wataalamu wa jimbo langu walimpatia andiko au maombi ya barua ili kuunganisha miradi ya Kijiji cha Muheza, Manda, Rukwa, Namkukwe, Gua Songambele na Halyongo liwe

andiko moja tuweze kupata mkandarasi, na alichukua barua hiyo lakini mpaka sasa hakuna majibu. Ni lini tutapata barua hiyo ili mkandarasi aweze kupatikana kuanza kujenga miradi ya vijiji vitano kwa thamani ya shilingi bilioni 1.5?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa nikiri nilifika jimboni kwa kaka yangu Mheshimiwa Mulugo na tulifanya ziara, na tulipokea andiko hilo, lakini ilikuwa tayari ndani ya bajeti ya fedha ambayo inaelekea mwishoni, na sasa tuko kwenye mchakato wa kuanzisha maandalizi ya kuelekea kwenye bajeti ya 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kuwa tutafanya tathmini vizuri na kujiridhisha na tutamshirikisha Mheshimiwa Mbunge, na tukisharidhika sasa kwamba tunaenda kutekeleza kwa namna gani, basi tutauingiza kwenye bajeti ya mwaka 2026/2027 ili ukatekelezwe katika vijiji hivyo vitano na wananchi wake wapate huduma ya majisafi na salama. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji. Tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi. Sasa ninamwita Mheshimiwa Mwinyi Jamal Ramadhani, Mbunge wa Bumbwini, aulize swali lake.

Na. 96

**Bandari ya Dsm Kushindwa Kupokea Meli Nyingi**

**MHE. MWINYI JAMAL RAMADHAN** aliuliza:-

Je, kwa nini Bandari ya Dar es Salaam inashindwa kupokea meli nyingi kwa wakati mmoja?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upokeaji wa meli katika gati za bandari zote duniani hutegemea mambo kadhaa yakiwemo urefu wa gati kwa meli husika, ukubwa wa yadi ya kuhudumia shehena, kina cha lango la kuingilia meli, vifaa vya kuhudumia shehena, mifumo ya kuhudumia meli na shehena iliyo fungamanishi, aina na ubora wa barabara na reli zinazoingia na kutoka Bandarini, kasi ya ongezeko la shehena na mahitaji ya meli, pamoja na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Bandari ya Dar es Salaam inazo gati 13 zenye uwezo kuhudumia meli za aina ya *Post Panamax* ambazo ni kubwa katika ukanda unaohudumiwa na Bandari za Afrika Mashariki, Kati na Kusini. Hata hivyo, idadi hii ya gati bado ni ndogo ukilinganisha na kasi ya ongezeko la meli na shehena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kutokana na ongezeko la meli na shehena kwa ujumla, Bandari ya Dar es Salaam inaendelea na mipango kuongeza idadi ya gati, vifaa na mifumo stahiki ili kukabiliana na hali hiyo. Kwa kuanzia, ujenzi wa gati la meta 500 katika Bandari ya Dar es Salaam umeanza sambamba na maandalizi ya ujenzi wa gati nyingine nne (gati namba 12-15) ambapo Serikali kupitia Wizara ya Fedha na *TPA* imeanza mazungumzo ya awali na Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata mkopo nafuu kugharamia ujenzi wa gati hizo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Maswali ya nyongeza, Mheshimiwa Jamal Ramadhan.

**MHE. MWINYI JAMAL RAMADHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa heshima hii ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa bandari hii ni bandari tegemezi kwa wafanyabiashara wetu kutoka visiwani na bara na inaleta tija sana kwa uchumi wa nchi yetu, swali langu lipo hapa, ni mara ngapi tangu nchi yetu imepata uhuru bandari hii imefanyiwa utanuzi ama ujenzi wa kuongezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la nyongeza, katika jitihada za Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

kukuza uchumi wetu wa nchi na kuweka mkazo katika eneo hili, hatuoni sasa suluhisho la kuongeza uchumi wa nchi yetu ni kwa kutengeneza Bandari ya Bagamoyo? Sambamba na hilo, tujue, je, Bandari ya Bagamoyo kwa sasa imefikia wapi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Jamal Ramadhan kwa uzalendo wake mkubwa wa kufuatilia miundombinu ya kimkakati katika Taifa letu hususan roho ya nchi ambayo ni bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia uhuru kwa kweli takwimu *specific* nitashindwa kuzisema hapa lakini ni mara ngapi Serikali imefanya maboresho? Ni mara nyingi katika kuhakikisha na kuona kwamba bandari hii inaongezewa uwezo. Pamoja na mambo ambayo yamefanyika huko nyuma, bado inaendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tumeboresha gati namba sifuri mpaka namba saba ambapo imeongeza uwezo wa bandari yetu kuhudumia. Pia tumeongeza kina cha bandari yetu ili iweze pengine kuwa na urefu zaidi kwenda chini pamoja na kuongeza upana wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tuna miradi mingine inayoendelea bandarini, kama vile kuunganisha reli kwenye bandari yetu, kuhakikisha kwamba tunajenga Gati Namba 12 mpaka 15, kama nilivyozungumza kuhakikisha kwamba, tunawezesha Kituo chetu cha Kurasini kinakuwa na uwezo mkubwa wa kuhudumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, tayari kuna mradi mkubwa ambao uko 32%, mradi wa kujenga matenki 15 yenye uwezo wa kuhifadhi mita za ujazo wa mafuta 378. Maboresho yote hayo yana lengo moja tu la kuhakikisha kwamba, bandari yetu inazidi kuimarisha uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, swali lake la pili la nyongeza ametaka kufahamu kuhusiana na ujenzi wa bandari yetu ya Bagamoyo ya Mbegani. Ni kweli kabisa ukiangalia uwezo wa mahitaji yetu sasa ya mzigo kutokana na diplomasia nzuri ya Rais wetu, na jinsi anavyosimamia Uchumi, unaona kabisa Bandari ya Dar es Salaam hata ungeifanyia maboresho kiasi gani inazidi kuzidiwa. Hivyo basi, Serikali imefanya maamuzi ya kuboresha au kuanza ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo, Mbegani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza, tumeshamaliza usanifu. Tayari tumeanza taratibu kwa ajili ya kuanza ujenzi, ili tuanze na kilomita moja, kwa ajili ya kupata kilomita 1.3, kupata gati ambayo itawezesha sasa meli kubwa ambazo kwa sasa haziwezi kutua kwenye Bandari ya Dar es Salaam, ambayo itakuwa inaweza kufika pale. Kwa kweli, bandari ile ikianza kufanya kazi itakuwa ndiyo bandari kubwa kuliko zote kwa ukanda wetu wa Afrika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Regina Malima.

**MHE. DKT. REGINA C. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Nina swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri kuhusiana na Bandari ya Nansio katika Kisiwa cha Ukerewe. Bandari hii pia, imechakaa, imechoka, haijawahi kufanyiwa ukarabati tangu uhuru. Wakati mwingine hali ya hewa ikiwa ni mbaya meli pia zinapata shida kuweza kupaki. Kwa hiyo, ninaomba kujua, ni lini Serikali itafanya ukarabati wa Bandari hii ya Nansio katika Kisiwa cha Ukerewe? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka anapoingia madarakani Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwaka 2021, takribani bandari 80 zilikuwa zinatambuliwa na kurasimishwa. Kutokana na umuhimnu wa sekta ya bandari, Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo maalumu na mahususi kwa Mamlaka ya Bandari Tanzania *(TPA)* na Wizara ya Uchukuzi kwanza, tufanye

urasimishaji. Tumekamilisha urasimishaji na bandari zimeongezeka mpaka 142.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya pili ni kuanza kutafuta fedha, kuboresha bandari moja baada ya nyingine. Namwomba Mheshimiwa Malima awe na Subira, Bandari ya Nansio ni moja kati ya bandari muhimu kwenye Taifa letu. Tutakwenda kuifikia pindi fedha zitakapokuwa zimepatikana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, tunaendelea. Sasa ninamwita Mheshimiwa Kiza Hussein Mayeye, Mbunge wa Kigoma Kaskazini, aulize swali lake.

Na. 97

**Kurejesha Bandari za Kibirizi na Ujiji**

**MHE. KIZA H. MAYEYE** aliuliza: -

Je, Serikali imechukua hatua gani za kurejesha Bandari za Kibirizi na Ujiji zilizokumbwa na madhara ya Mabadiliko ya Tabianchi na kujaa maji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TPA* imefanya tathmini ya madhara yaliyosababishwa na athari za mabadiliko ya tabianchi, hususan kuongezeka kwa vina vya maji katika Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa ambapo baadhi ya Bandari kama Ujiji na Kibirizi zimeathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa *TPA* imeanza kazi za ukarabati na kuweka miundombinu mbadala, ili Bandari hizo za Kibirizi na Ujiji zirejee kufanya kazi kama ilivyokuwa awali. Aidha, kazi zinazoendelea zinatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Juni, 2026.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mayeye, maswali ya nyongeza.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Ujiji na Kibirizi zina mahusiano ya moja kwa moja na Bandari Ndogo ya Kagunga, ambayo iko mpakani mwa Burundi na Tanzania. Sasa nataka kupata majibu ya Serikali, ni lini mtakamilisha miradi fungamanishi, kama Barabara ya Mwandiga - Bubango - Chankere mpaka Kagunga, ambayo itakuwa kitovu cha kuweza kuunganisha nchi ya Burundi na Kongo na kuweza kuongeza uchumi katika Jimbo la Kigoma Kaskazini, Kigoma na Tanzania kwa ujumla?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Serikali imekuwa ikihusisha sekta binafsi katika uwekezaji wa bandari, kwa mfano Kigoma, Dar es Salaam na maeneo mengine. Taifa limenufaika na nini katika kushirikisha sekta binafsi? Ninataka majibu ya Waziri, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Mayeye kwa maswali yake na uzalendo kwa Taifa lake, jinsi anavyosimamia miundombinu na kuunga mkono kazi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ni Wabunge wachache wanaweza kuelewa mchango ambao Mheshimiwa Rais anautoa katika Taifa letu. Kwa muda mrefu Wabunge kutoka Mkoa wa Katavi, Rukwa na Kigoma wamepiga kelele kutaka Serikali zote kuanzia ya kwanza mpaka sasa ziboreshe Ziwa Tanganyika kwa sababu ni uchumi, ni maisha, ni ulinzi na ni ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumtaarifu Mheshimiwa Mayeye, na yeye ni shahidi kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ana miaka minne tu, lakini mambo aliyoyafanya kwenye eneo hilo ni ya kipekee. Ukiacha *SGR* anayojenga kuipeleka mpaka Kigoma ili kuhakikisha kwamba Kigoma inafunguka; ukiacha meli anazokarabati ikiwemo *MV Liemba* ambayo inakaribia 40%, *MV Mwongozo* ambayo ipo kwenye

mpango wa Manunuzi, *MT Sangara* na meli ya mafuta inayofanya kazi; ukiacha kiwanda cha meli kinachojengwa pale Katabe, Kigoma, bado Mheshimiwa Dkt. Samia hajawaacha Wanakigoma pamoja na Ziwa Tanganyika kwa ujumla kwa sababu, ni yeye ameidhinisha mradi mkubwa wa maboresho wa Bandari tatu za Kibirizi, Kigoma na Ujiji na akapeleka fedha, shilingi bilioni 32.5 ambazo zimeboresha maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, Serikali hii kwa kutambua umuhimu wa Bandari hiyo ya Kagunga ilipeleka fedha shilingi bilioni tatu na kidogo, na tayari tumekamilisha pale gati ya mita 50. Kama nakubaliana naye, ni kweli kabisa, ili Mradi wa Bandari ya Kagunga uweze kuwa na tija kwa Taifa letu, na wananchi wa Kigoma ambao ninaamini wanafuatilia, ni lazima ufungamanishwe na miradi ya soko pamoja na barabara aliyoitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kulitambua hilo, tayari imeanza kwa upande wa soko. Wenzetu wa TAMISEMI wametenga shilingi bilioni 2.3 na wamemlipa mkandarasi shilingi milioni 222 kuhakikisha kwamba, soko linajengwa na faida ya soko lile inakwenda kufungua bandari. Watakuja wenzetu wa Congo, watakuja watu wa Burundi, watakuja eneo lile kwenye bandari na baadaye tutafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, barabara hii aliyoitaja ya Mwandiga Chankere, Mwamgongo pamoja na Kagunga yenye urefu wa kilomita takribani 65, Serikali imeanza kufanya kazi, imejenga kilomita 18, ili bandari ile iweze kufunguka. Namwahidi Mheshimiwa Mbunge awe na subira na Wabunge wote wa Kigoma. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anakwenda kuimarisha na kuendelea kuleta mapinduzi makubwa kwenye Mkoa wa Kigoma.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa majibu yako Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea. Sasa namwita Mheshimiwa Florence Laurent Kyombo, Mbunge wa Missenyi, aulize swali lake.

Na. 98

**Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Kyabajwa**

**MHE. FLORENT L. KYOMBO** aliuliza: -

Je, lini Uwanja wa Ndege wa Kyabajwa utaanza kujengwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza kutekeleza Mradi wa Kiwanja Kipya cha Mkoa wa Kagera kwa kuingia mkataba na mtaalamu elekezi, ili kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa kiwanja hicho kinachotarajiwa kujengwa katika Eneo la Kyabajwa. Mtaalamu elekezi anatarajiwa kukabidhiwa eneo la kazi na kuanza kazi ndani ya robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2025/2026 (Januari – Machi, 2026).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imepangwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2026. Baada ya hapo, hatua za utekelezaji wa mradi huo zitaanza.

**MWENYEKITI:** Maswali ya nyongeza, Mheshimiwa Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Naishukuru Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, wakati wa kampeni yake aliwaahidi wananchi wa Misenyi na Mkoa wa Kagera kwamba ndani ya siku 100 ataanza utakelezaji wa mradi huo, na sasa ni ushuhuda, kutokana na majibu ya Serikali ndani ya siku 100 mtaalamu mwelekezi amefika *site* na kuanza upembuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa hatua hiyo, chini ya Wizara ya Uchukuzi, chini ya Waziri, Mheshimiwa Prof. Mbarawa na Naibu Waziri, Mheshimiwa David Kihenzile, kwa kazi nzuri wanayoifanya. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, uwanja huo ni wa Kimataifa, na utainua uchumi mkubwa Mkoa wa Kagera na Jimbo la Misenyi kwa ujumla, je, ni mkakati gani ambao Wizara ya Uchukuzi inaweza kuuratibu pamoja na halmashauri kupima na kupanga maeneo yote yanayozunguka eneo la uwanja huo, ili kuweza kuleta taswira nzuri na kuwainua wananchi hao kiuchumi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Kwa kuwa, uwanja huo utakuwa wa kimkakati ukihudumia nchi za Maziwa Makuu, ni mwongozo upi ambao Serikali inautoa ili tuweze kujiandaa kwa shughuli za kiuchumi, ili uwanja huo sasa ukianza uwe na tija kubwa kwa wananchi wa Misenyi, Mkoa wa Kagera na Taifa kwa ujumla? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Kyombo kwa kutambua kazi nzuri ya Mheshimiwa Rais Samia, ambaye ndani ya siku 100 aliahidi na ameanza kutekeleza kwa ajili ya kujenga uwanja mkubwa wa Kyabajwa. Ninakubaliana naye, Serikali iko tayari kushirikiana na halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba halmashauri waweke mkakati huo na yeye mwenyewe Mbunge akiwa ni sehemu ya halmashauri, ili tupime maeneo yale yawe vizuri, wananchi wasivamie kwa sababu, uvamizi unatokea pale ambapo halmashauri ilikuwa inajua kwamba kuna jambo zuri linakuja, lakini haikuweka mkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba waanze kuweka mpango huo mzuri. Sisi kama sekta, kwa maana ya Wizara ya Uchukuzi, chini ya Mheshimiwa Prof. Makame Mbarawa, pamoja na *TAA,* tuko tayari kushirikiana na nyie kuhakikisha kwamba, tunaweka jambo hili vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, amezungumza kuhusiana na tija ya uwanja huo. Natoa wito na rai kwa wananchi pamoja na viongozi Mkoa wa Kagera kwamba, mradi huu ni mkubwa sana,

utakwenda kuunganisha nchi yetu na mikoa ya jirani, utakwenda kuunganisha nchi yetu na mikoa ya jirani, utakwenda kuunganisha nchi yetu na nchi jirani. Ni vyema wakaanza kuchangamkia fursa za kiuwekezaji na tuwaombe wananchi wetu walinde ardhi yao, wasiuzeuze tu, maana hii inayokuja sasa ni neema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia anawaletea neema. Itakuwa ni jambo la kusikitisha baadaye ardhi yote imechukuliwa na watu wa nje, wao hawana ardhi. Hivyo basi, tuchangamkie fursa, tutazame cha kufanya kuhakikisha kwamba, uwanja huu unakwenda kuwa na tija kubwa kwa wananchi na Taifa letu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Yagi Kiaratu, uliza swali dogo la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. YAGI M. KIARATU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Singida wana hamu sana ya kupata usafiri wa anga. Pamoja na kuchagiza shughuli za kiuchumi, usafiri na usafirishaji Singida ni katikati ya nchi. Singida ni jirani na Dodoma, ikitokea rubani akashindwa kutua Dodoma, mji wa karibu kutua ni Singida; lakini kwa sababu, Singida ni Katikati, itakuwa kiungo kizuri cha usafirishaji ndani ya nchi. Ninaomba kauli ya Serikali, ni lini sasa Singida watajengewa uwanja wa ndege? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Mbunge wa Singida Mjini na Mheshimiwa Mstahiki Meya Mstaafu kwa ufuatiliaji wake wa uwanja huu mzuri na muhimu kwa Taifa letu. Kama alivyoeleza yeye mwenyewe, uwanja huu ulijengwa miaka ya 1950 na Serikali imekuwa ikiutumia, lakini kwa kweli, kiwango chake kiko chini ni wa changarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na maombi ya Waheshimiwa Wabunge na wakati mwingine viongozi, Serikali

imepokea kilio hicho na imeanza kufanya usanifu. Ninamhakikishia, tunakwenda kujenga Uwanja wa Singida na mwaka wa fedha 2026/2027 tunaingiza kwenye bajeti. Tunaenda kuongeza *runway* kutoka 1,000 mpaka 2,000, tunaweka lami pamoja na kuhakikisha kwamba, tunaweka taa, ili uwanja utumike mchana na usiku.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante. Swali kwa kifupi sana, Mheshimiwa Mary Masanja.

**MHE. MARY F. MASANJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Uwanja wa Kimataifa wa Mwanza ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu, hususan Mkoa wa Mwanza. Uwanja huu mpaka sasa haujakamilika na ukizingatia ni wa muhimu kwa kuwa, tuko karibu sana na hifadhi ya Serengeti, ni kilomita 130 tu. Je, ni lini sasa Serikali itakamilisha uwanja huu, ili angalau wananchi wa Mkoa wa Mwanza waanze kufaidika na uchumi unaotokana na masuala ya utalii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nitakwenda kujibu kwa kifupi kama ulivyonielekeza. Ninampongeza Mheshimiwa Mary Masanja kwa kutambua umuhimu wa uwanja huu ambao kimsingi ndiyo kitovu cha Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kulitambua hilo, moja, imeanza mchakato, kwa ajili ya kuboresha jengo la abiria; na pili, imeanza na *documentation* ili kuufanya kuwa wa Kimataifa pamoja na mambo mengine, kama vile kumaliza mgogoro wa wananchi ambao walivamia eneo la pembeni ili uweze kuwa na ulinzi. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inalitambua hilo na itaongeza kasi kuhakikisha kwamba, inauboresha na kuufanya uwanja huu kitovu ndani na nje ya nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Jafari Chege, karibu, uliza swali lako kwa kifupi sana.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nataka nijue ni lini Uwanja wa Ndege wa Musoma, kama kielelezo cha Mkoa wa Mara, utakamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua umuhimu wa Mkoa wa Mara, ilianza ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Mara. Pale Serikali inajenga *runway,* kwa maana ya njia ya kuruka na kutua ndege, pia inajenga na majengo mbalimbali. Tayari *runway* imekamilika, tunakwenda kumalizia majengo yaliyobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema ninaomba kurejea kauli yangu niliyoitoa siku tano au sita kwamba, kuanzia mwezi ujao au unaofuatia, Serikali ina mpango wa kuanza kufanya *testing* ya ndege za Shirika letu la Ndege *ATCL* kwenye viwanja vitatu; Uwanja wa Musoma, Shinyanga na Sumbawanga. Hii ni kuthibitisha dhamira ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba, ameamua kuitendea haki nchi hii kwenye sekta ya anga.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi. Sasa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Ninamwitae Mheshimiwa Jesca David Kishoa, Mbunge wa Iramba Mashariki, aulize swali lake.

Na. 99

**Ujenzi wa Barabara ya Iguguno – Nduguti**

**MHE. JESCA D. KISHOA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Iguguno - Nduguti - Sibiti (kilometa 89) na Barabara unganishi za daraja la Mto Sibiti (kilometa 24.83)?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza mipango ya ujenzi wa Barabara ya Iguguno – Nduguti – Sibiti yenye urefu wa kilometa 84.95 ambapo upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika. Ili kurahisisha utekelezaji wa mradi huu, Serikali imepanga kuijenga kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa barabara unganishi za Daraja la Mto Sibiti, Mkandarasi amepatikana, na taratibu za kuanza kazi za ujenzi zinaendelea. Aidha, Serikali inaendelea na taratibu za manunuzi ya kumpata mkandarasi, kwa ajili ya ujenzi wa Sehemu ya Nduguti Mjini yenye urefu wa kilometa 10. Baada ya hatua za manunuzi kukamilika na mkandarasi kupatikana, kazi za ujenzi zitaanza, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kishoa.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru, pamoja na majibu ya Serikali, lakini Wilaya ya Mkalama ndiyo Wilaya pekee katika Mkoa wa Singida, ambayo, ili ufike makao makuu ni lazima upigwe na vumbi la kutosha. Ninaomba, ili kuwaepusha wananchi na adha hii, kwa sababu shughuli za kijamii zinadorora na hata za kiuchumi, na wakati mwingine wananchi wa kule wanapoteza maisha, ninaomba *commitment* ya Serikali, *very seriously,* barabara hii inaanza kujengwa lini, kama ambavyo imekuwa ikiahidiwa mara zote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu sasa wa kupeleka fedha za kutosha kwenye maeneo ambayo yana *geographical features* zile ngumu, kama milima, mabonde na mito, kwa ajili ya wao kujenga

miundombinu ya barabara, madaraja pamoja na ma-*culvert,* ili wananchi hawa waepukane na adha kutokana na hali waliyonayo ya kimazingira? Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa kutambua hilo, Serikali iliona pia kuna umuhimu wa kuanza mjini, pale Nduguti, tukiwa tunakuja Singida Mjini kuanzia Iguguno, lakini mpango ni kuijenga barabara yote kwa lami hadi kwenda Sibiti. Kwa hiyo, nakuhakikishia tumetangaza tenda, lakini mkandarasi akawa ame-*tender* juu. Kwa hiyo, tuko kwenye kuitangaza tena upya dhamira ipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitangaza, lakini tukashindwana na mkandarasi kwa sababu, alikuwa ame-*tender* juu. Dhamira ni kubwa sana, tunaendelea kuitangaza na kuanza kuijenga muda siyo mrefu. Tupo kwenye utaratibu wa kuijenga. Hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhusu maeneo korofi, yenye mito na mabonde. Kama kuna kitu Tanzania tumefanya na katika Wizara ya Ujenzi ni pale ambapo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hasa kutokana na changamoto tuliyoipata, alipoamua kutafuta fedha zaidi ya shilingi bilioni 500 kwa ajili ya kujenga madaraja na makalavati na maeneo yote yenye mabonde ambayo yalikuwa yanakwamisha, kupeleka hizo fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni kati ya mradi mkubwa ambao wale ambao maeneo yao yamepitiwa, wanafahamu, tumejenga madaraja mengi, tumeondoa changamoto ya milima ambako ilikuwa inaporomoka, tumeijenga na tunaendelea kukamilisha. Mwisho wa mwezi huu ndiyo *deadline*, madaraja zaidi ya 81 yamejengwa. Pia mabonde mengi yamefanyika. Hatuwezi tukamaliza maeneo mengi, lakini maeneo yote korofi tumeyafanya na tutaendelea kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna changamoto kubwa sana kwenye Jimbo lako Mheshimiwa tunakukaribisha, labda litakuwa halikuonekana, lakini hata Mkoa wa Singida mradi huo ulipita na tumejenga madaraja mengi sana. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Festo Sanga kwa kifupi sana.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri utakubaliana na mimi leo ni mara ya 13 ninauliza kuhusu barabara ya Makete - Mbeya. Ni takribani miaka minne toka mmesaini mkataba na hakuna hata sentimeta moja ya lami Jimbo la Makete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia utakubaliana na mimi mkandarasi huyu *certificate* zime-*mature* tayari, lakini hamjamlipa, na zaidi, mimi kama Mbunge kwenye kazi ya Kibunge ya kuisemea barabara hii na kukuuliza maswali, nimefanya kazi yangu. Ipi ni kauli ya Serikali kwa wananchi wa Makete kuhusu barabara hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, barabara ya Makete – Isyonje ipo kwenye ujenzi, japo kwa sasa ni kweli kuna changamoto kubwa sana ya mvua inayonyesha. Ninakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge, mtafute mkandarasi, tayari tumeshamlipa hizo *certificate* zake, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, nilikuona Mheshimiwa Zuberi Mfaume, swali dogo la nyongeza.

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Morogoro Kusini na wananchi wa Halmashauri ya Morogoro

ningependa kujua, ni lini ujenzi wa barabara ya Bigwa – Kisaki utaanza? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Bigwa – Kisaki, kilomita 78, mkandarasi ameshalipwa na ameshaanza kazi za awali kufanya *site clearance* ikiwa ni pamoja na kujenga zile kambi za mhandisi mshauri. Kwa hiyo, kazi imeshaanza Bigwa – Kisaki. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea sasa, ninamwita Mheshimiwa Kellen Rose Rwakatare, Mbunge wa Mlimba, aulize swali lake.

Na. 100

**Ujenzi wa Barabara kutoka Daraja la Lumemo – Mbingu – Chita – Mlimba**

**MHE. KELLEN R. RWAKATARE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara kutoka Daraja la Lumemo - Mbingu – Chita?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kuanzia Daraja la Lumemo – Mbingu – Chita ni sehemu ya barabara ya Ifakara – Njombe *Border* yenye urefu wa kilometa 220. Ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa, ujenzi umeanza sehemu ya Ifakara – Mbingu, kilometa 62.5. Aidha, kwa sehemu ya Mbingu – Chita, urefu wa kilometa 37.5, mkandarasi amepatikana na taratibu za malipo ya awali *advance payment* zinaendelea ili aweze kuanza kazi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kellen Rose Rwakatare.

**MHE. KELLEN R. RWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Je, ni lini Serikali imejipanga kukamilisha hayo malipo ya awali *(advance payment)* ili ujenzi uanze kufanyika kwa *speed,* kwa sababu wananchi wa Mlimba wamesubiri sana kwa muda mrefu?

Je, ni lini Mheshimiwa Naibu Waziri atapanga muda ili tuambatane kwa pamoja ili kujionea mwenyewe mazingira na hali halisi ilivyo ya barabara za Jimbo la Mlimba zilivyo? Mvua zinanyesha kwa wingi, barabara zina makorongo, hazipitiki na wananchi wanapata taabu sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeshapata mkandarasi, tunajua athari ya kutokumlipa malipo ya awali. Malipo ya awali yanaandaliwa ili aweze kuanza kazi ya ujenzi kwa kipande hicho cha kilometa 37.5. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba mkandarasi ameshapatikana na atalipwa malipo ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutembelea hiyo barabara, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, niko tayari. Ninakuhakikishia nimeshaitembea hiyo barabara mara mbili, kuanzia Ifakara – Mbingu – Mlimba – Kibena *Junction*. Kwa hiyo, ninaifahamu, ni barabara muhimu ambayo inaunganisha Njombe na Morogoro. Kwa hiyo, niko tayari, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Nilikuona Mheshimiwa Zacharia Issaay, kwa kifupi.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Je, ni lini Serikali itatekeleza ujenzi wa barabara ya Magara – Mbuyuni – Mbulu kwa kiwango cha lami ambapo ni ahadi ya Makamu wa Rais kwa miaka mitano sasa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara ni kweli inapita kwenye *escapement* ambapo tunachokifanya sasa hivi ni kujenga kiwango cha zege kwenye ile miinuko mikali ili magari yaweze kupita wakati tunatafuta fedha, lakini kikubwa atakubaliana na mimi kwamba lile Daraja la Magara tulishalikamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tunaendelea kutafuta fedha kuijenga barabara yote kwa kiwango cha lami, lakini kikubwa sasa ni kujenga kwa kiwango cha zege kwenye ile miinuko mikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Sasa tunaendelea na swali linalofuata, linaulizwa na Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, Mbunge wa Karatu, kwa niaba yake atauliza Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas.

Na. 101

**Ujenzi wa Barabara ya Karatu –**
**Mbulu - Haydom – Lalago**

**MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS K.n.y. MHE. DANIEL A. TLEMAI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Lalago kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itajenga barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Lalago kwa kiwango cha lami kwa awamu. Hadi sasa, taratibu za manunuzi ya mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya Nkoma – Lalago, kilometa 65 zimekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa sehemu ya Mbulu – Garbabi, kilometa 25, kazi za ujenzi zinaendelea na zimefikia 41%

na kwa sehemu ya Labay – Haydom, kilometa 25 kazi za ujenzi zimefikia 11%. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas, maswali ya nyongeza.

**MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Ninashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo inafanywa na Serikali na kazi inaendelea, lakini bado *speed* siyo kubwa. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Tuna wananchi ambao barabara imewafuata kwa upande wa Mbulu – Garbabi na Labay – Haydom. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kuwalipa fidia wananchi hawa na kumwezesha mkandarasi kuikimbiza hii kazi kwa wakati? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Tuna kipande cha Garbabi – Dongobesh – Labay, kilometa 35, ambayo bado mchakato wake haujaanza, na Barabara hii inategemewa sana na wakulima wa kilimo cha umwagiliaji. Je, ni lini Serikali itaanza mchakato wa ujenzi wa kipande hiki cha katikati? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hawa wananchi ambao barabara imewafuata, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutahakikisha wanalipwa kabla hawajaondolewa kwenye maeneo yao ambayo barabara imewafuata. Kwa hiyo, tutahakikisha, kwa sababu barabara tumeshaanza kuijenga, na ili tujenge, ni lazima tuwalipe. Kwa hiyo, niwahakikishie tutawalipa hiyo fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu eneo la Garbabi – Dongobesh, ninadhani ndiyo barabara ambayo inaenda Dareda. Tumeshaanza upande wa Dareda *Mission,* tunajenga, na tutahakikisha tunaikamilisha hiyo barabara kwa kiwango cha lami, kadri fedha itakavyokuwa inapatikana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Waheshimiwa, tunaendelea. Sasa tunahamia Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Ninamwita Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, aulize swali lake.

Na. 102

**Wananchi Kupewa Vizimba vya Samaki Bukoba**

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza: -

Je, lini wananchi wa Bukoba watawezeshwa kwa kupewa vizimba vingi zaidi vya samaki ili kushiriki katika kukuza uchumi?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, ninaomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania *(TADB)* inaendelea na zoezi la utoaji wa mikopo ya masharti nafuu ya vizimba, vifaranga na chakula cha samaki. Katika awamu ya kwanza mikopo ya vizimba 44, Bukoba 30, Muleba 12, Misenyi viwili yenye thamani ya shilingi milioni 986.80 ilitolewa Mkoani Kagera kwa wanufaika 101.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara imepokea kiasi cha shilingi bilioni saba kutoka Hazina kwa ajili ya kuwezesha vijana kupata mitaji kupitia mikopo yenye masharti nafuu. Fedha hizo zitatumika kukopesha vijana 308 waliohitimu mafunzo hayo wakiwemo vijana 32 kutoka Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Wizara inatarajia kupokea sehemu ya shilingi bilioni 200 ambazo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais

ndani ya siku 100, zitazotekelezwa katika kuwezesha mikopo ya vizimba. Aidha, Wizara inaendelea kutafuta vyanzo vingine vya fedha ili kuendelea kutoa mikopo ya vizimba katika maeneo mbalimbali hapa nchini wakiwemo vijana wa Bukoba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa rai kwa Halmashauri kuelekeza sehemu ya mikopo ya 10% katika ufugaji samaki kwa vizimba iwapo zina maeneo yanayofaa kwa shughuli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Jasson Rweikiza, maswali ya nyongeza.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninashukuru kwa majibu ya Serikali kuhusu jambo hili la vizimba Bukoba. Hata hivyo, vizimba 44 vilivyopo Bukoba nii vichache sana, tuna ukanda wa ziwa kilometa 59. Kwa hiyo, tunahitaji vizimba vingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Je, Serikali haioni kwamba vizimba vikiongezeka kwa wananchi wa Bukona ni ajira tosha kwa wananchi wale kuwaongezea uchumi na Taifa zima kwa ujumla?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Hata hivyo vizimba vichache vilivyopo 44 hatuna vifaranga hadi twende Mwanza, umbali mrefu sana, vifaranga vinakufa, vinakosa *oxygen*. Je, Serikali haioni haja ya kujenga miundombinu ya vifaranga pale Bukoba kusudi wananchi wapate vifaranga pale pale kwao?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Kwanza ninaanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kwa bidii yake kubwa ya kuendelea kufuatilia

mustakabali wa vijana wake, hasa wanaojihusisha na ufugaji wa vizimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza, ni kweli vizimba 44 kwa eneo la ukubwa wa Ziwa lililoko katika Jimbo la Bukoba Vijijini ni vichache, lakini kama nilivyosema katika jibu langu la awali, Serikali inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kujenga vizimba hivi kwa vijana, wanawake na vikundi maalum vikiwemo vya wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunaendelea kuhamasisha taasisi za fedha zikiwemo benki na taasisi nyingine za uwezeshaji kuendelea kuwanufaisha au kuwapa mikopo vijana ili tuweze kuongeza kasi ya vijana hawa wanaonufaika na miradi hii ya vizimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuhusu suala la vifaranga, ni kweli, wakati tunaanza miradi hii, tulikuwa na changamoto kubwa sana kwanza ya upatikanai wa vifaranga, na pili upatikanaji wa vifaranga vyenye ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwishapiga hatua, tangu mwaka 2021 tulikuwa na uzalishaji wa vifaranga takribani 24,024,000 kwa mwaka na sasa hivi tunazungumzia uzalishaji wa vifaranga zaidi ya 140,000,000 kwa mwaka. Maana yake ni kwamba tumeongeza uzalishaji, lakini tunaongeza uratibu wa karibu wa wazalishaji wote ndani ya sekta binafsi na katika taasisi zetu wenyewe ikiwemo *TAFIRI* kuhakikisha vifaranga hivi vinavyozalishwa vinakuwa na ubora unaofaa ili vinapofikishwa kwa vijana wetu, basi viweze kuwapa tija inayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea. Sasa ninamwita Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, Mbunge wa Musoma Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 103

**Mikopo kwa Wafugaji wa Samaki wa Vizimba – Mara**

**MHE. MGORE M. KIGERA** aliuliza: -

Je, Serikali ipo tayari kutoa mikopo kwa wafugaji wa samaki wa vizimba Musoma ili kutoa ajira kwa vijana?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, ninaomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mgore Miraji Kigera, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania *(TADB)* inaendelea na zoezi la utoaji wa mikopo ya pembejeo za ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba ambapo katika mikopo ya awamu ya kwanza jumla ya vizimba 47 vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.126 vimetolewa, kama mikopo ya masharti nafuu isiyo na riba kwa wanufaika 130 nchini ikiwemo vijana kutoka Musoma Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa kuongeza ushiriki wa vijana katika ufugaji wa samaki kwa vizimba, Wizara inatekeleza Programu ya Jenga Kesho iliyo Bora (*BBT*-Uvuvi) kwa kutoa mafunzo kwa vitendo na mikopo yenye masharti nafuu. Lengo ni kuongeza uzalishaji na kutoa ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara imepokea kiasi cha shilingi bilioni saba kutoka Hazina kwa ajili ya kuwezesha vijana kupata mitaji kupitia mikopo yenye masharti nafuu. Fedha hizo zitatumika kukopesha vijana 308 waliohitimu mafunzo hayo wakiwemo vijana 14 kutoka Musoma Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Wizara inatarajia kupokea sehemu ya shilingi bilioni 200 ambazo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ndani ya siku 100 zitakazoelekezwa katika kuwezesha mikopo ya vizimba. Katika mgao wa fedha hizo, vijana wa Musoma watafaidika na mikopo hiyo. Aidha, Wizara inaendelea kutafuta vyanzo vingine vya fedha ili kuendelea kutoa mikopo ya ufugaji wa samaki kwa vizimba katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mgore Miraji, maswali ya nyongeza.

**MHE. MGORE M. KIGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Ninapenda kutoa pongezi nyingi sana na shukrani kwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwathamini wananchi wa Jimbo la Musoma Mjini, kwani tunategemea sana Ziwa kuliko kitu chochote. Hivyo, kwa kuwezesha vijana wetu kupata mikopo ili waweze kufanya ufugaji kwa weledi mzuri, wataenda kufungua fursa ya ajira na mzunguko wa fedha na uchumi utakuwa Musoma Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: Je, ni nini kauli ya Serikali kuhakikisha inawathamini wafugaji wa samaki kwa kupitia vizimba? Kwani wamekuwa na changamoto kubwa sana kwenye suala zima la upatikanaji wa vifaranga vyenye ubora pamoja na chakula. Kwa kuwa changamoto ya chakula huwa ni shida, inapelekea samaki wengi waweze kudumaa na wafugaji hawa kupata hasara kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, samaki anafugwa kwa miezi nane, wanatarajia apate kilo moja *and above,* lakini kwa sasa hivi samaki wanafubaa na kupata *0.6 kg* mpaka *0.8 kg*. Kwa hiyo, ni nini mpango wa Serikali kuwawezesha wafugaji hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Je, kauli ya Serikali ni ipi kuhakikisha inawasaidia vijana kupata ujuzi pamoja na mikopo ili

waweze kuanzisha upatikanaji wa chakula wenyewe katika Manispaa ya Musoma na waache kutoa chakula Kenya pamoja na Kibaha? Kwani ni mwendo mrefu na gharama ya chakula inakuwa ni kubwa sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Ninarudia tena kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa bidii yake kubwa ambayo anaendelea nayo kufuatilia miradi hii ya vizimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la vifaranga na chakula, kama nilivyozungumza hapo awali, tunaendelea na harakati za utatuzi wa changamoto hizi tulizokuwanazo mwanzo. Moja, tumeendelea kuhamasisha sekta binafsi katika kuwekeza, kuzalisha vifaranga na kutengeneza viwanda vya chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakiri kwamba tumekuwa na ongezeko kubwa sana la vifaranga pamoja na chakula ambacho kimesaidia wafugaji wetu kwa njia ya vizimba kuweza kupata kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tunaendelea kuwapa vijana wetu elimu ya utambuzi ili pale wanapoona vifaranga na chakula sokoni waweze kutambua kile kilicho bora *against* kile ambacho hakipo bora. Pia, tumeendelea kurekebisha mifumo yetu ya utoaji wa mikopo ambapo hapo awali tulikuwa na wazabuni wa moja kwa moja ambao tulikuwa tunaelekeza vijana wetu kwenda kwao kwa ajili ya kujipatia vifaranga na chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa vile tumeongeza upatikanaji wa vifaranga na chakula, tumeongeza uwazi ili kijana aweze kuingia sokoni na kuchagua kifaranga na chakula kilicho bora kwa ajili ya samaki wake aweze kupata samaki walio bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la Mheshimiwa Mbunge, kuhusu uwezeshaji wa vijana kujipatia ujuzi na mitaji ya kuwekeza katika uzalishaji wa chakula, hiki ndicho ambacho tunafanya

mpaka sasa. Tunaendelea kuhamasisha vijana wetu kuandaa maandiko ili ile elimu tunayowapatia tunapokuwa tunawaandaa kwa ajili ya kuingia kwenye ufugaji wa vizimba kupitia taasisi zetu za *FETA* na programu zetu za *BBT*-Uvuvi, waweze kuitumia kwa ajili ya kuzalisha chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, waandae maandiko wapeleke katika Halmashauri zetu waweze kunufaika na fedha za 10% na pia waandae maandiko wapeleke katika taasisi zetu za fedha ili waweze kupata mikopo ya kuwekeza katika uzalishaji wa chakula kwa sababu ni fursa kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Wizara tumeandaa mwongozo wa utengenezaji wa chakula cha samaki ili kila anayetaka kuwekeza katika sekta hii ya uzalishaji wa chakula cha samaki aweze kupata wepesi wa uwekezaji huo, na sisi kama Wizara tunaendelea kutoa msaada wa utaalam na maelekezo kwa yeyote ambaye anahitaji kufanya uwekezaji katika uzalishaji wa chakula cha samaki ili tuongeze upatikanaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, sasa ninamwita Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 104

### Kufunguliwa kwa Kiwanda cha Chai cha *WATCO* Kilichopo Katumba – Tukuyu Wilayani Rungwe

**MHE. SUMA I. FYANDOMO** aliuliza: -

Je, lini Kiwanda cha Chai cha *WATCO* kilichopo Katumba – Tukuyu Wilaya ya Rungwe, kitafunguliwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imefanya jitihada za kuhakikisha Kiwanda cha Chai cha *WATCO* kinafunguliwa ambapo Kampuni ya *WATCO* inayosimamia kiwanda hicho imepata mkopo ambao umetumika kulipa madai ya wakulima, wafanyakazi na watoa huduma wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya malipo hayo, hatua inayofuata ni ufunguzi wa kiwanda hicho ambacho kinatarajiwa kufunguliwa ifikapo tarehe 2 Machi, 2026 baada ya kukamilika kwa usafi na ukarabati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Suma, maswali ya nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa maswali mawili ya nyongeza. Kwanza niipongeze sana Serikali kwa hatua iliyochukua, kwamba tarehe 2/2/2026 Kiwanda cha *WATCO* kinakwenda kufunguliwa. Ninashukuru sana kwa kuwa mmeelewa vizuri shida ya wananchi wa Wilaya ya Rungwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza. Wanawake wa Wilaya ya Rungwe pamoja na wananchi kwa ujumla wamezoea sana kuamka saa 11.00 alfajiri kwa ajili ya kwenda kuchuma chai, maana hiyo ni sehemu ya ajira yao. Ajira hiyo sasa hivi imekuwa kama ni ndoto kwao kwa sababu Kiwanda cha Chivanje kimefungwa, sasa hii ni miaka miwili imepita. Je, ni lini Serikali itakwenda kufungua Kiwanda hicho cha Chivanje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kwenye hicho hicho Kiwanda cha Chivanje, kwa sababu kipo kwenye Tarafa ya Pakati na *WATCO* iko kwenye Tarafa za huku Ukukwe na Tukuyu Mjini. Wakulima wa Wilaya ya Rungwe wanalima mazao mengi, ikiwemo pamoja na zao la parachichi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bei elekezi ya Serikali kilo ya parachichi ni shilingi 2,500, lakini sasa hapo katikati wameingia watu ambao wanaitwa madalali ambao wanawaumiza sana wakulima wa Wilaya ya Rungwe ambapo wamepelekea bei ya

kilo ya parachichi kuwa shilingi 1,200 mpaka 1,500. Inaleta hasara kubwa sana kwa wakulima. Je, Serikali ina mkakati gani wa kwenda kusimamia bei hizo ili wananchi wa Wilaya ya Rungwe waweze kupona?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimpongeze dada yangu Mheshimiwa Suma Fyandomo kwa maswali mazuri, lakini pia kwa ushirikiano ambao amekuwa akiufanya na Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo husika, ni jambo jema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja tu ninamhakikishia ni kwamba, kila hatua tunayoifanya sisi Serikali ni hatua. Hatua ya kwanza ni kufungua Kiwanda cha *WATCO* ambacho kilikuwa na changamoto ya muda mrefu. Baada ya hapo, maana yake tutahamia katika hatua inayofuata kwenda katika eneo la Kiwanda cha Chivanje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote haya ni kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wakulima wanauza chai yao, na pia kwa akina mama ile ajira ambayo wamekuwa wakiipata ya kuchuma chai inaendelea. Kwa hiyo, hilo lipo katika mipango ya Serikali na tutalitekeleza kwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu parachichi na hao madalali ambao wamekuwa wakifanya hiyo kazi, maelekezo ya Serikali yako pale pale, kwamba bei elekezi ndiyo ambayo inatakiwa ifuatwe kwa wanunuzi wote wa parachichi. Ndiyo maana sisi Serikali tumekuwa tukisisitiza wakulima kujiunga na vyama vya ushirika ili wawe na nguvu ya pamoja katika kupigania bei ambayo sisi tumeiainisha. Kwa hiyo, kwa sababu ameitoa hapa kama taarifa nasi tutaendelea kufuatilia ili tuhakikishe ile bei ambayo imetolewa inafuatwa na wanunuzi wote. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilikuona Mheshimiwa Timothy Mnzava, kwa kifupi sana.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wakulima wa chai wa Tarafa ya Bungu wameteseka kwa muda mrefu baada ya mwekezaji kufunga viwanda; na pamoja na ahadi nyingi, lakini hawaoni mwelekeo mpaka sasa. Je, Serikali ina mpango upi wa kuwaondolea adha wakulima wa chai wa Tarafa ya Bungu kule Korogwe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimpongeze vilevile Mheshimiwa Mnzava, ninafahamu kwamba amekuwa akilifuatilia jambo hili kwa muda mrefu. Nimwambie tu jambo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, tuna uhakika na hiki ninachokisema. Ni kwamba Serikali tayari tumeshanunua kiwanda kwa ajili ya kupeleka katika eneo la Jimbo lako katika *AMCOS* ya Sakare pale, kiwanda kwa ajili ya kuchakata chai. Kimekamilika pale nchini China, sasa hivi tuko katika harakati za kusafirisha na kuleta hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, awahakikishie wananchi wake kuwa, pamoja na kwamba mazungumzo mengine yanaendelea, lakini sisi kama Serikali tumeshanunua kiwanda hicho na tutakuja kukifunga ndani ya muda mfupi ambao naamini itakuwa ni suluhisho la kudumu kwa wakulima wa chai katika eneo lake, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea. Sasa namwita Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo aulize swali lake.

Na. 105

**Mkulima Kununua Mbegu za Mahindi kila Mwaka**

**MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA K.n.y. MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza: -

Je, kwa nini Mkulima analazimika kununua mbegu za mahindi kila mwaka badala ya kutumia zile ambazo amevuna?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkulima hulazimika kununua mbegu kila msimu ili aweze kupata tija iliyodhamiriwa kwa sababu mbegu anazonunua katika maduka ya pembejeo huwa zimepitia majaribio ya kisayansi katika maabara ili kuthibitisha ubora wa sifa mbalimbali, ikiwemo kiwango cha uzalishaji, uhimilivu wa magonjwa na ukame. Mkulima anapovuna mazao na kutumia kama mbegu kwa mara ya pili au zaidi husababisha sifa za mwanzo za mbegu husika kupungua ama kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia kubwa ya mbegu zinazotumiwa na wakulima nchini, ni mbegu aina ya chotara ambazo utengenezaji ama uzalishaji wake hutumia aina mbili au zaidi tofauti za mbegu wazazi kutoka jamii moja. Kutokana na sababu hiyo, iwapo mbegu hizo zitatumika kama mbegu kwa mara ya pili au zaidi husababisha kupotea au kupungua kwa sifa bora za mbegu hivyo kuchangia kushuka kwa tija na uzalishaji wa mazao ya mkulima.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Japhael, maswali ya nyongeza kwa kifupi.

**MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Margaret Sitta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kilimo cha mahindi ni zao la mkakati katika nchi yetu, na ni zao linalolimwa na wananchi wengi, wakiwepo wananchi maskini na hasa wale ambao wanahudumiwa na Serikali, kwa maana ya *TASAF,* ukilinganisha gharama ya mbegu kwa wastani kilo mbili za mbegu zinanunuliwa kwa shilingi 15,000 kwa maana ya ekari moja inatumia mifuko minne kwa thamani ya shilingi 60,000, ukijumlisha

pamoja na mbolea na gharama za kilimo inapelekea wastani wa heka moja *cost* yake kama 350,000, je, Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba gharama ya mbegu inashuka ili kuweza kuzibeba na familia maskini ziweze kulima vizuri zao la mahindi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Katika Mkoa wa Tabora, na hasa kwenye Jimbo la Urambo, Ulyankulu, Kaliua na majimbo mengine, lipo tatizo la wadudu waharibifu wa mahindi hasa yakiwa na kina kuanzia futi moja mpaka futi tano. Wadudu wanaitwa al-maarufu rusomi, wanashambulia sana mahindi na kuyaharibu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba dawa za kuwatibu wadudu wale zinaingia kwenye ruzuku?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, ameuliza maswali ya msingi kwa niaba ya Mheshimiwa Mama Sitta. Nimwambie tu kwamba moja ya mpango wa Serikali katika kupunguza gharama kwa mkulima ni pamoja na kuweka ruzuku. Miongoni mwa ruzuku tulizoweka, tumeweka ruzuku katika mbegu, lakini vilevile tumeweka ruzuku katika mbolea na viuatilifu, lengo tu ni kupunguza gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bado Serikali tumeendelea na mikakati ya kuhakikisha kwamba uzalishaji wa mbegu unaongezeka. Ndiyo maana sasa hivi kwa wakulima ambao wanataka kuingia katika kile kilimo cha kimkataba katika mashamba ambayo yanamilikiwa na Wakala wetu wa Uzalishaji wa Mbegu *(ASA),* tumekuwa tukiruhusu watu kuingia katika kilimo cha kimkataba ili tuongeze uzalishaji wa mbegu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba bado tunaendelea na michakato ya kuhakikisha kuwa tunaongeza uzalishaji ili tuhakikishe kuwa bei inashuka pamoja na kwamba tumeweka ruzuku ndani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hawa wadudu waharibifu ambao ameainisha, watu wetu wa *TPHPA* wanaendelea na hiyo

kufanya tathmini kwa sababu uwekaji wa ruzuku katika viuatilifu ni hatua kwa hatua. Kwa hiyo, tumeweka sehemu katika mazao kama ya parachichi, tumeweka sehemu katika mazao ya korosho na vilevile tutaangalia katika wadudu waharibifu wa mahindi. Kwa hiyo, na lenyewe lipo katika mchakato na tukishalikamilisha tutatolea taarifa hapa. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Tunahamia Wizara ya Afya, sasa namwita Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo, Mbunge wa Ukonga aulize swali lake.

Na. 106

**Malipo ya Huduma za Afya kwa Wajawazito na Watoto Chini ya Miaka Mitano**

**MHE. BAKARI B. SHINGO** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja kukemea vitendo vya kutoza gharama za matibabu kwa wajawazito na watoto chini ya miaka mitano?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo, Mbunge wa Ukonga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza Sera ya Afya ya Mwaka 2007 inayoelekeza kutoa huduma za matibabu bure kwa makundi maalum ikiwemo akina mama wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano pamoja na wazee wenye umri zaidi ya miaka 60 wasio na uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshatangaza rasmi kuanza utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa wote awamu ya kwanza itakayohusisha makundi ya wananchi ikiwa ni pamoja

na watoto, wajawazito, walemavu  na wazee wasio na uwezo, ambapo kundi hili litagharamiwa na Serikali.  Kukamilika kwa hatua hii kutawezesha wajawazito na watoto chini ya miaka mitano kupata huduma za afya kwa kugharamiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa rai kwa waganga wakuu wa mikoa na wilaya pamoja na waganga wafawidhi wa vituo vya kutolea huduma za afya kuhakikisha kuwa wanatekeleza maelekezo ya Serikali katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma za afya kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bakari Bakari, maswali ya nyongeza.

**MHE. BAKARI B. SHINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali inaandaa mpango kwa ajili ya bima za afya. Swali langu lilikuwa linazungumzia kipindi hiki ambacho bima hiyo ya afya kwa wote haijaanza kukamilika, na huku tukijua kwamba nyuma kuna sera ya wazee kuhudumiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jimbo langu, kuna wazee kadhaa wameshindwa kupata hiyo huduma. Swali langu linasimama kwamba, hawana sifa ya kupata huduma hiyo wakati tukisubiri mpango huo wa Bima ya Afya kwa Wote?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Ukonga Mheshimiwa Bakari Bakari kwa kuwa kinara wa kutetea afya za akina mama wa Tanzania ili waweze kujifungua na kuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya Bima ya Afya kuanza, Serikali ilikuwa na utaratibu maalum ambao wagonjwa hawa wa makundi maalum wakiwemo wajawazito, akina mama, watoto, na wazee walikuwa wanagharamiwa matibabu na Serikali bure kwa kupelekewa vifaa na kwa kupewa msamaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikitumia zaidi ya shilingi bilioni 40 kwa mwaka kuwahudumia wagonjwa hawa kwa kutoa msamaha katika hospitali zetu. Wanapewa vipimo, wanapewa matibabu, wanajifungua kwa gharama za hospitali. Hii ndiyo imepelekea vifo vya mama na mtoto kupungua katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa, nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Suluhu Hassan ambaye aliamua kuwekeza kwenye idara hii ya mama na mtoto. Tumeona vifo vikipungua kwa zaidi ya 80%. Vifo vimetoka 556 kwa vizazi hai 100,000 mpaka vifo 104 kwa vizazi hai 100,000, hali iliyopelekea mpaka Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Suluhu Hassan kutunukiwa tuzo ya *Goal Keeper Award* na *Gates Foundation* ambayo haijawahi kutokea kwa Rais yeyote mwananamke duniani kupewa tuzo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haijawahi kutokea Rais yeyote Afrika kupewa tuzo hii. Yeye akiwa ni Rais wa kwanza Tanzania kupewa tuzo hii kwa sababu kwa moyo wa dhati kabisa amewekeza katika kumhudumia mama na mtoto ili kupunguza vifo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo malengo mkakati, ifikapo mwaka 2030 tunataka kupunguza vifo vya mama na mtoto mpaka kufikia vifo 70 kwa kila vizazi hai 100,000. Ndiyo maana tumekwenda kwa Bima ya Afya kwa Wote ili sasa kuwa na huduma bora zaidi kwa ajili ya akina mama waweze kujifungua salama na watoto wao waendelee kuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru. Sasa tunaendelea na Wizara ya Fedha, namwita Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga, Mbunge wa Kigamboni aulize swali lake.

Na. 107

**Kupunguza Riba ya Mikopo kwa Wafanyakazi**

**MHE. HARAN N. SANGA** aliuliza: -

Je, lini wafanyakazi wa Tanzania watapunguziwa riba ya mikopo na kufikia asilimia saba au nane?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga, Mbunge wa Kigamboni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na sera za uchumi wa nchi yetu, riba za mikopo zinazotolewa na taasisi za fedha nchini kwa wateja mbalimbali, ikiwemo wafanyakazi huamuliwa na soko *(market determined)*. Hivyo, Serikali inaona kuwa kuelekeza taasisi za fedha kuweka viwango vya riba vya asilimia saba au kiwango chochote mahususi au maalumu kwa ajili ya wafanyakazi itakuwa inakinzana na maelekezo ya sera za soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua kuwa swali hili lina msingi wa kwamba taasisi za fedha, maeneo pekee ambayo yanapata faida kwa kukopesha ni kwa watumishi ambao mishahara yao kukatwa ni rahisi. Hata hivyo, taasisi ya fedha inaweza kuweka kiwango cha riba kwenye mikopo ya wafanyakazi au mkopaji yeyote kufikia asilimia saba au pungufu ya hapo, kama itaona inafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, wafanyakazi au mkopaji yeyote anaweza kukubaliana na taasisi ya fedha na kupata kiwango cha riba cha asilimia saba au pungufu kwa kadri itakavyowezekana. Vilevile, wafanyakazi kupitia waajiri wao wanayo fursa ya kuwasiliana na benki husika na kukubaliana riba wanayoweza kutoza wafanyakazi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga, maswali ya nyongeza.

**MHE. HARAN N. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipongeze tu majibu ya Serikali, lakini nataka kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, benki zetu zinazoitwa *commercial banks* zinategemea vitu viwili katika kufanya biashara, kwa kutumia *consumers' loan* na *Government Bond,* kwa sababu hivi vitu vyote vina *security* kwao. Kwa Serikali kuacha watumishi ambao wamekuwa wakitumikia miaka yao 55, 60 mpaka 65, amekuwa akifanya kazi za Serikali, kwa sababu tunaamini kabisa watumishi wa Serikali siyo wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mshahara wake ndicho kitu pekee ambacho anakitegemea ili aweze kupata mkopo aweze kujenga nyumba, apate mkopo aweze kutengeneza maisha yake ya kujikimu kwa ajili ya kustaafu. Je, Serikali ina kauli gani ambayo itawasaidia watumishi hawa kuanza kuwa-*motivate* katika kufanya kazi, na pia kuwasaidia kwamba watapokuwa wanastaafu, wawe na maisha bora ya kujikimu?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru Mheshimiwa Sanga, anauliza maswali haya bila shaka ni kutokana na kwamba wafanyakazi hawa ni dada zetu, ni kaka zetu na wengine ni wanetu. Kwa hiyo, maisha yao na matumaini yao ya kuishi kwa kufanya kazi, mwisho wa siku yawe na faida kwao. Serikali itaendelea kuandaa mazingira wezeshi ya kifedha kwa watumishi kama ambavyo imekuwa ikifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Serikali kupitia Wizara ya Fedha iliunda mfuko maalum wa *Advances Fund* kupitia Tangazo la Serikali Na. 709 lililotoka mwaka 2018 likisomeka kama "*Advances Fund Establishment Order.*" Lengo kuu la kuanzishwa

mfuko huu ilikuwa ni kuwezesha utoaji wa mikopo kwa watumishi wa umma kwa masharti nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo inayotolewa kupitia Mfuko wa *Advances Fund* huwa inatozwa kwa gharama ya jumla ya asilimia nne, ambayo kimsingi huwa ni kwa ajili ya *services charges* na bima tu ya huo mfuko. Mpango huu unawahusisha wafanyakazi au tuseme watumishi wa umma, kwa maana ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na utekelezaji wa utaratibu huu, Serikali ilielekeza taasisi nyingine za umma kuanzisha mifuko yao ya ndani ya utoaji mikopo kwa watumishi wao kwa lengo la kuhakikisha wanapata mikopo yenye masharti nafuu na hivyo kuwezesha kuimarisha ustawi wa uchumi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tangu mwaka 2021 hadi Januari, 2026 watumishi hao wamekopeshwa zaidi ya shilingi bilioni 497, lakini kwa kipindi cha mwaka 2025/2026 pekee watumishi wamekopeshwa kwa zaidi ya shilingi bilioni 74.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali hiyo, watumishi hao wataendelea kuishi kwa matumaini na watastaafu wakiwa wanawezeshwa na Serikali, na bila shaka mpango huu utaendelea kufanyika na jitihada nyingine za kuwezesha wafanyakazi waweze kuwa na maisha mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii. Swali litaulizwa na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba yake Mheshimiwa Asia Halamga.

Na. 108

**Kukabiliana na Wanyamapori Wakali – Karatu**

**MHE. ASIA A. HALAMGA K.n.y. MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukabiliana na wanyama waharibifu na wakali wanaotoka Hifadhi ya Ngorongoro na Ziwa Manyara – Karatu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kwa unyenyekevu mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu Wilaya ya Karatu, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kuongeza doria pamoja na kuimarisha matumizi ya teknolojia kwa kutumia ndege nyuki; kuanza ujenzi wa Kituo cha Askari katika Kijiji cha Lostete kilichopo mpakani mwa hifadhi; na kutumia Askari wa Vijiji *(VGS)* wanaoshirikiana na askari wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, katika mwaka wa fedha wa 2025/2026, Serikali itajenga uzio wa umeme wenye urefu wa kilometa 15 ili kukinga na kuzuia tembo na wanyamapori wengine kuingia kwenye maeneo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua nyingine, Serikali imeandaa Mkakati mpya wa Kitaifa wa Kusimamia Utatuzi wa Migogoro baina ya Binadamu na Wanyamapori wa miaka 10 kuanzia 2025/2026 hadi 2035/2036. Mkakati huu utatekelezwa kwa ushirikiano na Wizara za kisekta ikiwemo TAMISEMI, Maliasili na Utalii, Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Ardhi, Nyumba na Maendeleo

ya Makazi chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu ili kuhakikisha kuwa jitihada za kupunguza changamoto hii zinafanyika kwa pamoja na kwa ufanisi mkubwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Halamga, maswali ya nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii kwa kuhakikisha kwamba inakuwa na mkakati mkubwa na endelevu wa kuweza kutatua changamoto zinazowakabili wananchi dhidi ya wanyama waharibifu. Je, ni lini sasa ujenzi huu fensi kilometa 15 utaanza? Kwa kuwa katika majibu ya msingi yalieleza kwamba ujenzi utanza kwenye bajeti hii ya mwaka huu, na kwa kuwa tuko mwezi wa Pili wa mwaka wa bajeti, na mwaka huu unapofika mwezi wa Sita mwaka wa bajeti unakuwa umekwisha, je, nini kauli ya Serikali, ituambie itaanza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kufuatana na Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso ili kwenda kujionea kadhia hiyo wanayopata wananchi wa Karatu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi ya kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Asia Halamga. Kwanza, nimpongeze sana kwa mashirikiano mazuri, na kwa kuwa ameonesha kabisa anauliza maswali ambayo yanaenda kujenga. Pia nimpongeze na Mwenyekiti ambaye kimsingi ndio ameuliza swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwondoe shaka Mheshimiwa Asia kwamba ujenzi huu utafanyika ndani ya mwaka huu wa fedha haraka iwezekanavyo kwa sababu tayari fedha imeshaingia. Mradi wote gharama yake ni shilingi milioni 900, na tayari shilingi milioni 300 zimepelekwa *site*. Ninachomhakikishia ni

kwamba wakati wowote, wala asihofu ya kwamba tumefika mwezi wa Pili, ujenzi unaenda kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, huu ni wajibu. Ninaachaje sasa kufuatana na Mwenyekiti kupata baraka zake kwenda katika *site* hiyo huko? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge ili kujadili jambo la dharura.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali na majibu. Sasa ninaomba nilete kwenu matangazo. Tunaanza na tangazo la wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Kwanza ni mgeni wa Mheshimiwa Spika, Ndugu Seraphin Lusala, Mkurugenzi wa Masoko na Mauzo wa *Serena Hotel* ya Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 20 wa Mheshimiwa Beng'i Mazana Issa, ni familia yake kutoka Mkoani Kigoma, Dar es Salaam na Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 12 wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge, ambao ni Wanamaombi kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Pia tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunaye Ndugu Yohana Benjamin Kasimba kutoka Ilemela Jijini Mwanza; wapo wanafunzi 53 na walimu watano wa Shule ya *Dar es Salaam Independent* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Vile vile tunao wageni 19 ambao ni Umoja wa Wanawake wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania Jimbo la Makao Makuu, Ushirika wa Bethel Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele, Mbunge, ambao ni Madiwani kutoka Jimbo la Dodoma Mjini. *(Makofi)*

Tunao watumishi 16 wa Shirika la *Youth with Mission* pamoja na wageni wao kutoka Korea ya Kusini. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwaletee tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge wote, kutakuwa kuna uchaguzi wa viongozi wa *Bunge Sports Club* utakaofanyika siku ya Alhamisi tarehe 6 Februari, 2026 katika Ukumbi wa Msekwa saa 7.30 mchana. Uchaguzi huo utahusisha viongozi wafuatao: Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, Makamu Mwenyekiti, Meneja na Wajumbe watano wa Kamati ya Utendaji ya *Bunge Sports* angalau wanawake wawe wawili.

Fomu za kugombea zitaanza kutolewa leo tarehe 3 Februari, 2026 katika Ofisi ya Katibu wa Bunge na zitarejeshwa tarehe 5 Februari, 2026 saa 10.00 jioni.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba mpokee tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa Bunge Marathon Mheshimiwa Festo Sanga.

Taarifa kuhusu Tamasha la Bunge Bonanza lililofanyika Jumamosi tarehe 31 Januari, 2026 Shule ya Sekondari ya John Merlin Dodoma. Washiriki wa Bunge Bonanza la tarehe 31 walikuwa ni Wabunge, Watumishi wa Ofisi ya Bunge na wadhamini wetu wa Benki ya Azania. Bonanza hili lilibebwa na kauli mbiu, "Umoja wetu ni Nguvu yetu."

Waheshimiwa Wabunge, washiriki wengine walitoka Wizara ya Ulinzi, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Vijana, *RAS Dodoma,* Chuo cha *St. John,* Chuo cha Mipango, *CBE* na *REA*. Aidha, mashabiki wa timu za Simba na Yanga kutoka maeneo mbalimbali ya Jiji la Dodoma walisherehesha tukio hilo. Mgeni Rasmi wa Bonanza

alikuwa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Tanzania.

Tunawashukuru Azania Benki kwa udhamini wao, uongozi wa Shule ya John Merlin, na watoa huduma wote kwa kufanikisha tamasha hilo. Kipekee, tunaishukuru Ofisi ya Waziri Mkuu kwa uratibu wao kwa upande wa ushiriki wa Serikali. *(Makofi)*

Tamasha hili lilifanyika kwa utaratibu wa kushindana mashabiki wa timu ya Simba na Yanga ambapo matokeo yalikuwa kama ifuatavyo: Michezo ya ushindani, mpira wa miguu, Simba ilishinda goli mbili na Yanga sifuri. *(Makofi)*

Mpira wa Pete, Simba iliifunga Yanga magoli 20 kwa 15. Mpira wa kikapu wanaume, Simba walishinda vikapu 60 kwa vikapu 54 vya Yanga. Mpira wa Kikapu wanawake wa Yanga walishinda vikapu 37 kwa 30 vya Simba. *(Makofi)*

Mpira wa Wavu Wanaume, Yanga ilishinda Simba kwa seti mbili kwa sifuri. Mpira wa Wavu Wanawake Simba ilishinda kwa seti mbili kwa sifuri. Kuvuta Kamba Wanaume Simba walishinda kwa mivuto miwili kwa sifuri. Kuvuta Kamba wanawake Simba walishinda mivuto miwili kwa sifuri. *(Makofi)*

Washindi wa medali: washiriki wa Bunge Bonanza walipewa vikombe kwa baadhi ya timu na medali kwa washindi wa michezo iliyoshindaniwa.

Waheshimiwa Wabunge, wafuatao walipata medali za dhahabu. Mchezo wa *Draft,* Wanaume: Mshindi alikuwa Mheshimiwa Faraji Mandala (Yanga). Mchezo wa *Draft* Wanawake: Mshindi alikuwa Mheshimiwa Khadija Taya (Yanga). Mchezo wa *pool table*, wanaume mshindi alikuwa Shaffin Ahmedali Sumar (Simba). Mchezo wa riadha Meta 100 Wanaume: mshindi ni Mheshimiwa Jafar Rajab Seif (Simba). *(Makofi)*

Mchezo wa Riadha Mita 100, Wanawake: Mshindi alikuwa Magreth Ezekiel (Yanga). Mchezo wa Bao, Wanawake: Mshindi

alikuwa Mheshimiwa Hawa Mchafu (Yanga). Mchezo wa Kufukuza Kuku, Wanaume: Mshindi alikuwa Sadifa Juma (Simba). Kupenya kwenye Pipa, Wanaume: Mshindi Mheshimiwa Joel Nanauka (Yanga). Mchezo wa Kupenya kwenye Pipa, Wanawake: Mshindi alikuwa Mheshimiwa Zainab Katimba (Yanga). *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa matangazo.

Katibu.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hoja ya dharura! Hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge kujadili jambo la dharura.

**NDG. BAKARI KISHOMA - KATIBU MEZANI:** Kamati ya Mipango.

**MWENYEKITI:** Kamati ya Mipango.

## KAMATI YA MIPANGO

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA - KATIBU MEZANI:**

**Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda mrefu 2026/2027 - 2050/2051, Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/2027 – 2030/2031) na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2026/2027**
**na**
**Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Muda wa Kati ya 2026/2027 - 2028/2029**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Keneth Ernest Nollo, wajiandae Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga.

**MHE. KENETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii nikupongeze wewe kwa kupata nafasi ya kuwa Mwenyekiti wa Bunge. Pamoja na yote, vilevile niishukuru Serikali kwa kuleta mpango huu wa miaka mitano pamoja na mpango huu mrefu kwa ajili ya kujadili dira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza mchango wangu, nilitaka ninukuu sehemu ya Hotuba ya Waziri aliyowasilisha hoja hii kwamba, Tanzania ina historia ndefu ya kuandaa mipango ya maendeleo. Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu wa kwanza uliandaliwa mwaka 1964 na maelezo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo mipango hii haikutekelezwa kikamilifu kutokana na changamoto za kiuchumi zilizoikumba dunia na nchi yetu ikiwemo ukame na hali mbaya ya hewa, kuharibika kwa soko la mafuta duniani na vita ya Tanzania na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hizi mbili ambazo Waziri amezionesha za suala la ukame na suala la kupanda bei ya mafuta duniani bado zipo zinazunguka. Suala la ukame kwa kiasi kikubwa bado tunategemea kilimo cha mvua. Kwa hiyo, tatizo hili bado lipo kama ambavyo liliharibu mipango ile ya nyuma, tatizo hili bado hatujalitatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la mafuta na uhakika wa mafuta katika nchi yetu. Mabadiliko makubwa yanatokea hasa katika nchi zinazozalisha mafuta, lakini tunaona hali ya usalama katika nchi za Mashariki ya Kati. Vilevile, tunaona namna ambavyo Mataifa makubwa hasa Marekani yanavyotoka katika mradi wa kufanya biashara na zaidi ya kutumia niseme mabavu katika biashara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sisi Tanzania kama watumiaji wa mafuta ambayo kwa kiasi kikubwa 100% tunaagiza kutoka nje. Serikali ina mpango gani wa kuangalia kwamba 1974 tulifungua mtambo wetu wa kusafisha mafuta *(Tiper)* na zao lake, tumeona kama tumefanya ya kupeleka mafuta Zambia ile *crude oil*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumepata mafuta kutoka Uganda, na sisi ni sehemu ya bomba lile. Naishauri Serikali ione namna ya kuanza kusafisha mafuta hapa nchini. Lengo letu ni tuwe na uhakika wa mafuta badala ya kuagiza kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili tukilifanya, kwanza tutaweza kuhudumia nchi nane ambazo zitatutegemea sisi kwa ajili ya kuingiza mafuta hapa nchini. Suala hili Serikali haiwezi kusema ni gumu, tulishalifanya kupitia *Tiper*. Mimi ninaomba mpango huu tuufufue ili Tanzania sasa iwe ni sehemu ya kuzalisha mafuta na kuzalisha nchi nyingine ambazo zinatutegemea katika ukanda wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la uchumi ukiangalia mpango na dira, Serikali inasema tuwe na ustawi mzuri wa Uchumi, lakini kubwa zaidi tunalenga katika sekta binafsi. Mimi ninataka niseme na Serikali iangalie bado uchumi wa dunia sasa unaongozwa na Serikali. Tukichukua mfano wa China, mashirika 362 yote yanaongozwa na Serikali *(state owned enterprises)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili siyo baya, na wala siyo aibu kwa Serikali kufanya biashara, lakini kufanya biashara katika maeneo ambayo yanahitaji mitaji mikubwa sana. Kama nilivyosema, kwa mfano, China yale mashirika yanayomilikiwa na Serikali 100% yako mashirika 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye majimbo kama halmashauri zetu ni karibu mashirika 150. Halafu yapo mashirika yanayoendeshwa na wawekezaji, Serikali ina mkono wake pale, ndiyo inafika karibu 362. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake ni nini? Tukiweza kuwekeza fedha zetu katika maeneo ambapo unahitajika mtaji mkubwa, tutakuwa na uchumi himilivu bila kutegemea fedha kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri nchi yetu ifanye uamuzi katika maeneo matatu. Kwanza, uzalishaji wa chuma ambapo ndiyo fedha nyingi nchi yetu inaingiza, na chuma hiki tunachopata ni chuma chakavu, tunakirudisha lakini hatujawa na chuma ghafi cha kuweza kuzalisha chuma. Chuma hicho tukitumie sisi wenyewe, na pia tukiuze katika nchi zinazotutegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina uwezo wa mtaji, inaweza ikaamua kuanza uzalishaji wa chuma. *Story* ya Liganga na Mchuchuma imechukua muda mrefu sana, lakini *story* hii ya Liganga na Mchuchuma ipo kampuni ambayo inatoka kwenye jimbo mojawapo la *China. Is a state-owned company*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetuchukua muda mrefu sana. Mimi siamini kuwa Serikali haina uwezo wa kuanza ujenzi na kiwanda cha pale Mchuchuma kwa ajili ya uzalishaji wa chuma. Jambo hili tunalifanya. Kielelezo cha kujenga *SGR* ni kielelezo cha kuonyesha nchi hii inaweza kufanya jambo lolote ikiamua kuwekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, *China* sasa ameenda katika suala zima la madini. Ameanzisha Kampuni kubwa ya *rare earth minerals. China* sasa anazalisha yale madini yanayohitajika sana duniani. Wana kampuni yao ya kuzalisha mafuta, *The PetroChina*, lakini *The China Minmetals* kwa ajili ya chuma, *zinc*, na *copper*, na wana *China Coal* kwa ajili ya *aluminium*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa na sisi kwa nini tusizalishe dhahabu? Nchi yetu ina dhahabu nyingi, kwa nini Serikali isiingize mkono tuanzishe shirika? Tunayo *STAMICO*, tuweke mtaji mkubwa wa kuzalisha dhahabu ambapo tutaenda kiwango sawa kama akina *GGM* na akina *Barrick*. Ninaiomba sana Serikali, suala la

kuwekeza kwenye dhahabu nchi yetu itapata dhahabu za kutosha, tutaweza kuuza na tutakuwa na uchumi mkubwa kupitia uzalishaji wa dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni *textile*, uzalishaji wa nguo. Sote ni mashahidi kwamba nchi yetu kwanza imekaa katika lango, kwamba nchi zinazotuzunguka zinategemea *importation* kupitia nchi yetu. Jirani yetu ambaye vilevile ana sifa kama za kwetu anakwenda *speed* kubwa katika uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ethiopia ambaye ana sifa kama za kwetu anazalisha sana *textile*. Katika jambo hili tuondoe *story* za Urafiki, na za *Musoma Textile*. Vile ni viwanda vya zamani, hatuwezi kuvifufua. Serikali iamue kabisa kwamba ianze uzalishaji wa nguo ambapo tutahudumia watu wetu na nchi zinazotuzunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la uwekezaji mkubwa katika kilimo. Fedha nyingi tunaitumia katika kuagiza ngano katika nchi yetu. Suala hili kama nilivyosema, na kwenye mpango huu, Serikali iangalie. Kwanza matumizi ya jembe la mkono tuseme jambo hili tunakwenda kulikomesha kama ambavyo tulimtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya jembe la mkono kwanza ile ni *corporal punishment*, hatuwezi kwenda nayo. Kwa hiyo, Serikali ije, kama hatuwezi kwenye matrekta, basi hata majembe ya kukokotwa na ng'ombe. Tuwe na *timeline* ya kuli-*phase out* jembe le mkono. Serikali iliangalie jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takribani kaya milioni saba bado zinatumia jembe la mkono. Sasa hatuwezi tukawa na uzalishaji wa kilimo kama tutatumia jembe la mkono. Kwa hiyo, Serikali katika mpango wake ninadhani iweke *timeline* kwenye dira, kwamba mwaka 2030 au mwaka 2035 jembe la mkono sasa likae kwenye maktaba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninakushukuru. Ahsante sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Nilimwita Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, na Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma wajiandae. *(Makofi)*

**MHE. ABDALLAH S. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyopo Mezani. Kipekee nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambazo anaendelea kuzifanya katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninachukua nafasi hii kuwapongeza watoa hoja: Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo na msaidizi wake Mheshimiwa DKt. Chaya kwa wasilisho zuri. Pili, Waziri wa Fedha Mheshimiwa Balozi Khamis Omar pamoja na Manaibu wake, Mheshimiwa *Eng*. Mshamu Munde na Mheshimiwa Luswetula. Ninawapongeza kwa kazi nzuri, wameanza kazi zao vizuri. Ni Mawaziri ambao wanafikika, wanasikiliza, na wanashaurika. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumewasilishiwa hapa nyenzo tatu na Waziri wa Mipango kwa ajili ya utekelezaji wa Dira 2020 – 2050. Ninanukuu maneno yake katika wasilisho lake amesema: "Kama sehemu ya maandalizi ya utekelezaji wa Dira 2020 – 2050, nyenzo tatu zimeandaliwa."

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajikita kwenye Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Ukiangalia wasilisho la Mheshimiwa Waziri na ukurasa wa 86 wa huu mpango wa nne unaelezea kinagaubaga kwamba, ili kuhakikisha utekelezaji wenye mafanikio wa mpango wetu, imebainika mambo manne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitajikita katika jambo moja tu la msingi. Utawala bora katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, na zimeainishwa changamoto hapa, kwamba Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa, asilimia 85 ya bajeti yake inategemea Serikali

Kuu. Changamoto ya pili ni kwamba, kuna mwingiliano wa majukumu kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile imeelezewa vizuri kwamba, kuna upungufu mkubwa wa watumishi katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa, na ikaja na suluhisho kusema, "hapa ili tuziwezeshe Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa lazima tuzingatie ugatuaji, *D by D (Decentralization by Devolution)*." Mimi nitajikita hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kitu hakiwezi kutekelezeka kama hakutakuwa na Sheria ya Ugatuaji. Ugatuaji Tanzania bado tunatekeleza kwa tamko la kisera tu, hata sera bado haipo. Maelezo ya Wizara kwamba sasa hivi wamekamilisha sera, basi sheria ya ugatuaji ije ili yawekwe wazi majukumu ya Serikali Kuu na majukumu ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa. La sivyo, tutakuwa tunachanganyana kila siku na kutakuwa na mabadiliko kila siku. Akija huyu, anasema watumishi wa kilimo wahamie Serikali Kuu, mwingine anasema watumishi wa kilimo wabaki Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, ni lazima ije sheria ya ugatuaji ambayo itaelezea vizuri majukumu ya Serikali Kuu na majukumu ya Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, itaainisha vyanzo vya fedha kwa Serikali Kuu na vyanzo vya fedha kwa Serikali za Mitaa. Sasa hivi kuna kuchanganyana. Vyanzo vyote vya fedha vya kuaminika vipo Serikali Kuu. Vyanzo vya fedha vya Serikali za Mitaa siyo vya kuaminika, havitabiriki, na siyo vya kuleta mapato kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, huu mpango unaelezea vizuri kwamba lazima kuwe na maboresho katika uendeshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, na kukawa na wazo kwamba hata Wakurugenzi sasa wapatikane kwa njia ya uwazi, wasailiwe na nafasi ziwe za ushindani. Mimi ninashauri tusiishie tu kwa Wakurugenzi, twende mpaka kwa Wakuu wa Idara, nao wapatikane kwa ushindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunapofanya hayo tusiangalie upande mmoja wa *management,* tuangalie na hadhi ya

Madiwani katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kama Diwani tunampa kutunza shilingi bilioni 100 kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa, inakuwaje Diwani yule anakwenda kule kwa posho ya shilingi 300,000/=? Kwa hiyo, ni muda muafaka sasa hivi tuangalie hata hadhi ya Diwani, tuangalie sifa ya Diwani, tuangalie majukumu ya Diwani ili waweze kuzisimamia vizuri Serikali zetu za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, ili kweli tuboreshe utawala kwenye ngazi ya chini, twende mpaka kwa wenyeviti wa Serikali za Vijiji, mpaka na Wenyeviti wa Mitaa. Majukumu yao sasa yameongezeka. Majukumu ya Mwenyekiti wa Mtaa leo siyo yale ya mwaka 1971. Kwa hiyo, ni lazima tuangalie zile hadhi zao, tupandishe hadhi zao, na tuhakikishe kwamba tunawatengenezea mazingira wezeshi ili waweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendeshaji wa halmashauri una changamoto. Sisi wakati wa bajeti hapa tunakaa miezi mitatu kujadili bajeti. Hivi inawezekanaje Madiwani wanakwenda halmashauri kwa masaa matatu wanapitisha bajeti ya mwaka mzima, tena kwa idara zote nne kwa masaa tu? Hicho kitu hakiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wanakwenda pale wanaweka makabrasha yao, na ukikuta Mkurugenzi ambaye yuko *smart,* anamwambia karani wagawie posho sasa hivi. Akianza kuzungusha karatasi ya posho tu basi, wote wanaangalia saa, wanaangalia wakapande magari, wanatawanyika. Hatuwezi kuendesha hivyo Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Lazima tuwape siku za ku-*debate* hiyo halmashauri yao. Tuwape siku tatu siku nne wajadili bajeti ya halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tuangalie hata uendeshaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Je, kwa muda tulionao huu, hivi bado kweli Baraza la Madiwani liendelee kuwa Mamlaka ya Nidhamu kwa watumishi wa halmashauri? Mamlaka ya Nidhamu ambayo Mkuu wa Idara anaweza akasema Kamati ile ya Fedha ina Madiwani wakorofi watatu. Kesho akaenda kuwarubuni,

amefanya ubadhirifu inaonekana kwamba tumwachie tu tumsamehe. Kwa hiyo, vitu kama hivi inabidi vibadilishwe katika Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mengi ya kuelezea kwenye Serikali za Mitaa, lakini ninaomba niishie hapo. Lazima tufanye mabadiliko ya kweli ili kweli tupeleke nguvu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Kamati ya Bajeti, kwanza niwapongeze sana, wamefanya uchambuzi mkubwa sana. Wao vilevile wanampongeza Rais kwa kuongeza bajeti. Walipopitia pale Mwongozo wa Mpango wa Maandalizi ya Bajeti wamempongeza Mheshimiwa Rais kwa kuongeza bajeti ya sekta ya elimu. Nami pia ninaungana nao kwa sababu sasa hivi bajeti ijayo itatoka shilingi trilioni 7.3 kwenda shilingi trilioni 8.19, sawa na ongezeko la 10.4%. Hili ni ongezeko kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, hizi fedha ambazo zinaongezeka zisiende kwenye miundombinu tu, tumwangalie na mwalimu mwenyewe ambaye anafanya mabadiliko katika sekta ya elimu. Hakuna elimu pasipokuwa na mwalimu mahiri. Ni lazima tumwezeshe mwalimu kwa *in-service training*, tumwezeshe mwalimu kwa maslahi yake, walimu wapate stahili zao kwa wakati ili waweze kuchapa kazi vizuri. Tukiwawezesha walimu kama anavyowekeza Mheshimiwa Mama Samia, matokeo yanaonekana. Sasa hivi *Division One* zimejaa kwenye shule za kata na matokeo mmeyaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti tukiendelea kumthamini mwalimu, tukiendelea kuwekeza kwa walimu, matunda yataonekana vizuri katika shule zetu za kata. Kwa hiyo, zitengwe fedha za kutosha kwa ajili ya kutoa motisha kwa walimu, zitolewe fedha za kutosha kwa ajili ya mafunzo kazini kwa walimu, na pia stahili zao zilipwe kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule mtindo wa baada ya miaka minne inaundwa timu ya kushughulikia madeni ya walimu,

hapana. Walimu walipwe kwa wakati. Hakuna sababu ya kuunda Tume ya Kushughulikia Madeni ya Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwenye Mapendekezo ya Mwongozo wa Utayarishaji wa Bajeti nichangie mambo mawili. Suala la kwanza ninashauri kwamba, kwenye mwongozo yatolewe maelekezo mahsusi kwa Maafisa Masuuli katika bajeti ijayo kwa mambo mawili. Jambo la kwanza ni kwamba wasianze miradi mipya, tukamilishe viporo vya zamani. Hakuna haja ya kuanza miradi mipya wakati tuna viporo hatujakamilisha. Pili, zitengwe fedha za kutosha kulipa madeni ya wazabuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Chikota. Nilimwita Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga, Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma, Mheshimiwa Festo Richard Sanga, Mheshimiwa Saashisha na Mheshimiwa Ester Bulaya wajiandae. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hii mipango ya muda wa kati, muda mfupi, na muda mrefu. Nami nianze kwa kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wote wawili kwa wasilisho zuri sana ambalo lina takwimu za kutosha. Vilevile ninampongeza Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa uwasilishaji mzuri sana wa taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nianze kwa kuchangia sehemu ambayo Kamati ya Bajeti imependekeza kwamba Serikali ione uwezekano wa kuanzisha sera na sheria ya tathmini na ufuatiliaji *(Monitoring and Evaluation)*. Hili ni jambo muhimu sana kwa sababu ukiangalia fedha ambayo Serikali inaelekeza kwenye maendeleo ni fedha nyingi sana. Ni kiasi kikubwa cha fedha ambayo inatoka kwenye vyanzo mbalimbali, ambavyo vingine ni mikopo. Mikopo, mapato yanayotokana na kodi na vyanzo vingine mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana kukawa na sera ambayo imeandaliwa kwa ajili ya kusimamia mambo ya tathmini na ufuatiliaji, kukatungwa na sheria, ikapitishwa na Bunge kwa ajili ya kuelekeza mambo mbalimbali. Hii ni muhimu sana kwa sababu fedha ambayo inaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo ni kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi tunacho kitengo katika Ofisi ya Waziri Mkuu ambacho kinafanya *Monitoring and Evaluation*. Vilevile kwenye Wizara ya Mipango na Uwekezaji nako ninaamini kuna kitengo ambacho kinafanya kazi hiyo. Hata hivyo, tungekwenda mbali zaidi. Hiyo ingejichukulia kama ni vitengo tu kwa ajili ya kuishauri Serikali upande wa ndani, lakini tukija na sera na sheria ikaundwa na taasisi maalumu ya kusimamia, kwa sababu hata kwenye maeneo ya ukaguzi kuna ukaguzi wa ndani, *(internal auditors)* na vilevile kuna *external auditors*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile inasaidia sana mtu asiweze kujichunguza mwenyewe. Yaani Serikali hiyo hiyo inafanya miradi, lakini inajichunguza yenyewe. Kwa hiyo, ili tupate maoni yenye uhuru, ni vizuri tukawa na taasisi ambayo ni *independent* kabisa, ikiwezekana kama ilivyo taasisi ya *CAG*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingine ukiangalia, unaona hadi wa Wizara kabisa ambayo inasimamia mambo ya tathmini na ufuatiliaji. Ikiwa taasisi, kwa kweli itakuwa na uhuru mkubwa zaidi na itaweza kutushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachukua mikopo kwa ajili ya kuwekeza kwenye miradi ya maendeleo. Unakuta mradi umechelewa kutekelezwa, lakini muda wa mkopo kuanza kulipwa tayari umeshafika. Kwa hiyo, tunampa kazi Waziri wa Fedha kutafuta fedha nyingine kwa ajili ya kurejesha ule mkopo. Kumbe mradi ule ambao umechukua mkopo ungekuwa umesimamiwa vizuri, ungekamilika kwa wakati, ungelipa deni wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sasa, mambo haya ili tuweze kuyafanya vizuri, ninapendekeza kwamba hili suala ambalo Kamati ya Bunge ya Bajeti imeweza kushauri ya

kutungwa kwa sera, sheria, na kanuni ikiwezekana kwa ajili ya tathmini na ufuatiliaji, vilevile twende mbali zaidi tuunde na taasisi ambayo itakuwa huru na ambayo haitaingiliwa na chombo chochote kama alivyokuwa *CAG* ili waweze kufanya kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itatusaidia sana tunavyozungumzia hii Dira ya Maendeleo ya Taifa, na haya mageuzi ya kimifumo na kubadili *mindset* ambapo Mheshimiwa Waziri ameelezea kwenye ripoti yake tutaweza kwenda sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imesisitiza, na siyo mara ya kwanza kuzungumzia umuhimu wa Serikali kutenga angalau asilimia moja ya pato la Taifa kwa ajili ajili ya tafiti. Tukitenga asilimia moja kwa ajili ya tafiti, tukavishirikisha vyuo vyetu vikuu, tuna Chuo Kikuu cha Sokoine, tuna Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na vyuo vingine, Chuo Kikuu cha Dodoma, hizi fedha wakashirikishwa ili ziweze kuelekezwa katika tafiti, tafiti zitatusaida kuwa na sera ambazo zimefanyiwa tafiti nzuri, ambazo zitakuwa zinajibu changamoto halisi za kwenye jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu sana kwenye pato letu la Taifa Serikali ikafuata ushauri wa Bunge ambao unaielekeza kutenga asilimia moja kwa ajili ya kuelekeza kwenye tafiti mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo lina umuhimu mkubwa sana lakini vilevile hata kwenye upande wa hizi sera, sheria; tulikuwa na ile Tume ya Kurekebisha Sheria na yenyewe ikipewa fedha iweze kufanya tafiti kuona sheria ambazo zinaweza zikawa kikwazo katika kufikia malengo ya utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050. Kwa hiyo, kuna umuhimu sana, kwa sababu unaweza kukuta kuna *gaps* nyingi sana katika mipango yetu, katika sera zetu. Kwa hiyo, hao watafiti mbalimbali watatusaidia kuonesha maeneo yenye upungufu ili tuweze kuyafanyia marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaiomba Serikali ipokee ushauri wa Bunge, asilimia moja ya pato la Taifa liweze kutengwa

kwa ajili ya tafiti. Tafiti hizi zifanywe na taasisi mbalimbali za Serikali. Kwenye kilimo kuna taasisi nyingi sana ambazo zinahusika na tafiti za mbegu; na tafiti za mambo ya uongezaji thamani wa mazao na vitu vingine. Kwa hiyo, ziweze kupewa fedha kwa ajili ya kufanya tafiti ili sera zetu na mipango yetu iweze kuwa na uhalisia isiwe na pungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kwenye taarifa hizi kuna hoja ya ugharamiaji wa mpango. Serikali imetuletea taarifa kwamba mpango elekezi wa muda mrefu unagharimu Dola za Marekani bilioni 3,582 na katika hizo, 70% Serikali inatarajia kuzipata kwenye sekta binafsi wakati 30% zitagharamiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tukiangalia mazingira ya sekta binafsi hapa nchini katika eneo la ukuaji wa uchumi wa nchi yetu, maeneo mengi ambayo ukuaji wake unaenda vizuri yametegemea zaidi uwekezaji ambao umefanywa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sekta binafsi bado zina changamoto nyingi. Kwa upande wa mikopo, sekta binafsi bado wana changamoto ya kupata mikopo ambayo ina riba nzuri, ambayo itapatikana kirahisi ili wakienda kuwekeza waweze kufanya biashara na Serikali iweze kupata kodi za kutosha na ukuaji wa uchumi uweze kwenda kwa kasi. Kwa hiyo, mazingira ya ufanyaji biashara bado ni changamoto. Pia hilo suala la *mindset* za watumishi bado ni changamoto kwenye baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilikutana na mtu mmoja analalamika kwamba yeye ana biashara, ana *TIN number*, sasa kutokana na shughuli zake kuwa nyingi alikosa muda wa kwenda kufuatilia leseni ya biashara. Kwa hiyo, alimtuma mtu mwingine ili anavyopata ile leseni ya biashara maana yake analipa mapato Serikalini. Alipofika kule kwenye halmashauri (ninaomba niihifadhi) akaambiwa hii *TIN* haina majina yako. Kwa hiyo, uje na kiapo kutoka kwa mwanasheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa *mindset* kama hizi, kwa sababu mtu anakuletea fedha, unamwambia alete kiapo

kutoka kwa mwanasheria kwa ajili ya kupeleka kwenda kufanya *assessment* ya kodi. Kwa hiyo, vitu kama hivi ninafikiri *mindset* za aina hii tuweze kuziepusha na urasimu ili tuweze kufikia malengo haya ya hii mipango ya maendeleo ni muhimu sana tukaangalia hili eneo la sekta binafsi tukapunguza urasimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tukahakikisha kwamba sekta binafsi zinapata mikopo ambayo ina riba nafuu, kwa sababu ukiangalia mikopo mingi ambayo wanachukua sekta binafsi, riba zake zinaanzia 15% mpaka 24%. Kwa hiyo, sasa hii ni riba kubwa sana na inaweza ikawa ni kikwazo kikubwa sana kwa sekta binafsi kuchangia kwenye utekelezaji wa hii mipango ya muda wa kati na muda mrefu ambayo tunaielezea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati anajibu swali la Mheshimiwa Sanga Nyakisa, ameeleza kwamba mambo ya mikopo yanategemea zaidi nguvu ya soko, lakini ninadhani kuna haja ya kuangalia vizuri hapa ili sekta binafsi iweze kupata mitaji ya kutosha kwenda kuwekeza na itakayosaidia kwenye utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kama ambavyo tumezungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia pia sekta binafsi zinakabiliwa na changamoto ya utitiri wa kodi. Kwa hiyo, tuangalie kodi zetu zile za Serikali Kuu na kodi zinazotozwa na halmashauri zetu, Serikali za Mitaa tuone zile kodi ambazo ni kikwazo katika maendeleo ya nchi yetu katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa ili tuweze kuziweka sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, eneo la mwisho ni eneo la miundombinu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, muda wako umeisha.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana, na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, nilimwita Mheshimiwa Joseph Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi, kwa mara yangu ya kwanza leo toka tuchaguliwe. Ninawashukuru wananchi wa jimbo langu kwa kuendelea kuniamini na mimi nitaendelea kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninaomba nitoe mchango wangu kwa Mapendekezo ya Mpango tunaoujadili. Kwanza nina imani kubwa sana na Profesa kama msimamizi wa Mpango na Waziri. Tunamwelewa, lakini ninaoushauri ambao ninadhani ni vizuri nikatoa ushauri. Kwa muda mrefu nikiwa Bungeni, sisi Tanzania hatuna shida na mpango na mawazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo tunayo mengi sana, sana tu, mpaka na ziada na *library* tumeweka, tatizo ni utekelezaji wa Mpango wenyewe. Kila mwaka tunapanga vizuri, linapofika suala la utekelezaji tunatawanyika na mara nyingi Waziri wa Mpango anakuwa kivyake, Waziri wa Wizara nyingine hamzungumzi lugha moja kwenye kutekeleza huu Mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka maandiko yanakuja yanasema tuwaimarishe wakandarasi wa ndani. Nyinyi wote humu ni mashahidi tunatoka kwenye jamii inayotuzunguka ya wakandarasi. Kama kuna watu wanaishi maisha ya vidonge vya presha kwenye mifuko ni wakandarasi. Tunazungumza tu kirahisi tuwaimarishe, lakini kazi zinapotoka wanapewa wageni na ukisoma mikataba ya wageni ina kikomo. Ukichelewesha kulipa, unapigwa *penalty*. Ukienda kwenye mikataba ya wazawa, unamcheleweshea hata miaka miwili kila siku wanajikomba maofisini. Hii siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatengeneza mpango mzuri, lakini kuusimamia hatuwezi, na mimi nimwombe Profesa, nimeona amesema anataka kuwaimarisha wakandarasi wa ndani. Hivi kwa nini kuna kazi tunaweza tukasema kuanzia hata shilingi bilioni 50, hata shilingi bilioni 100 zote wapewe wazawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unaweka kazi, unawashindanisha na wageni. Wageni wanajua ku-*lobby*, wana-*lobby,* halafu wakandarasi wetu wanabaki kuhenyeka na vumbi na kulipa hatuwalipi. Hii siyo sawa. Kama kweli tunakubaliana kwamba tunataka kuimarisha wakandarasi wetu wa ndani, ni vizuri tukatenga kiasi cha fedha kama shilingi bilioni 50 au shilingi bilioni 100. Hizi zisishindaniwe na wageni, zishindaniwe na wazawa. Hapo ndipo tutakapoimarisha uchumi wa nchi yetu kwa sababu pesa yote itabaki huku kwetu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi sana kusikia Wenyeviti wa Bodi sasa wataingia kwa kushindana. Hili ni jambo zuri sana na mimi leo ni kama mara ya nne ninazungumza. Mwenyekiti wa Bodi ndiyo mbeba maono. Sasa mara nyingi imekuwa kama cheo cha shukurani. Mtu anastaafu na miaka 70, kashindwa kufanya kazi vizuri akiwa kazini, ameshakuwa mstaafu, maisha yamempiga kule, unamchagua tena unampa bodi, hana atakachopoteza na muda wake wa Mungu umeshafika miaka 70. Kwa hiyo, anaenda pale kukaa tu na kusinzia, matokeo yake tunaanza kusumbuana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. Ninafurahi waingie kwa ushindani, lakini na umri pia. Mtu akishastaafu anatakiwa apumzike, mawazo mapya yaingie. Ninatoa mfano mmoja, tulipata Mwenyekiti kwenye Kamati yetu ya Nishati, Nyansaho ambaye sasa ni Waziri wa Ulinzi, ni kijana. Kapiga kazi vizuri, kapelekwa *NSSF*. Kapiga kazi vizuri, leo ni Waziri hapa. Sasa unachukua mtu amesha-*expire,* tena unamtundika kazi ya kuzurura, haiwezekani. Anataka kwenda akajiridhishe mradi, anataka kwenda sijui Liganga na Mchuchuma, ukiangalia hapa ana pingili zimechengana, basi anafanyia kazi kwenye simu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninadhani hili wazo ni zuri kabisa kwamba ipatikane hiyo kazi kwa ushindani, lakini pia na umri uwepo kwamba tunashindana na watu wa *design* gani? Ukishindanisha watu wameshastaafu, ana uwezo hawezi ku-*compete* na kijana wa miaka 45 katoka Chuo Kikuu, lakini ana

mawazo mazuri. Kwa hiyo, ninaomba sana, hilo tuliweke kama ninavyoshauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni utekelezaji wetu wa mipango. Mipango inakuwa mizuri, lakini kama Serikali inakuwa haiongei lugha moja, ni tatizo. Ninatoa mfano wale mnaotoka Dar es Salaam, sisi tulipanga vizuri, tutajenga barabara za mwendo kasi; na tutajenga barabara za njia nne. Ninyi mnaopita ile barabara, ukishuka *Airport* niambieni mmefananisha na nchi gani ile barabara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazunguka wote huko duniani. Nchi gani unatoka *Airport* vizuri, ukishaingia hiyo barabara ya kwenda Posta, yaani gari inaenda hautulii, inazunguka hivi, inazunguka hivi, wakati huku mliacha eneo? Ramani mliitoa wapi hiyo ya njonginjongi, hizo kona kuanzia mwanzo mpaka mwisho, eeh!

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunatengeneza Barabara kwenda mpaka Tegeta. Kwa hiyo, chukua mfano mtu anayeishi Tegeta, akitoka *Airport* ya Dar es Salaam zile kona unahesabu moja mpaka utafika Tegeta kona 100 *concentration* ya kustarehe kwenye gari hamna. Huo Mpango ulitengenezwa na nani? Mlijifunza wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niwashauri sana ndugu zangu, kwa kweli tunafika mahali tunaona sasa kama Serikali haizungumzi lugha moja. Ni vizuri ikawa na lugha moja, wanapotengeneza Mpango washirikiane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunajenga barabara, baada ya miezi miwili au mitatu unaona tena wengine wanakata barabara, wanapitisha waya wa umeme; wanakata barabara wanaweka mabomba; jamani eeh! Kwani kwenye mipango yao hawajui kama huku kuna watu, huku hakuna watu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani hiki kitu tunafika mahali kushauri kwa kweli mtaona kama tunawapinga, lakini ndugu zangu hasa waliobahatika, ma-*engineer* na wasomi tuliowaamini

kwenye Wizara, watengeneze mpango wa pamoja, washirikiane. Wanapotengeneza, kila mtu alete hitaji lake, wanapotaka kutengeneza kitu kimoja, lakini siyo tunatupa fedha leo, baada ya wiki moja tena, unakuta *grader* zinalia, tunapitisha bomba la maji kupeleka kulia. Hili ni Taifa la wasomi, na sisi tunawaamini. Tengenezeni vitu vya kisomiki, msitengeneze vitu vya *blah blah*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekuwa kwenye Kamati ya Nishati muda mrefu, tumeshauri kwenye Madini. Mwaka 2017 ukiangalia makusanyo yaliyokuwa yanakusanywa kwenye dhahabu, leo tunachangia 10%, lakini kuna vitu tunazungumza leo mwaka wa tatu tupo humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alikuja Waziri Mavunde hapa akasema *Vision 2025/2030* tunanunua ndege tupime. Eneo letu limepimwa 16%. Tunaimba kila siku, leo mwaka wa tatu bado tuna-*order* ndege. Hii ndege inatengenezwa wapi? Tununue ndege ili tupime, tukusanye dhahabu. Ninyi wenyewe mmeona mafanikio kutoka sifuri; leo tuna tani 17 ndani ya miezi 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiona ng'ombe anatoa maziwa, mlishe na majani ili maziwa yatoke mengi. Sasa tunakuwa tunapanga vitu halafu kukamilisha hatukamilishi, sasa hii inakuwa kiukweli siyo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana Profesa, mimi ninamwamini sana. Profesa, nina imani atasimamia vizuri…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninaomba nizungumze. Mimi ni Mbunge wa awamu ya tatu na nilikuwa ninafuatilia sana Bunge…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** …hasa Wabunge wanaotokea Kanda ya Ziwa. Wabunge, wanaotokea kanda ya ziwa tumezungumza suala la *Airport*…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma, kuna Taarifa.

**TAARIFA**

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpa taarifa kaka yangu Musukuma, mtu bingwa wa Jimbo la Geita. Nimpe tu taarifa kwenye kile alichokuwa anazungumza kuhusu madini, mimi ndio mchimbaji mdogo katika nchi hii. Ninapenda kumpa tu Taarifa kwamba juzi Mheshimiwa Mavunde, Waziri Makini wa Wizara ya Madini, amerusha ndege ya *Barrick* kwa ajili ya uanzishwaji wa kupima maeneo kwa ajili ya madini, alikuwa hajapata hiyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamkaribisha Bungeni. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, mimi sizungumzii ndege ya Barrick, nazungumzia ndege ya Serikali, ya kwetu wenyewe. Hatuwezi kutumia ndege za kuazima watu. Kwa hiyo, karibu na ninakushukuru sana. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kushauri. Kwa kweli, tufike mwisho. Hebu oneni aibu. Mimi nimekuja hapa mwaka wa 15, kulikuwa na Wabunge, na Wabunge, na Wabunge tunazungumza *Mwanza International Airport*. Kwani hamwoni aibu! Yaani kila mwaka mnatuambia tunakarabati. Profesa Mbarawa yupo hapa, alinialika kwenda kutia saini, tukazungusha na mabati, tukafanya na sherehe, tukapiga na ving’ora, sasa hivi mmeng’oa tena na mabati na mkandarasi hayumo. Hivi jamani mnatuonaje eh? Mpaka tuongee nini sasa ili mjue kama mnatukera eeh?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli sisi Mwanza ni watu wa kuzidiwa na *Airport* ya Arusha Mjini ndogo ile? *Airport* ndogo, mnaweka mavioo, mnaweka manini, sisi mnatuzungushia mabati! Hapana. Profesa niwaombe tufike mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sehemu yenye uchumi mkubwa kwenye mambo ya ndege ni Mwanza, lakini tunakuwa wa mwisho, tunazidiwa mpaka na Ibadakuli. Mpaka tuongee nini sasa? Tuongee nini? Sehemu ambayo mnapeleka ndege moja kwa wiki, tunajenga majengo mazuri, tumejenga *runway* kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ambayo tunapeleka ndege mpaka *dreamliner,* tunakaa tunaongea kitu hakifiki mwisho. Mnapanga mipango mwaka huu, tunakuja tunapangua tena, tunaweka mwingine, tunapangua. Ni nini kimetokea mpaka mmemwondoa mkandarasi aliyekuwa pale? Ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mlizungusha mabati, tumeshindilia, tukaanza kung'oa vioo. Sasa hivi vioo vinaanguka, mkandarasi naye ametoa vitu. Jamani, fikeni mahali mwone huruma. Nasi ni kipande cha hii Serikali, na tunauchangiaji mkubwa sana kwenye mapato ya hii nchi, na sisi ndio tunaongoza kusafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanda ya Ziwa ndio tunaongoza kusafiri. Tumejenga mpaka Uwanja wa Musoma, tunauzindua; wa Mwanza ni stori, ni *swagger*. Tukishuka pale na *Dreamliner,* hamna hata pa kujikinga, wageni wanaloa na mvua. Au nani ameturoga kwenye huu uwanja wetu wa Kanda ya Ziwa? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe sana tufikie mwisho. Tunapopanga mipango ifike mwisho. Profesa kama na mwakani tena tukiwa hai, akija tena na Mpango wa 2027/2026, tunaupiga chini. Mimi nikueleze ukweli.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ahsante, muda wako umekwisha…

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Festo Richard Sanga. Ajiandae Mheshimiwa Saashisha Mafuwe na Mheshimiwa Ester Amos Bulaya.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye Mpango huu wa Serikali. Nitakuwa na mambo machache ya kuzungumza. La kwanza, ninaipongeza Serikali kwa Mpango wao mzuri na hususan Mwalimu wangu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Mheshimiwa Prof. Kitila kwa uwasilishaji mzuri wa Mpango pamoja na Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache ya kuzungumza. La kwanza, ninalotaka kuzungumza ni kushauri. Kwanza kushauri kwenye utekelezaji wa Mpango, tunapokwenda kutekeleza Mpango huu, ni vyema tukaangalia wapi ambapo tumekwama? Moja kati ya maoni ya Kamati wanayoyazungumzia kwenye utekelezaji wa Mpango ni kwamba kuna mambo mengi hayajamalizika, na tunaenda kuanzisha mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni hoja kubwa sana kwenye Kamati wamelizungumza na hii inaendana na kwamba kukosekana kwa kitengo cha tathmini *(Monitoring and Evaluation)* ndicho kinacholeta haya ambayo yanaoonekana tunaanzisha mambo mengi katika Taifa na mengine hayajakamilika kiasi kwamba wananchi wanakuwa hawaoni tija ya utekelezaji wa Mpango husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimshauri Mheshimiwa Waziri, na Serikali. Cha kwanza ni kufanya tathmini, ni miradi ipi imekamilika na miradi ipi bado haijakamilika? *For instance,* kwenye miradi ya barabara, kila Mbunge akisimama hapa ndani anazungumza kwamba tumefanya sherehe kwenye kusaini mikataba, lakini barabara hizi hazijatekelezwa na hazijaanza kujengwa. Ukienda kwenye miradi ya maji, ukienda kwenye miradi mingine mbalimbali, sasa ni vyema Serikali ikafanya

tathmini ya miradi yote ambayo haijakamilika, tukamilishe ili tulete tija kwa wananchi waone kwamba Serikali imefanya kazi. Kuwa na viporo vingi vinaisababishia Serikali iwe na mzigo mkubwa inaopoenda kuanzisha na miradi mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kipindi hiki ambacho Mheshimiwa Rais, amejikita kwenye kuongeza ajira, tafsiri yake ni kwamba, *wage bill* inaenda kuongezeka. Mkienda kuanzisha pia miradi mingine, mnakuwa na mzigo mkubwa sana wa kutafuta fedha kiasi kwamba hiyo mingine inaenda kukwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninashauri kwenye utekelezaji wa mipango, tufanye tathmini ya hii miradi ya kimakakati ambapo tumeona kabisa kwamba Serikali inaenda kujikita kwenye sekta ya uzalishaji. Hatuwezi kwenda kwenye uzalishaji kama barabara hazijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kwenda kwenye uzalishaji kama miradi ya maji kwenye umwagiliaji haijakamilika. Hatuwezi kwenda kwenye uzalishaji kama sekta ya afya na huduma bora kwa wananchi hazijakamilika. Kwa hiyo, ni lazima kitengo cha tathmini na ufuatiliaji kiwekewe mkazo na kitungiwe sheria kiwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Mheshimiwa Rais ya kuanzisha Wizara ya Mipango ilikuwa ni kuona haya mambo yanaenda kufanikiwa. Sasa haiwezekani tukawa na Wizara ya Mipango na bado kwenye utekelezaji wa mipango tunakwama kwa sababu hakuna tathmini. Kwa hiyo, ninashauri ni muhimu tuwe na hicho kitengo cha tathmini na ufuatiliaji ili kuangalia jinsi gani miradi yetu inaenda kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumza, kwa mfano tu Wilaya ya Makete, barabara ya kutoka Makete kuelekea Mbeya, yenye takribani miaka minne toka tumesaini mkataba, *centimeter* moja ya lami haipo hadi leo. Sasa huu ni mfano tu, lakini barabara ya kutoka Njombe kuelekea Ludewa ni *same case*, barabara kutoka Lupembe kuelekea Morogoro ni *same case*. Barabara ya Mbeya Mjini pale kwa muda mrefu ime-*stuck*. Sasa ni vyema Serikali ikafanya tathmini kwenye hii miradi, ikakamilisha ili

tuweze kwenda kwenye hatua nyingine ili miradi iweze kuwa na tija kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ni kwenye vyanzo vya mapato. Hii mipango tunaizungumza kwenye utekelezaji wa mipango hii. Mipango hii haiwezi kukamilika kama hatuna fedha. Serikali yoyote duniani, cha kwanza lazima tujikite kwenye ukusanyaji wa fedha. Ukiangalia kwenye Mpango wetu, tunakiri kabisa na Kamati imekiri, 70% ya Mpango inaenda kutekelezwa na sekta binafsi. Sekta binafsi ndiyo inaenda kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tumpongeze Mheshimiwa Rais, kwa sababu ni maono makubwa kwenda kuibeba sekta binafsi. Sekta binafsi ni *engine* ya uchumi popote pale. Nyinyi kama Serikali hamwezi kufanikiwa kutekeleza miradi hii yote bila kutegemea sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye utekelezaji wa mpango huu lazima tuangalie vyanzo vya mapato. Mheshimiwa Waziri hatuwezi kuepuka kabisa kutafuta namna ya kupata fedha kupitia kwenye *e-economy,* kwenye *digital economy,* hii ni mifumo ambayo Mheshimiwa Rais amekuwa akisisitiza kuhusu Serikali kuwa na mifumo inayosomana, lakini kuachana na utaratibu wa kukusanya fedha kwa taslimu. Niipongeze Kamati ya Bajeti wameandika kabisa, kukusanya fedha kwa mfumo wa taslimu ni upotevu wa mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima twende kwenye mfumo wa kukusanya mapato kupitia mifumo na zaidi tupunguze idadi ya mifumo kuwa mingi Serikalini. Mifumo lazima isomane, ili mapato yaweze kutekelezeka. Ninampa tu mfano Mheshimiwa Waziri, ukusanyaji wa fedha kwenye Daraja la Mwalimu Nyerere; wakati wanakusanya fedha kwa taslimu walikuwa wanakusanya shilingi milioni 150, milioni 600, lakini kwa kukukusanya kupitia mfumo wanakusanya zaidi ya *1.5 billion* ndani ya mwaka mmoja. Maana yake ni kuna fedha nyingi zilikuwa zinapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda kwenye Hospitali ya Tumbi pale, Dar es Salaam, walivyokuwa wanakusanya kwa taslimu

walikusanya shilingi milioni 30, milioni 40, lakini sasa hivi kwa mwaka ni shilingi milioni 600, baada ya kufungiwa mfumo wa *GoTHOMIS* kuhakikisha kwamba, wanakusanya fedha kupitia kwenye mfumo. Sasa ni hospitali ngapi, ni maeneo mangapi, ambayo fedha hazikusanywi kwenye mfumo, zinakusanywa kwa taslimu na zinapotea? Kwa hiyo, Serikali ni lazima iangalie ni namna gani ya kuhama kabisa kuachana na ukusanyaji wa fedha kupitia kwenye hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumzia TEHAMA, Mheshimiwa Waziri, ni lazima iendane na *speed* ya *internet*. Sisi hapa tumekuwa ni mashahidi tunaenda kwenye kulipia hati unaambiwa mfumo uko chini, unaenda kulipia *TRA* unaambiwa mfumo uko chini. Taifa letu, kama dunia inakimbizana na ukusanyaji wa mapato kupitia mifumo, ni vyema tukaangalia kuboresha upatikanaji wa *internet* nchini yenye *speed,* yenye *standard,* ili hii mifumo iweze kukusanya fedha kwa uhakika na mapato yasiweze kupotea. Kwa hiyo, hilo ninaomba sana lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia *TCRA* wanahitaji kama shilingi bilioni 480 ninadhani, ili kuhakikisha kwamba, wanaweza kufanikisha hili jambo. Ninatumia nafasi hii kuwaomba kuimarisha *TCRA,* ili mifumo iweze kukusanya mapato na pia, kuweza kuboresha *internet* kwenye Taifa letu. Tunapozungumza, Mheshimiwa Waziri, kwenye suala la ukusanyaji wa mapato kupitia mifumo kuna namna nyingine ya kuangalia kupitia madini, kama ambavyo Serikali tumeona inafanya kazi ya kununua *gold* na kuhifadhi kwenye *BOT*. Bado wachimbaji hapa wamekuwa wanaomba pia, benki zitengenezewe wigo kuhakikisha kwamba, wao pia, wanakuwa na uhifadhi wa madini kwenye benki, kama wanavyohifadhi fedha. Hii yote ni kuhakikisha kwamba, uchumi unaendelea kuimarika na mipango yetu inaenda kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ninataka kulizungumza ni ambalo linahusisha upotevu wa mapato. Hatuwezi kutekeleza miradi hii kama rushwa itaendelea kushamiri kwenye Taifa letu.  Mikataba mingi inaigharimu fedha. Ukiangalia

Mheshimiwa Waziri tunatumia fedha nyingi kwenda kulipa watu ambao wameingia mikataba, ambayo baadaye imegeuka kuwa mizigo kwenye Taifa kutokana na kwamba, tumeshindwa kuitekeleza kwa wakati na zaidi rushwa kushamiri kwenye kusaini mikataba na kuliumiza Taifa. Tutakwamisha utekelezaji wa mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, *accountability* kama haiwezi kuchukua nafasi kwa Watumishi wa Serikali hatuwezi kufanikiwa kutekeleza kwenye hii miradi, lazima watu wawe *accountable*. Ninampongeza Mheshimiwa Waziri kuja na mfumo wa kushindanisha watu kupata watu bora kwenye usimamizi wa wakurugenzi wa hizi taasisi na mambo mbalimbali. Kwa sababu, kati ya eneo ambalo Serikali imekuwa iki-*inject* fedha ni kuwekeza hizi taasisi mbalimbali ziweze kujiendesha, lakini tuna-*injec*t fedha mwisho wa siku zinaliwa na mafisadi. Sasa ni lazima Serikali iangalie ni namna gani ya kuhakikisha kwamba, watu wanakuwa *accountable* na tunasimamia suala la upotevu wa mapato kupitia rushwa na kutokukusanya fedha kupitia mifumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninataka kushauri ni kuhakikisha kwamba, ndani ya Serikali tuna Wizara ya Vijana, ile pale, hakuna mpango unaweza kufanikiwa dunia hii, kwenye nchi yoyote, bila kuangalia Wizara ya Vijana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, cha kwanza, ndiye *champion* kuelekea mipango ijayo ya miaka 50 kwa kuanzisha Wizara ya Vijana. Sasa ukisoma kwenye ripoti mbalimbali inaonesha Tanzania tuna Mifuko zaidi ya 70 kwenye Wizara mbalimbali inayohusika na Wizara ya Vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hatuwezi kuwa na Wizara ya Vijana, lakini kuna Wizara nyingine huko zimekaa na mifuko ambayo inasimamia Wizara ya Vijana. Ni wajibu na ni muhimu kwa kipindi hiki Wizara zote ambazo zina mifuko mbalimbali ambayo inahusisha vijana mifuko hiyo ielekezwe kwenye kapu moja isimamiwe chini ya Wizara ya Mheshimiwa Joel Nanauka, Wizara ya Vijana na Maendeleo, ili angalau kwenye hili kapu tukisimamia tuwe tuna uwezo wa kufanya *monitoring* kwamba, ni Mfuko gani na Mfuko gani haujafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye hii mifuko 70, kwenye ripoti, inaonesha tumekopesha zaidi ya shilingi trilioni 3.5 kwa vijana zaidi ya 24,000,000. Sasa kama tumekopesha hizo pesa na vijana nje wanalalamika ajira hazijapatikana, ni nani anayekula hizo fedha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima tuwe na kapu moja ambalo linaweza lika-*control* Mifuko yote, ambayo inaweza ku-*support* vijana kwenye nchi yetu. Tofauti na hapo kufanya Wizara ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuwa na Mfuko wa Vijana, Wizara nyingine tena ina Mfuko wa Vijana, hii mifuko ilivyosambaa kwenda huku ndipo tunaruhusu kuonekana ule utendaji kazi wa hii mifuko usiwe na tija. Kwa hiyo, ni lazima Wizara ya Vijana iwezeshwe iweze kupewa hiyo Mifuko yote isimamiwe ndani ya kapu moja, ili Waziri wa Vijana awe na nguvu ya kufanya hiyo kazi. Hayo ni maoni yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ninaendelea kushauri kwamba, sekta ya kilimo ni vyema pia ikaendelea kuwezeshwa kwa sababu, ni eneo ambalo katika nchi yetu linaongeza sana kwenye suala la uzalishaji. Mvua imeanza kuwa inakata kutokana na mabadiliko ya tabia ya nchi, kwa hiyo, tumejikita kwenye kilimo cha umwagiliaji. Tunatamani sana tuendelee kuweka fedha nyingi kwenye kilimo cha umwagiliaji, ili wakulima wetu waweze kubadilisha mazingira ya kutegemea mvua, sasa wawe na uwezo wa kutegemea maji kwa msimu mzima tuweze kulima kwa sababu, bila kilimo Taifa letu litapata wakati mgumu na pia, sekta nyingine zitakwama. Kwa hiyo, ninaendelea kuhamasisha kwamba, tunavyohamasisha kilimo, tuhamasishe pamoja na barabara za *TARURA*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwani dakika zimeisha?

**MWENYEKITI:** Ndyio, muda wako umekwisha Mheshimiwa. Ninakushukuru.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aah! Sijaanza hata kuchangia. Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Nilimwita Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi ili niweze kuchangia kwenye Hotuba ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa. Kabla sijachangia ninaomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali cha kurudi hapa Bungeni na niwashukuru sana wananchi wema wa Jimbo la Hai kwa kunipa heshima nyingine ya kuwa Mbunge wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kushukuru chama changu kuanzia ngazi ya Taifa, Mwenyeketi wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mpaka ngazi ya Mwenyekiti wa Shina kwa kunipa hii heshima. Ninawaambia tu yale ambayo tulifanya miaka mitano iliyopita na sasa tunaenda kufanya zaidi ya hapo na wao ni mashahidi. Hivi ninavyoongea, kwa kipindi ambacho tumeingia, tayari mkandarasi yuko *site* anajenga Soko la Kwasadala, mkandarasi yuko *site* anajenga Soko la Mula, mkandarasi yuko *site* anajenga Ofisi ya Wilaya ya Hai, mkandarasi yuko *site* anajenga nyumba ya Mkurugenzi. Hii ni miradi mipya ambayo tumeanza nayo na hiyo ndio *speed* ya Mama Mheshimiwa, Dkt. Samia na tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kuchangia hotuba hii, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Waziri, hotuba imeandikwa vizuri, kitaalamu kabisa, hii inadhihirisha uprofesa wake. Ninampongeza sana na wasaidizi wake, pamoja na Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma mpango huu vizuri, umesheheni takwimu na unaonesha kweli dira. Nimesoma Mpango wetu wa Taifa wa Miaka 50 kweli, unawiana na takwimu zipo za kutosha kwa kweli, lakini Mheshimiwa Waziri nina jambo

ninataka kushauri, namna ya kuweza kushusha mpango huu kuuleta chini na vitu viweze kuwa halisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kutambua uwezo wa Waziri na wasaidizi wake, lakini nimekuwa nikishauri hapa tutengeneze timu ya wataalam, watafute jina lolote watakaloita, hawa wataalam wakae chini wawe ndiyo watu wanaofanya tathmini ya mipango yetu na wanaojibu maswali magumu yanayohusu Taifa letu. Walipwe vizuri, wawe nje ya utumishi wa umma tuliouzoea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza kuanza kwa sababu, ninajua yanahitajika mabadiliko ya kisheria, tunaweza kuanza na *lab* za wataalam wakutane na jopo la wataalam kutoka sekta zote wakae watafute majawabu. Kwa nini tuna Ziwa Victoria, lakini ukienda watu wa Mwanza, watu wa Ilemela, bado wana shida ya maji? Hapa Dodoma tunaambiwa *water table* ipo kubwa na maji ya kututosheleza, kwa nini hatuna maji? Kwa nini, tukitoka hapa Dodoma kwenda kuikuta Singida mashamba yako ya kutosha, lakini ukiangalia takwimu zinaonesha hali ya ukosefu wa chakula, umaskini wa chakula ni asilimia nane?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa timu hii ikae vizuri tutafute mfumo wa kuajiri wataalam hawa. Ninaamini nchi hii bado ina vijana wengi wenye uwezo mkubwa, wachaguliwe kwa sifa zao, wapewe *security of tenure* ya kutosha, ikiwezekana twende Masaki pale tuwatafutie nyumba za kukaa tuwape magari mazuri, watoto wao tuwalipie ada, wakae wawe ni watu *free from politics* wawaze na watutafutia majibu. Waje na *theories,* wazipime, tuje kwenye utekelezaji, ndiyo mambo haya mazuri yanaweza kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kwa sababu, ukitazama mambo haya yalivyo mengi yanachangiwa, yana falsafa ya kwako wewe mwenyewe, kama Profesa kesho akiwa hayupo tunayawekaje? Tuna ya *ring fence* vipi, lakini, kukiwa na hiyo *intellectual team* itahakikisha haya mambo, tutawapa nguvu ya kisheria, watayasimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliona nianze na hilo, lakini nimesoma taarifa hii, ninarudia tena, ukurasa wa sita umesema hali ya umaskini wa chakula ni asilimia nane. Sasa ninajiuliza mpaka leo tunahubiri hali ya umaskini wa chakula kwa nini? Taifa lenye watu wasomi namna hii!

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeonesha pale namna ambavyo wamekuza eneo la umwagiliaji. Ninaomba kama kuna eneo ambalo linaweza ku-*capture* Watanzania wengi ni kilimo. Tuondoke kwenye kilimo cha karatasi twende *site* tukalime kwelikweli, tuweke mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafikiri tungeweza ku-*site zone,* labda tuseme Ukanda wa Kaskazini, mikoa hii izalishe mazao ya aina fulani twende tukuze umwagiliaji tuhakikishe maji ya kumwagilia yapo. Mle ndani tuweke viwanda vya kuongeza thamani ya mazao na kila Mkuu wa Mkoa apewe jukumu kwamba, wewe tunahakikisha kwa mwaka huu tunataka tani kadhaa za mahindi, za maharage; tukienda hivyo itatusaidia. Tutaongeza uzalishaji na sisi tutauza mazao nje ya nchi, pato hili la Taifa tunalolizungumza litakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huohuo naomba kule Wilaya ya Hai, sisi ni wakulima, tuna eneo dogo, lakini tuko tayari kulima kisayansi. Ninaomba wekeni kwenye mpango, tunajua tuna skimu ambazo zimeshafanyiwa *feasibility study;* Metromu, Makeresho, Bwawa la Borutu na nyinginezo, tuleteeni fedha kwenye skimu hizi, ili sisi Wilaya ya Hai tuwaoneshe kilimo kinavyolimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tuna Soko la Kwasadala pale na ikumbukwe ardhi yetu ni ndogo. Kwa hiyo, hizi skimu zikijengwa pamoja na Skimu Ndogo ya Ngusero, Mkalama, Kilanya na pale Urara, tukipata sisi tutawaonesha kwa vitendo na mimi Mbunge nitatangulia mbele, namna ya kuongeza uzalishaji, lakini profesa anafahamu katika dhana hii hii, ili tuondokane na neno umaskini wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Prof. Mbarawa anajua tulimaliza mgogoro pale *KIA,* wananchi wameondolewa na tumekubali, lakini ndiko tulikokuwa tunalima. Kwa sasa hivi hawahitaji hekta zote 11,000, kule Chekimaji kuna maeneo ambayo wananchi walikuwa wanalima wameondolewa. Ninaomba turudi kwa mkataba maalum tulime, kama tunavyofanya kwenye mashamba ya *NDC* pale *Kilimanjaro Machine Tools,* ili tuondokane na hali hii ya chakula. Vinginevyo, Mheshimiwa Profesa Mbawara na Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo, wajiandae tutakuja kuwaomba chakula. Hili jambo sidhani kama ni gumu kiasi hicho, tupo tayari, tunatambua ni maeneo ya *KIA*, watupe maeneo tukafuge, watupe maeneo pale tukalime kwa mkataba maalum na tuko tayari kulipia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni sambamba na mpango wa maendeleo. Tumezungumza hapa na bahati nzuri Serikali imekubali, Kiwanda cha *Kilimanajro Machine Tools,* ninafahamu suala la makaa ya mawe ya Liganga na Mchuchuma linaendelea vizuri, wakimaliza kile kiwanda wakifanye cha kuzalisha chuma. Waziri wa Viwanda anatikisa kichwa, ninamshukuru wa biashara pale. Maana yake ni hiki kitu na bahati nzuri ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni kwamba, kile kiwanda kitahamishiwa mahali kwenye benki ya ushirika, ili kiweze kuzalisha. Wakati tukiwa mbioni kusubiri chuma tuanze sasa kile kiwanda kukitanua, ili kiweze kuzalisha chuma kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona kwenye mpango wamegusa eneo la vijana na wakatoa takwimu kwamba, kwa mwaka 2025 vijana 62,570 wanamaliza vyuo vikuu. Nikajaribu kutafuta, kwenye mpango, hawa vijana 62,000 wanaomaliza vyuo vikuu mpango wao uko wapi? Wanaenda kuishia wapi? Tunampongeza Mheshimiwa Rais ametengeneza Wizara ya Vijana, lakini ninaomba, waende wakakae tena, hawa 62,000 wakija mtaani wanaenda kufanya jambo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu pekee ambayo ninaiona kwa haraka haraka, pamoja na viwanda na vitu vingine, ni kwenye kilimo. Tuwahamasishe vijana wawekeze kwenye kilimo na kwamba, mkulima isionekane ni adhabu au ni mtu wa chini.

Wale waliofanikiwa kwenye kilimo watumieni kuwashawishi na kuwahamasisha vijana wahamie kwenye sekta ya kilimo, ndiyo itakayotusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni pamoja na kurudisha vile vyuo vya kati vilivyokuwepo virudi kutoa elimu kwenye ngazi ya kati. Hii *population* ya vijana wanaomaliza vyuo vikuu, kama hatutaiangalia vizuri, hili ni bomu lingine linalotujia. Hawa vijana wana maono yao, wasipopata majawabu sahihi, ndiyo maana tunasema, hiyo *intellectual committee,* hicho kikosi kazi kiende kikatafute majawabu. Hawa vijana wanaomaliza vyuo vikuu baada ya kumaliza wanaenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa harakaharaka sana ninaomba ule mpango wa kuanzisha treni ya umeme kutoka Dar es Salaam kwenda Arusha waukimbize. Wanajua mikoa hii ya kaskazini ni *hub* pia, ya uchumi wetu. Tuombe hilo na lenyewe walitazame liende kwa haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana Serikali imefanya miradi mingi mikubwa, lakini kuna jambo ambalo sijaliona kwenye mpango vizuri, mpango wa matengenezo ukoje? Tumejenga shule nyingi, mpango wa matengenezo na ku-*maintain?* Tuna miradi mikubwa hapa, *SGR,* mpango wa matengenezo ukoje ili inapotokea kuna kitu kimeharibika kusiwe na fedha, tena tuanze kuhangaika. Hii miradi yote tunayoijenga, shule na nini, tuiweke kwenye mpango, kuwa na fedha ya matengenezo ili miradi yetu iweze kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tunaelekea mwishoni, ninaomba sana *Local Government Authority* iacheni ifanye kazi yake, iacheni i-*enjoy autonomy* yake. *Local Government* inaingiliwa sana, tuwape nguvu Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Vitongoji na Madiwani wafanye kazi yao kwenye *jurisdiction* yao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaongezee nguvu tena ya fedha, kama posho yao. Ninafahamu ni jambo kubwa, lakini tufikirie namna ya kuongeza posho ya Madiwani, posho ya Wenyeviti wa Vijiji, posho ya Wenyeviti wa Vitongoji...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwape wa-*enjoy full autonomy,* kama *Local Government* maana inaingiliwa sana na *Central Government.* Madiwani wanapanga hivi, anakuja mtu wa *Central Government* anapanga hivi, wakati wenye wananchi ni Madiwani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha. Tunakushukuru kwa mchango wako.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Ester Amos Bulaya. Ajiandae Mheshimiwa Masanja Kungu Kadogosa na Mheshimiwa Pius Zebhe Yanda.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchagia. Kwanza kabla sijachangia mpango ninawatoa hofu wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ipo kwa ajili yao, haijatoa maelekezo yoyote ya kuwasumbua wananchi wa Nyatwali, haijatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi nimetoka kuzungumza na Waziri wa Utalii na Waziri wa Ardhi, tayari ametoa maelekezo. Hakuna mtu wa kuwasumbua wananchi wa Nyatwali mpaka jambo lao liweze kukamilika; tayari nimeshalifanyia kazi Mbunge wao wa kazi kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachangia mpango. Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Wabunge, tutakubaliana kwamba, chakula, mazao, mbegu, ni usalama wa nchi. Bila mbegu bora hakuna chakula cha kutosha, bila mbegu bora hakuna mazao na, bila mazao bora hakuna masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa letu lina mahitaji ya mbegu tani 250,000, lakini uwezo wa Taasisi yetu ya *ASA* pamoja na wawekezaji binafsi wanaolima mbegu *capacity* yetu, ya uzalishaji wa mbegu, ni tani 70,000 inayobaki tunaagiza. Ni *risk* pia kwa Taifa letu watu wakiamua kuchochea vita ya kiuchumi kupitia sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti zilizofanywa, Mheshimiwa amezungumzia ukame, mbegu zinazozalishwa nchini kupitia Taasisi yetu ya Serikali *ASA* na wazalishaji binafsi zina uwezo wa kuhimili ukame. Sasa kwa nini, tusiiwezeshe Taasisi ya Serikali ya Wakala wa Mbegu *(ASA)* wakawa na uwezo wa kuzalisha mbegu za kutosha? Kwa nini, tusiwawezeshe wawekezaji binafsi wanaozalisha mbegu nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao wanazalisha tani 61,000. Taasisi ya Kiserikali ya *ASA* inazalisha tani 9,000 na hapo wana hekta 13,000. Zinatosha kwa uzalishaji wa mbegu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *imagine,* mbali na kutegemea mvua kwenye hiyo tani 9,000, *ASA* inachangia mapato ya Serikali shilingi bilioni 11 leo hii kwa hizo hekta 13,000. Kwa hii *ASA* (Wakala wa Mbegu) tukiweka miundombinu ya umwagiliaji itakuwa ina uwezo wa kuzalisha mbegu tani 22,000 na kuiwezesha Serikali kupata mapato shilingi bilioni 33. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *imagine* tukiwapa eneo lenye umwagiliaji wa hekta laki moja, *ASA* itazalisha mbegu kiasi gani? Tukiwawezesha wawekezaji wa ndani wanaozalisha mbegu tani 61,000, tukawawekea mazingira mazuri wana uwezo wa kuhakikisha usalama wa mbegu wa nchi yetu ni mkubwa na tusiagize mbegu nje ya nchi. Mbegu ni usalama wa nchi, mbegu

ni uhakika wa chakula, mbegu ni uhakika wa soko, halafu unakwenda kwenye masuala mengine ya pembejeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia huu mpango umesema zaidi ya 70% zitaenda kwenye sekta binafsi. Sekta binafsi utakuta kwenye kilimo, kwenye uvuvi, kwenye viwanda, leo hii kwenye sekta ya kilimo tunazo hekta milioni 29.4 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji, leo hekta ambazo zimeunganishwa mfumo wa umwagiliaji ni hekta 700,000 peke yake na tumeona mwaka huu tumekuwa na tishio ya hali ya hewa ya mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi leo tukiamua kuwekeza kwenye sekta ya umwagiliaji, tukasema tunafunga mkanda, tunaanza na hekta milioni tano, kwa wakulima wadogo wadogo kuunganishiwa mfumo wa umwagiliaji tutaongeza pato letu pia tutakuwa na uhakika wakulima muda wote eneo ambalo walikuwa wanalima kwa msimu mara moja watalima mara mbili, pili pato la mkulima mmoja mmoja litaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hata ile *idea* yako ya kusema lengo la kufikisha pato la Mtanzania mmoja mmoja mwaka 2050 kufikia dola 7,000 itatekelezeka kama haya yakikamilika hata huko 2050 hatufiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakutolea mfano tu kwa mkulima wa parachichi, heka moja ya parachichi yenye miche 80 mkulima mdogo mdogo ukimwezesha kupata miche bora, ukimwezesha kumpa miundombinu ya umwagiliaji, hiyo dola 7,000 anaifikisha kwa msimu huu, wala hasubiri 2050. Hujaenda kwa mkulima wa kahawa, hujaenda kwa mkulima wa alizeti na huku ndiko ambako umaskini upo mwingi, sekta ya kilimo ndiyo inayochangia kutengeneza ajira nyingi kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango hii imewekwa sasa tuende tukatekeleze, Dkt. Samia Suluhu Hassan ana kiu ya kubadilisha kilimo kutoka kilimo cha kutegemea mvua mpaka twende kwenye kilimo cha uhakika cha umwagiliaji. Mungu ametujalia mito, mabonde, Mungu ametujalia ardhi yenye

rutuba, sasa mipango yetu tuende tuka-*implement* tubadilishe hali ya kiuchumi ya Watanzania kupitia sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia mpango umezungumzia 70% ni kuwekeza kwenye sekta binafsi, hapa pia unagusa kwenye *economic zone*. Nilikuwa ninapitia taarifa mbalimbali za kwenye Wizara ya Viwanda, leo hii maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji ni hekta 59,000 kwa ajili ya *economic zone*, hiyo ni pamoja na kwenye Wizara, taasisi, hii pia ni pamoja na Halmashauri na pamoja na *TIC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye *TIC* peke yake, kwenye *special economic zone* hekta zilizotengwa 17,000 lakini imetumika asilimia moja tu, hekta 1,600. Ukiangalia hayo maeneo yaliyotumika, ukienda kule Kwala, Bagamoyo, Nala, Benjamini Mkapa, *impact* yake ya kiuchumi ni kubwa. Sasa tumelipa watu maeneo makubwa, lakini bado hatujaamua kwenda kuwekeza kwenye viwanda, hii yote inaenda sambamba na ujenzi wa vyuo kila Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sasa tunajenga vyuo kila Wilaya, tuna eneo kubwa la uwekezaji bado hatujalitumia, wananchi wamepisha maeneo, tunazungumzia kukuza uchumi wa Taifa letu, lakini haya maeneo lazima tukayawekeze, hizi ni hekari nyingi sana na nchi hii haijawa na uchache wa kuwa-*convince* wawekezaji waje wawekeze kwenye nchi yetu. Kinachohitajika wawekezaji wa ndani pamoja na nje ya nchi ni kuhakikishiwa mazingira mazuri ya uwekezaji. Wanahitaji kuona sheria zetu, *bylaws* zetu kwenye halmashauri ni rafiki, vilevile Mheshimiwa Waziri tunahitaji kubadili *mentality* ya watu, siyo kila mwekezaji mwizi, tuone wawekezaji wanaokuja nchini ni chachu ya kuchangia mabadiliko ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tubadilishe vilevile hali ya watendaji wetu kwenye maeneo yetu na huu mpango huu asilimia kubwa unakwenda kutekelezwa na TAMISEMI, *mindset* za Wakurugenzi wetu zipoje? Kazi yake pale ni kukimbizana na ujenzi na ukarabati wa madarasa na vyoo au Mkurugenzi ndiyo *CEO* wa kusimamia mabadiliko ya kiuchumi kwenye eneo husika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote yanapaswa kwenda sambamba katika kuhakikisha mpango huu unatekelezwa kikamilifu na Waziri amesema hatujawahi kuwa na tatizo la maarifa na kupanga mipango mbalimbali. Sasa Serikali ya Awamu ya Sita inataka kutekeleza kwa vitendo. Twendeni tukaongee na Watendaji kwenye maeneo mbalimbali waone hii dhamira ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ili maendeleo chanya na huu mpango uweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Saashisha alizungumzia jambo moja la kujenga miradi mbalimbali, tunajenga miundombinu mbalimbali, tunajenga madarasa, tunajenga shule, hivi hata siku moja tumeshawahi kufikiria kuwa na fungu maalum kwa ajili ya ukarabati? Hivi tunavyozungumza ni Bunge hili tulianzisha Mfuko wa Maji leo unafanya kazi kubwa sana, ni Bunge hili hili tulianzisha Mfuko wa Barabara, leo unafanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu fikiria ziwe shule maalum za wasichana zinazojengwa kwa zaidi ya bilioni nne kama hakuna pesa kwa ajili ya *maintenance* ndani ya miaka kumi zitakuwa kwenye hali gani? Mimi Jimboni kwangu nimefanya utafiti, kwenye shule za *primary* na shule za sekondari ambazo zimechakaa zinahitaji bilioni 1.6, *imagine* nchi nzima kwenye miundombinu tunayojenga nchi nzima, kwenye shule zetu tunazojenga nchi nzima, kwenye hospitali tunazozijenga zinagharimu kiasi gani? Tunajenga sana. Sasa kama Taifa ni jukumu letu kutenga pesa kwa ajili ya kulinda miundombinu yetu, kwa ajili ya kulinda shule zetu, kwa ajili ya kulinda hospitali zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninashukuru. Nilimtaja Mheshimiwa Masanja Kungu Kadogosa.

**MHE. MASANJA K. KADOGOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kushukuru kwa fursa hii, vilevile ninamshukuru Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maono haya ambayo

tunayazungumza kwa sababu mpango maana yake sasa tunawekwa katika namba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana vilevile Waheshimiwa Mawaziri, Waziri wa Fedha, Waziri wetu wa Mipango na Uwekezaji Profesa kwa wasilisho zuri sana na la kitaalam lakini kubwa mawazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Taifa ni vizuri tukajipongeza pamoja na kwamba tunayo safari ya kwenda. Nilikuwa ninasoma kitabu cha Mheshimiwa Benjamini Mkapa Marehemu (*My Life My Purpose*). Kufikiri kuanza kuwa na dira ya Taifa ilianza mwaka anazungumzia mwaka 1995, ndiyo mawazo yalianza hapo pamoja na kwamba ilichukua muda kidogo kabla hatujawa na mipango ya miaka mitano mitano, lakini tulianzia huko na wakati huo bajeti yetu, siyo bajeti kwa maana ya makusanyo yetu kwa wakati huo tunazungumzia takribani kama bilioni *334na point* kadhaa. Huko ndiyo tulikoanzia na mpaka Mheshimiwa Mkapa anatoka alikua kwenye trilioni *two point something,* lakini sasa hivi tunazungumzia makusanyo kwa taarifa tulizopata hizo tulifikia *above 34 trillion*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tulikotoka ni mbali sana. Kwa hiyo, ni vizuri sana kama Taifa tukawa *proud* kwamba kuna kazi kubwa sana imefanyika na mpaka hapa tulipofika na tunajenga sasa *base* kuanzia hapa kwenda mbele na ndiyo maana tunakuwa na jeuri ya kusema sasa tunauendea uchumi wa dola trilioni moja ni kwa sababu kuna *bases* ambazo zimetangulia na watangulizi wetu, wazee wetu wamefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukianza na Baba wa Taifa kwa maana ya ujenzi wa Taifa moja, hii imetupa *base* nzuri sana ya kuzungumza haya makubwa tunayoyazungumza, ukija 'Mzee Ruksa' amefanya kazi kubwa sana ya kufungua uchumi kwa maana ya kwamba tuwe na uchumi ambao unakaribisha na *private sector*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mzee Benjamin Mkapa na pengine jambo moja ambalo ni la muhimu sana, *TRA* mnayoiona hii wazo lilianzia kwa 'Mzee Ruksa' alipounda *President Commission* na baadaye Mzee Mkapa alipokuja akai-*pick up then* tukawa na *TRA*. Wakati wa Mheshimiwa Benjamin Mkapa kuna *institutions* nyingi sana zilitengenezwa kwa ajili ya ujenzi wa uchumi. Ukizungumzia *TANROADS* sijui *TRA* na hizi *institutions* nyingi ambazo tupo *proud* sasa hivi kama *regulators* zimetengenezwa wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile hata *BOT Act* kwa sababu kwa historia ni kwamba hata ukizungumzia kwa mfano *monetary policy* ilikuwa *part* ya *department* ndani ya Wizara ya Fedha, mambo ya *pension* lakini *then* zikatengeneza *institution*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninachosema ni nini? Kwamba kama Taifa tumetoka mbali na kuna mambo ambayo yamefanywa ya msingi kuanzia wakati ule, ukianzia kwa Mzee Mkapa kama nilivyosema, kwa Mzee Jakaya Mrisho Kikwete, tumejenga shule za Kata nchi nzima, jambo kubwa sana kwa Taifa. Tumejenga *UDOM*, tumejenga diplomasia wakati huo ilipanda sana upande wa diplomasia. Tulikuwa na Marais watatu kwa wakati mmoja, Rais wa Marekani ambaye yupo madarakani, Msaidizi wake ambaye alimtangulia na Rais wa China alikuja hapa ku-*launch* mipango ya Afrika, kwa maana ya Afrika na China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni nini hapa? Kuna mambo makubwa ambayo yamefanyika kama Taifa ni lazima tuwe *proud* na ndiyo maana sasa hivi tunaweza tukazungumzia mambo makubwa. Nimezungumzia Jakaya Mrisho Kikwete, lakini amekuja Magufuli amefanya mambo makubwa sana, tumeanza *SGR*, tumeanza ujenzi wa Bwawa la Nyerere, tumehamia hapa Dodoma, hivi vitu vyote kama Taifa inatufanya tujiamini tunakokwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kenned alikuwa anazungumzia kuhusu ukomavu wa Taifa, upevu wa Taifa unapima uwezo wa kufikiri, ku-*design* na kusimamia mipango

mikubwa katika Taifa, hilo tumeweza kulifanya na ndiyo maana kama Taifa sasa tunaweza tukasema tunasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya mambo makubwa, ukiacha mambo ya kuendeleza *SGR* alivyoikuta, mambo ya madaraja makubwa tuliyokuwa tunajenga vilevile Bwawa la Mwalimu Nyerere lakini na mambo mengine mapya ambayo ameanzisha, kama vile tunatoka Dodoma tunaenda Mwanza kwenye *SGR*, tunatoka Dodoma tunaenda Kigoma, tunatoka Dodoma tunaenda Burundi. Haya ni maamuzi makubwa sana kwa kiongozi, yanahitaji uzalendo na yanahitaji uthubutu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo, kwa sababu ninataka tuanze kwanza kwa kujipongeza na kujua kwamba kuna kazi kubwa sana imefanyika katika Taifa hili, kuna baadhi ya watu wanaweza wakazungumzia katika akili yao inavyowatuma, lakini Taifa hili tumefanya mambo makubwa sana na tuna uwezo sasa wa kufikiri mambo makubwa ya kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nizungumzie mambo matatu ambayo hasa katika mchango huu, kwa maana ya mpango wetu kwa mwaka mmoja, miaka mitano na miaka 25. Vilevile kabla sijaanza hapa tulianza na kuzungumzia hotuba ya Mheshimiwa Rais. Kwa hiyo, nini maana yake? Maana yake ni kwamba tunapoanza kuzungumzia mpango ni muhimu ika-*reflect consistency* ya kile Rais alichokizungumza. Kwa hiyo, tunategemea kwamba mipango yote izungumze na hotuba ya Rais, kwa hiyo, *consistency* izungumze kila mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sehemu moja ambayo ninafikiri Profesa inabidi wakaliangalie. Kwa mfano, mpango wa muda mrefu wa miaka 25, tunazungumzia *target* yaku-*archive inter-model,* lakini hotuba ya Rais inazungumzia *multi-model transport system*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi vitu viwili ni tofauti. *Multi-model transport system* katika *logistics* ndiyo *system* ya hali ya juu ambayo nchi inatakiwa kwenda huko. Kwa maana nyingine ni

kwamba lazima kuwe na *consistency* kwa sababu haya ni makabrasha ambayo yanaishi, inawezekana watekelezaji wa sasa hivi wasiwe watekelezaji baada ya miaka mitano wakaja watu wengine. Kwa hiyo ni lazima tuweke mambo yetu vizuri tuwe na *consistency*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumzia ukurasa wa 145-149. huku tunazungumzia *inter-model* unapo-*refer inter-model, what's the difference between the inter-model* na *multi-model?* Hii inazungumzia kufungamanisha kwa maana kuna *modes* mbalimbali, unafungamanisha vipi? Maana yake unakuwa na *contract* moja. Kwa wale wa zamani kidogo hapa na mimi nimeshakuwa muhenga kidogo. Zamani mlikuwa mnatoka kutoka Bukoba mnakuwa na tiketi moja unapanda meli, unakuja kwenye reli unatumia tiketi hiyo hiyo, unashuka pale Itigi, unatumia tiketi hiyo hiyo kwenda huko Kyela kwenye mabasi. Sasa hiyo *at least* ina-*come a little bit closer, but it is not real reflection* ya *multi-model.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninachosema ni nini? Hizi *document* lazima zizungumze, *try to speak to each other*, kuwe na *consistency,* lakini kuna wakati mwingine kuweka *timeline*, unasema unataka kufanya *transformation* ya *mindset* ambayo ni jambo kubwa sana katika nchi, kama tutaenda katika mambo haya ya kubadilisha mtazamo wetu, ni wakati gani unataka tukamilishe? Unapoweka 2050 wakati ni kitu muhimu tunapoanza utekelezaji *then* kunakuwa kidogo na mushkeli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninataka kuzungumzia namba zinasema nini? Namba zinazungumza na bahati nzuri katika ripoti ukianzia Profesa amezungumza vizuri sana, kwamba mpango wetu tuta-*fund* kwa trilioni 477 na *70%* ya hiyo *comes from private sector* na *only 30%,* now ukirudi mpango ulioisha tulikuwa na trilioni 114, trilioni 40 zilikuwa zinatoka kwenye *private sector* na *the rest* zilikuwa zinatoka kwenye public, maana yake kuna *shift*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa Profesa amezungumza vizuri sana, tunahitaji *shift* kubwa ya sera*,* sheria na kanuni ndani

ya Serikali, sasa *to what extent? Is it 70%, 60%, 50%* shift? Sasa hilo ni suala la kuangalia katika utekelezaji. Kwa hiyo, ninafikiri nizungumzie katika hilo na ninampongeza sana Profesa kwa kuliona hilo kwa sababu *it takes guts*, unajua mtu mwingine unapozungumza *private sector, now has to drive*, mwingine anaweza akaja na *scenario* ya kusema, sasa tunataka kuachana na ujamaa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujamaa haina maana ya umaskini! Watu kwa mfano wa China, ninafikiri Rais wa China wakati huo alikuja na *slogan* ya kusema kama *cat* eeh? *I don't care*, *it doesn't matter* kama *cat is black or white so long* as anaweza kukamata panya! *That was a shift* katika *policy* za Kichina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ni la mwisho, mipango hii inahitaji pesa, sasa ni lazima tuwe *innovative*. Tunapozungumzia *private sector* kuwa *part* ya ku-*fund* mipango yetu ya miaka mitano 70%, tunazungumza *PPP*. Maana yake ni nini? Ni lazima kuwe kuna *total change ya the way* tunavyoangalia *funding organisation* kwa mfano Wizara ya Fedha, yawezekana *structure* uliyonayo inatakiwa ibadilike. *May be the biggest department now* tunapozungumzia Wizara ya Fedha inaweza ikawa ni bajeti lakini kwa ujio huu yawezekana tukawa na *total change* ya namna ambayo tunavyo-*organize* katika *funding*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la ku-*fund* pengine kwa kutumia *future asset*, tuseme labda madini. Tunafanyaje kuona kwamba haya madini tuna-*leverage*…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha.

**MHE. MASANJA K. KADOGOSA:** *Okay*, Mheshimiwa Mwenyekiti ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Pius Zebhe Yanda atajiandaa, Mheshimiwa Jafari Wambura Chege.

**MHE. PIUS Z. YANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia na ninashukuru kwa sababu niliomba nitoe mchango kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais lakini sikupata nafasi. Awali ya yote ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kuwa Rais kwa kipindi kingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo iko wazi kwamba ni kwa sababu aliweza kupata kura za kumwaga na ninaomba niweze kutoa taarifa kwamba katika Jimbo letu la Buhigwe, alipata kura 98%. Kwa hali hiyo naomba basi pia niweze kumshukuru yeye kama Mwenyekiti wa Chama Taifa, kwa kuweza kuteua jina langu ili niweze kupeperusha bendera ya Chama Cha Mapinduzi na wananchi wakaweza kunipigia kura za kutosha. Kwa hiyo, ninawashukuru pia Wanabuhigwe kwa kuniamini na kunipa kura za kutosha na ninawahakikishia ya kwamba nitawatendea haki katika kuwasilisha yale yanayowahusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme tu kwamba hizo kura nyingi zilizopatikana zilitokana na kazi kubwa ya Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuwezesha miradi mbalimbali katika Jimbo la Buhigwe; tukizingatia kwamba Wilaya ya Buhigwe ni changa ikiwa na umri wa miaka 12, lakini tunavyoongea sasa hivi tumepata hospitali ya wilaya yenye vifaa vyote vya kiwango cha juu, tumeweza kupata barabara inayounganisha Mnanira na Kasulu ambayo ni *link* moja muhimu sana. Pia tumewezeshwa vituo vya afya, zahanati, shule za sekondari na shule za misingi ikiwemo shule ya watoto wa kike, ambayo ni *boarding* na iko *dedicated* kwa ajili ya wasichana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, hayo yaliwafurahisha Wanabuhigwe wakaona kwa kweli wana kila sababu ya kutoa shukrani. Sasa baada ya kusema hayo naomba sasa niweze kuchangia kwenye hoja iliyoko mbele yetu, nikianza kwanza kuwapongeza Mawaziri waliowasilisha hiyo hoja, tukianza na Profesa Kitila Mkumbo ambaye ni Waziri wa Uwekezaji, lakini pia na Mheshimiwa Balozi Hamis Mussa Omar ambaye pia ni Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema tu kwamba, ninaweza nika-*confirm* tu kwamba, hiyo mipango mitatu ya mwaka wa muda mrefu, mwaka wa muda wa kati na mwaka wa muda mfupi, imeweza *ku-reflect* yale yaliyoko kwenye dira lakini pia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais. Nianze na sekta ya kilimo, ningependa kunukuu kwenye hotuba ya Mheshimiwa Rais ukurasa wa 20 ambayo inasema kwamba: "*Katika miaka mitano ijayo tunaenda kufanya uwekezaji mkubwa kwenye sekta za uzalishaji tukianza na kilimo, tutaongozwa na dhana ya kilimo ni biashara, mkulima ni mwekezaji.*" Kwa kweli huo ni mwelekeo unaolenga kufanya mapinduzi makubwa sana katika sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara kadhaa tumekuwa tunawaangalia wakulima kama ni wakulima ambao wanalima kilimo cha kujikimu. Sasa ukishaanza na neno hilo maana yake ni kwamba ni wakulima ambao wanalima ili waweze kupata tu kile kiasi kidogo cha kuwezesha familia yake kuweza kuishi, lakini tukija na mtazamo huu maana yake ni kwamba sasa wanapewa fursa wakulima waweze kuonekana kama wawekezaji wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi tunahitaji kufanya hivyo, moja ni kubadilisha *mindset* mtu ajue kabisa ana fursa ya kuweza kufanya shughuli zake za kilimo kama mwekezaji na sio mkulima wa kutafuta chakula cha kuweza kutumia ndani ya familia. La pili ni kwamba, tuangalie sasa mazingira wezeshi ya hawa wakulima ambao tunataka sasa wabadilike wawe ndio wawekezaji kama wawekezaji wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni kwamba, inabidi tuweze kufanya maandalizi ya wao kuweza kupata mikopo au mtaji katika mazingira rafiki. La pili, masuala ya miundombinu, kuna baadhi ya maeneo huko tunakotoka nikirejea Jimbo langu la Buhigwe; wakati wa masika kuna maeneo huwezi kufika na ninaomba nitoe ushuhuda tu kwamba mara kadhaa nimeenda nyumbani, nimeshindwa kufika kijijini kwangu. Sasa kama tunaweza tukaboresha miundombinu ambayo inaunganisha vijiji na maeneo mengine hasa kwenye maeneo ya masoko, basi

maana yake ni kwamba watakuwa na uhakika wa kuweza kupata maeneo ya kuweza kuuza bidhaa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika nikirejea Jimbo langu la Buhigwe ni jimbo ambalo ni wakulima wazuri wa matunda, nanasi, ndizi kwa wingi sana. Sasa kama tungeweza tukatengeneza mazingira ambayo wawekezaji wakaanza kuwekeza kwenye *agro-processing industries* maana yake ni kwamba thamani ya yale mazao yanayozalishwa basi yataweza kupata pesa kubwa zaidi na wananchi watahamasika kuendelea kulima kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirejee mfano mwingine, Kata ya Munzezi na vijiji jirani wanalima tangawizi kwa kiasi kikubwa sana, lakini sasa wanauza kwa bei ya chini kwa sababu hawajaweza kuwezeshwa kuweza kupata uwekezaji wa kuweza kuchakata ile tangawizi ili kwamba waweze kupata faida katika kilimo chao. Tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati wa ziara ya kampeni, aliahidi kiwanda cha kuchakata tangawizi katika Kata ya Munzeze na ninaomba sasa Wizara husika iweze kulichukulia hilo jambo *seriously* ili kwamba wananchi waweze kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tunapozungumzia barabara maana yake ni kwamba ni barabara zinazowezesha wafanyabiashara kuchukua mazao sehemu moja kupeleka sehemu nyingine hasa kwenye masoko. Kuna barabara moja ya msingi ambayo inatoka hayo maeneo ninayoyazungumzia ambayo wanalima tangawizi ambayo inakuja mpaka Buhigwe Mjini, inaenda mpaka Mwiyama na kuelekea huku kuungana na *SGR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni barabara ambayo ni kilio cha wananchi wa Buhigwe walio wengi, vijiji vingi. Bahati nzuri pia wakati wa ziara Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliahidi barabara hiyo iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Hii ilikuwa ni kuona kwamba anajaribu kutekeleza ile ndoto yake ya kuhakikisha kwamba sasa wakulima wa sasa hivi, waweze kuwa

*transformed* kuwa wafanyabiashara wawekezaji kama wawekezaji wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa mtazamo huu nataka nirejeshe suala la vijana kuwashirikisha kwenye kilimo. Ninafikiri hii ni fursa pekee ambayo tunaweza tukawashirikisha kwenye kilimo na hiyo itapunguza pia kasi ya vijana kutoka vijijini kwenda mjini. Changamoto moja ambayo ninaiona na ninafikiri hilo ni jambo ambalo ninaliweka hapa kwenye kikao hiki tukufu kwamba, tuanze kufikiria kwa kina, tuanze kutenda kitu kinaitwa *Land Bank* kama ambavyo kwenye ngazi ya kitaifa kuna *Land bank* kwa ajili ya wawekezaji wa nje basi tuwe na *Land bank* kwa ajili ya vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kila mwaka kuna idadi kubwa ya vijana *wana-graduate* kutoka sekondari, kutoka vyuo vikuu wanarudi vijijini je, hicho kilimo tunachozungumzia wataenda kulima wapi? Sasa hilo ni suala ambalo tunaweza tukaliangalia linaweza *either* likafanyika kwenye ngazi ya wilaya au mkoa, au Taifa lakini ni jambo la msingi sana. Kwa sababu *otherwise* itafika mahali na tukiangalia idadi ya watu inavyozidi kuongezeka maana yake ni kwamba wanaweza wakajikuta hawana maeneo hata kama tutawahamasisha kwamba waweze kuwa na kiu ya kuingia kwenye shughuli za kilimo, lakini maeneo yanaweza yasipatikane…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako, muda wako umeisha.

**MHE. PIUS Z. YANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimuita mchangiaji wetu wa mwisho kwa asubuhi ya leo, Mheshimiwa Jafari Wambura Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kutoka kwa

Waziri Profesa Mkumbo, lakini pia nipate nafasi ya kuchangia mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya bajeti kutoka kwa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kusema ninaunga mkono hoja zote mbili na ninakubaliana na maono yao mazuri yaliyopo kwenye taarifa zao zote mbili kwa Mawaziri hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuridhia na kukubali kuanzishwa mchakato wa Dira mpya ya Taifa ya mwaka 2050. Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa mambo makuu matatu. Moja kwa kutekeleza maono ya Dkt. Samia, maono ya Watanzania na mwelekeo wao na dhamira waliyokuwa nayo juu ya kupatikana kwa dira mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri kwa kuandaa mpango elekezi na dira yenyewe, kiukweli amefanya kazi kubwa nzuri kama ambavyo tunatambua changamoto ya Dira ya mwaka 2025 ilikwenda kwa kusuasua kwa sababu ya kukosekana kwa mpango elekezi wenyewe ya namna dira inavyokwenda kutekelezwa. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa hilo. La pili, nimpongeze pia kwenye taarifa yake kwa kutambua umuhimu wa wawekezaji hasa wazawa na kurudi kuangalia namna ambavyo Serikali inapaswa kushirikiana na *private sectors* bila kuwaacha wazawa katika kuinua uchumi wetu kama watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili Mheshimiwa Waziri aende alitazame upya pamoja na kwamba wazawa wanaruhusiwa kufanya kutekeleza miradi iliyo chini ya bilioni 50, ninashauri Serikali ipanue wigo iende zaidi ya bilioni 100 mpaka bilioni 200 kwa sababu ninaamini tunao wazawa ambao wana uwezo mkubwa wa kufanya haya. Tatu, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwenye taarifa yake na ndiyo jambo muhimu sana la kuanza la kupendekeza walau Wakurugenzi wa Halmashauri kupata nafasi kulingana na uwezo wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu nimeona kwenye Kamati pia wamekwenda mbali wameshauri Wakurugenzi wa Taasisi mbalimbali na Mashirika ya Umma nao waende watazamwe katika nyanda hiyo, wateuliwe kulingana na nafasi zao ili tuweze kuwapima kulingana na ukuaji wa taasisi zao na utendaji wao wa moja kwa moja. Kwa hiyo, kwa kweli nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa taarifa hii. Nina maoni kadhaa kwa malengo mahususi katika dira. Yapo malengo mahususi manne, lakini nitajikita leo kwenye lengo moja tu la maisha bora na ustawi wake kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza dhana ya maisha bora, kama taifa linaloendelea tunatambua yapo maeneo kadhaa ambayo Serikali kwa ujumla wake inapaswa kujikita ili kuinua uchumi wa wananchi kwa ujumla wake. Wizara hii imeonesha mwelekeo na njia ya kupita, ni kazi sasa ya wizara za kisekta kuchukua maono ya wizara hii ya mipango na uwekezaji, kuyachakata na kuyaingiza kwenye mipango ya wizara za kisekta ili yaende yakashamiri na yasambae kwa wananchi kwenye maeneo yote kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maeneo hayo nilitaka nijikite kwenye maeneo kadhaa. Mfano, tunapozungumzia maisha bora ni lazima uzungumze maisha bora kwa wananchi kwa kutazama miundombinu ya barabara inayozunguka wananchi wale. Katika miundombinu ya barabara lazima tuiangalie kwa nafasi mbili tofauti. Lazima tuangalie barabara zinazosimamiwa na *TANROADS,* lazima tuangalie barabara zinazosimamiwa na *TARURA* katika kutekeleza na kupunguza minong'ono na kuimarisha Maisha bora kwa ustawi wa wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakubaliana na mimi, kuna baadhi ya meneo mengi sasa barabara imekuwa ni changamoto kubwa sana na Waheshimiwa Wabunge wamesema hapa, zipo barabara ambazo zimetangazwa, wakandarasi wapo *site*, wanatekeleza, zipo barabara ambazo zimesaini mikataba, wakandarasi hawajaingia *site* na zipo barabara ambazo zipo kwenye *procurement process* kwenye maeneo mbalimbali.

Lazima tukubaliane kwa kuwa Wizara ya Fedha imesema hapa imetoa mwelekeo wake wa uandaaji wa bajeti, watenge fedha ya namna ya ukamilishaji wa barabara hizi kwenye maeneo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko barabara ambazo tunazungumzia maisha bora kwa wananchi zimetajwa kwa awamu nne, tano kwenye maeneo tofauti toka miaka ya 95 zinatajwa barabara zile, mpaka sasa tuko mwaka 2025 tunakwenda 2030. Mfano wa Barabara yangu ya Utegi - Shirati kwenda Kirongwe ni matarajio yangu sasa Mheshimiwa Waziri, Wizara ya Fedha itatenga fedha kusaidia Wizara ya Ujenzi ili kuimarisha maisha bora kwenye maeneo yale, ili barabara zile ziweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara inapokamilika ndiyo inakwenda kuinua uchumi wa eneo husika kwa sababu kuna barabara zinaunganisha kati ya mkoa na mkoa, wilaya na wilaya na zingine zinaunganisha nchi na nchi. Kwa hiyo, katika kuimarisha na kutengeneza maisha bora lazima uweke fedha ya kukamilika kwa barabara ile ili wananchi waweze kupita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni utekelezaji wa miradi ya maji nchini. Niombe sana Wizara husika ya sekta ya maji, ifanye tathmini ijiridhishe badala ya kuwa na tathmini ya namna tumetatua maji kwa asilimia ngapi iangalie upatikanaji wa maji kwenye maeneo yale. Yako maeneo ambayo yana miundombinu ya maji, tunayahesabu kama asilimia katika kutekeleza mpango kazi wa maji, lakini maji hayatoki kwenye maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wito wangu ni nini, Wizara ya Maji, kwanza ihakikishe miradi ya maji iliyoanzishwa inakamilika, inakwenda, inafika mwisho na inatoa maji. Mbili, wafanye tathmini kwenye miradi ambayo tayari walipeleka miundombinu badala ya kuihesabu kwenye asilimia ya utekelezaji wa maji wajiridhishe kama miradi hiyo kweli inatoa maji na wananchi wananufaika kwenye yale maeneo. Wakifanya hivyo, maana yake watakuwa wanakwenda kwenye ile itifaki ya maisha bora na ustawi wa wananchi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni sekta ya ardhi, hili eneo tumekuwa tukilisahau sana. Kipanga, kupima na kumilikisha tumezungumza kwa mda mrefu sana. Niombe Waziri wa Sekta kwenye awamu hii ya bajeti inayokuja, hili jambo liende lipewe msukumo mkubwa kwa sababu ardhi isiyopangwa na kupimwa kwani ndiyo chanzo cha migogoro ya ardhi kwenye maeneo yetu, maana yake kunakuwa hakuna amani kwenye maeneo yetu. Ardhi yetu inakosa thamani halisi pale inapokuwa haijapangwa, kupimwa na kumilikishwa kwenye maeneo yao. Niombe sana Mheshimiwa Waziri husika, aende alione hili tunapokwenda kuchakata bajeti yake ili waweze kulipa nguvu ili waweze kupata ustawi ulio mzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa hapa jambo la soko la vijana, ajira kwa vijana na nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuanzisha Wizara husika ya Vijana, lakini ningeomba sana Waziri husika pamoja na michakato mbalimbali inayoendelea kwenye Wizara hii, lazima waende wakawa-*group* vijana, tujue hawa vijana wanaowazungumzia ni kuanzia umri upi mpaka umri gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende pia tukazungumze fursa sawa kwa hawa vijana kwa kutazama mazingira ya vijana wanayotoka. Kijana wa Rorya mazingira yake kwenye fursa hayawezi kuwa sana na kijana anayeishi Dar es Salaam. Kwa hiyo, Wizara iende ikajikite itazame kama inakwenda kusaidia vijana, isaidie vijana kulingana na mazingira ya maeneo yao wanayotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, itazame fursa za kimaeneo hayo wanayotoka hao vijana. Tusizungumze *general* moja kwa moja kwa kuwa-*generalize* vijana wote kama vile ni sawa kutokana na fursa wanakotoka. Kijana wa Rorya inawezekana fursa yake isiwe sawa na kijana wa Tandahimba, haiwezi kuwa sawa na kijana wa Kinondoni. Kwa hiyo, ni lazima Mheshimiwa Waziri, aende alione hili namna ambavyo anaweza akaliweka ili litengeneze ustawi ulio mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwenye mpango, ni kuhusiana na kilimo. Sisi tunazungumza Mkoa wa Mara, leo hii hatuna zao kuu la kibiashara tunalojivunia, tunazo *skim* mbalimbali za umwagiliaji pamoja na kuzunguka Ziwa Victoria zaidi ya 70%, hatuna *skim* kubwa ya kuzungumza leo kama kielelezo cha ukuaji wa kilimo kwenye Mkoa wa Mara. Tunatamani Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na mpango huu umekwishaonesha ili waende wakatengeneze upembuzi yakinifu kwenye maeneo yale na sisi tunatamani kupitia mkoa ule tuwe tuna *skim* ambazo zinawainua wananchi kwenye uchumi na zinaleta manufaa kwenye Wizara hii na kwenye sekta ya kilimo kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri alitazame hili. Mfano, mimi Rorya nimezungukwa na maji 77% lakini ninavyozungumza na wewe hatuna *skim* yoyote tunayojivunia pamoja na kuzungukwa na maji 77%. Tazama katika 100%, ni 23% peke yake nchi kavu, lakini sina *skim* yoyote ya umwagiliaji. Kwa hiyo, nikatamani pamoja na kusema, wenzangu wameshauri hapa kuwe na timu ya *monitoring and evaluation* lakini Wizara ione namna bora ya kusaidia maeneo haya ili waweze kuwasaidia kwenye kilimo, badala ya kubaki na kuzungumza kilimo kwa ujumla wake, lakini maeneo ambayo yana fursa hayanufaiki na kilimo hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ningetamani nizungumzie juu ya uchumi wa kimaeneo na Mheshimiwa Waziri amelizungumza sana hapa kwamba, pamoja na kwamba tunakwenda kuunda timu ya *monitoring and evaluation* lazima tuangalie maeneo hasa ya kimkoa namna yalivyokaa, ni fursa zipi za kiuchumi ambazo zinaweza zikaanzishwa zikawanufaisha mikoa husika. Mkoa wa Mara hatuna mradi mkubwa kama kielelezo kinavyozungumza, hatuna mradi wa *skim* ya umwagiliaji lakini viwanda tulivyokuwanavyo vyote vimekufa. Matarajio yetu ni nini kutoka kwa Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, Serikali ione namna ambavyo kama fursa yetu ni kufufua viwanda vilivyokuwepo vikiwemo viwanda vya nguo, kiwanda cha maziwa na fursa zingine ambazo zinaweza zikainua uchumi wa maeneo yale.

Ningetamani sana nione Wizara hii na Serikali ikiona namna ya kuweka fedha kuinua mkoa ule. Kwa sababu, ukifanya hivyo kwanza unainua ajira kwa wale vijana, lakini pia watatengeneza uchumi wa mkoa wenyewe husika, kuliko namna inavyokwenda kwa ujumla wake na sisi kama mkoa tunabaki tukiwa bado hatujapata kitu ambacho tunaweza tukasema tunajivunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na ninasema tena kwa mara nyingine kwamba, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:** Bunge linarudia.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Waheshimiwa tumefika mwisho wa shughuli zetu za asubuhi ya leo. Ninaomba niwataje watakaoendelea jioni; atakuwa Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando na Mheshimiwa Boniventura Desdery Kiswaga, atajiandaa.

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo hapa kutoka kwa Katibu wa Bunge. Anaomba tuwatangazie Waheshimiwa Wabunge wote kutakuwa na uchaguzi wa viongozi wa *Bunge Sports Club* utakaofanyika siku ya Ijumaa, tarehe 6 Februari, 2026 katika ukumbi wa Msekwa saa 7.30 mchana. Uchaguzi huo utahusisha viongozi wafuatao:-

Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, Makamu Mwenyekiti, Meneja, Wajumbe watano wa Kamati ya utendaji ya *Bunge Sports Club*, angalau wanawake wawe wawili. Fomu za kugombea zinaanza kutolewa leo tarehe 3 Februari, 2026 katika Ofisi ya Katibu wa Bunge na zitarejeshwa tarehe 5 Februari, 2026 saa 10.00 jioni.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba kusitisha Shughuli za Bunge hadi saa 11. 00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11. 00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Mipango.

**MWENYEKITI:** Kamati ya Mipango.

**KAMATI YA MIPANGO**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda mrefu 2026/2027 - 2050/2051, Mapendekezo ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2026/2027 – 2030/2031) na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2026/2027**
**na**
**Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali katika Muda wa Kati ya Mwaka 2026/2027 - 2028/2029**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Alishaitwa Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Clayton Revocatus Chipando na Mheshimiwa Boniventura Kiswaga wajiandae.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kupata nafasi niweze kujadili mpango huu wa maendeleo ulioletwa mbele yetu. Kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini nikishukuru Chama changu Cha Mapinduzi na wananchi wangu wa Wilaya ya Chunya na Jimbo la Lupa kwa kuweza kunichagua na kunirudisha tena niweze kuwawakilisha. Ninawaambia kwamba tunaendelea pale tulipoishia kuhakikisha kwamba mipango ya Serikali inakwenda vizuri na wao wanaendelea kupata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa mpango huu mzuri ambao ametuletea hapa mezani, mpango ambao umesheheni vizuri. Hakika tunaona kwamba *PhD* yake inafanya kazi vizuri, yeye pamoja na wasaidizi wake, lakini pia na Waziri wa Fedha. Hakika tupo sehemu salama zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyofahamu mpango huu ni mpango ambao unaenda kuakisi yale ambayo mipango ya Serikali kwa miaka mitano lakini kwa miaka 50 inayokuja. Hata hivyo, kwenye mipango hii ambayo inaendelea imeweza kueleza mambo kadha wa kadha, imeweza kugusa vizuri kila sekta na wananchi huko nje kila mmoja ameweza kuisifia hii hotuba. Jambo kubwa ambalo liko mbele yetu waweze kuona matokeo ya hii mipango ambayo imeelezwa kwenye hii hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona namna ambavyo ukitaka kuhakikisha kwamba uchumi unaendelea kuwa vizuri zaidi na kwenye mpango imeeleza namna ambavyo kwenda kuiwezesha sekta binafsi. Sekta binafsi ukuaji wake ambao tunategemea kwamba, zaidi ya 70% tunaweza kupata mapato kutoka kwenye sekta binafsi hasa kwenye upande wa ajira, lakini kwenye upande wa kodi na mambo mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kwenda vizuri zaidi lazima mazingira mazuri hasa kwenye sekta binafsi yatengenezwe. Tumeona kwenye mipango ya Serikali namna ambavyo kwenye upande wa nishati leo tuna uhakika wa kuwa na umeme wa kutosha, tuna Bwawa la Mwalimu Nyerere na tunazo megawati za

ziada. Je, hizi megawati ambazo tunasema tunazo za ziada huko chini kwa wananchi wetu wanaufurahia huu umeme? Huko chini kwenye viwanda vyetu wanaufurahia huo umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nishauri kwenye upande huu. Lazima tuwekeze nguvu kubwa kwenye usafirishaji wa huu umeme kwa maana miundombinu tuliyokuwa nayo ilikuwa ni ya zamani ambayo sasa imechakaa, pamoja na kwenye usambazaji wa huu umeme. Tukiweza kuwekeza kwenye usafirishaji na usambazaji tutaweza kuwafikia watu wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali, juzi tarehe 17 Januari, tumeona kwenye usambazaji tumeweza kusaini kwenye vijiji zaidi ya 9,000 na mimi kwa Wilaya yangu ya Chunya tumepata zaidi ya vitongoji 31. Hii ni hatua kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe ili tuweze kwenda vizuri zaidi tuhakikishe kwamba njia ya usafirishaji inakwenda vizuri. Mathalani leo kwenye Wilaya yangu ya Chunya, tuna umeme umesambaa kwenye vijiji vyote, lakini umeme huu tunaoupata ni mdogo ambao haujitoshelezi na haujitoshelezi kwa sababu miundombinu imeshakuwa ni chakavu ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo nishauri namna ya kuweza kukabiliana na hii changamoto. Tuweze kujenga *substation* ya kutosha pale kwenye Wilaya yetu ya Chunya ili tuwe tuna umeme wa kutosha ambao utaweza kulisha viwanda vyetu, utaweza kulisha kwenye maeneo ya wachimbaji na wao waweze kunufaika na huu umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tu wachimbaji wengi wa kutosha wanashindwa kunufaika na huu umeme, kwa sababu ni mdogo matokeo yake wanatumia majenereta hivyo gharama za uendeshaji zinazidi kwenda juu zaidi. Hivyo nishauri kwenye hili, tukifanya hivyo tutaweza kuwafikia watu wengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, sisi watu wa Chunya maeneo mengi sana ni wachimbaji, tunapeleka umeme kwenye vitongoji, lakini maeneo ya wachimbaji kasi ya kupeleka umeme

ni ndogo sana. Niombe ili mpango huu uweze kwenda vizuri na uwaguse wananchi wengi, twende tuhakikishe tuwe na mpango mahususi wa kupeleka umeme maeneo ya wachimbaji, ili kuweza kwenda kule kuongeza uzalishaji ambapo pamoja na kwamba umeme ni huduma, lakini umeme pia ni biashara. Wataweza kununua kwa gharama, lakini pia tutapunguza uendeshaji kwenye migodi ya wachimbaji wetu wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema kwamba tunaenda kuwagusa hawa wachimbaji wetu, tunaona namna ambavyo Sekta ya Madini imezidi kuchechemuka. Leo hii kila mchimbaji wa madini anafurahia hasa kwenye uchimbaji wa madini ya dhahabu namna ambavyo mazingira ya uchimbaji yametengenezwa yamekuwa mazuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha mazingira ya uchimbaji kuwa mazuri zaidi, bei ya soko la dunia na soko la ndani kwa mara ya kwanza tumeweza kufikia kwa gramu moja zaidi ya shilingi 400,000. Haijawahi kutokea, lakini kwenye Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Mama Samia Suluhu Hassan kutokana na sera nzuri na mambo mazuri huko duniani leo tunaona namna ambavyo bei imekuwa nzuri na wachimbaji wetu wananufaika, hivyo tukiwekeza zaidi hapa, tutaweza kupata na kuwapata wachimbaji wakubwa zaidi. Ili tuweze kuwafikia wachimbaji wengi na wakubwa zaidi lazima tuwekeze kwenye utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tunaliimba jambo la utafiti kila siku. Wizara kupitia Mheshimiwa Waziri amekuwa anazungumza kwamba utafiti unafanyika, vifaa vinanunuliwa lakini pamoja na kwamba vifaa vinanunuliwa bado hatujaweza kuwafikia wachimbaji wengi. Tukifanya utafiti wa kina tukaupeleka maeneo hizi taarifa kwa wachimbaji wetu wadogo tutaweza kuongeza uzalishaji wa dhahabu, lakini tutaweza kuwainua wachimbaji wetu kutoka kuwa chini kwenda kuwa wa kati, uchumi wa nchi utaendelea kukua, lakini siyo kukua tu tutaendelea kuwatengeneza mabilionea wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kupitia Sekta ya Madini peke yake kwenye mchango wa pato la Taifa tunachangia zaidi ya

10%; siyo kiasi kidogo na tukiendelea hivi tutazidi zaidi ya 10%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe, Mheshimiwa Waziri yuko hapa na Naibu Waziri wa Madini yuko hapa; tuendelee kuweka nguvu kubwa sana kwenye Sekta ya Madini. Tukiwekeza nguvu kwenye Sekta ya Madini kwenye utafiti tuna uhakika tutapata fedha nyingi hasa fedha za kigeni na nchi yetu itazidi kwenda mbele na tutaweza kupiga hatua kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, tulikuwa tuna mpango wa kuweza kuwasaidia wachimbaji wadogo kupitia Mradi wa *MBT (Mining for Brighter Tomorrow)*. Mradi huu unazungumzwa, lakini utekelezaji wake bado haujaanza mpaka leo. Niombe tuweze kuwatengeneza vijana. Tumeunda Wizara ya Vijana; namna gani tutaweza kuwasaidia hawa kupitia *MBT* maeneo ya wachimbaji wadogo tutengeneze *rush*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule kwangu tuna baadhi ya maeneo ambayo tumeyaweka kama hifadhi kuna Hifadhi ya Mbiwe, kuna hifadhi ya kule Gepu kuna watu walitolewa kule. Tuone namna ambavyo kule Gepu tutengeneze tuwapatie leseni hata mbili au tatu kwa wachimbaji wadogo ambao tuwaweke kwenye mpango wa *MBT* ili wao waweze kuchimba pale. Hivi ndivyo tutakavyoweza kuwasaidia vijana na Wizara yako Mheshimiwa Nanauka itaonekana inafanya kazi vizuri na wananchi wetu wataweza kupiga hatua kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona pia kwenye upande wa Sekta ya Kilimo. Sekta ya Kilimo kazi kubwa imefanyika na zaidi ya 65% – 70% ya Watanzania tunategemea kilimo kuendesha maisha yetu ya kila siku, lakini na uchumi wetu kwa ujumla. Tumeona Serikali imeweka ruzuku ya kutosha leo wananchi wananufaika wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mbolea hii ambayo leo wananchi wananufaika, kule kwangu tuna wakulima wa mazao ya chakula na wakulima wa zao la tumbaku. Mpaka kwenye zao

la tumbaku tumeweza kuweka ruzuku na wananchi hawa wanaweza kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mazao ya chakula, wale mawakala ambao wanapata hii mbolea kwa ruzuku na bei elekezi, wanashindwa kwenda kuifikisha mbolea hii maeneo yote kwa sababu usafiri kutoka eneo moja kwenda eneo lingine gharama zinatofautiana. Leo wakala anachukua mbolea anaambiwa atauza mfuko kwa 75,000 kwa Wilaya ya Chunya, kutoka Mbeya mpaka Chunya ni 75,000, lakini kutoka Chunya Mjini mpaka Kambikatoto ni kilometa 240, huwezi kwenda kuuza kwa shilingi 75,000. Kwa hiyo, leo mwananchi huyu tunamuadhibu, kwa sababu ya bei elekezi na yule *supplier* anashindwa kuifikisha kule kwa bei ile ambayo ilitakiwa iweze kumfikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba, Wizara ziko hapa, ziangalie namna ya kuangalia hizi bei kutoka eneo moja hadi lingine ili wananchi wetu hawa waweze kufikiwa bei ikiwa nzuri kwenye ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mpango huu imeeleza pia, namna ambavyo kwenye kilimo tunaendelea kuwekeza kwenye kilimo cha umwagiliaji. Tumeona kutoka mwaka 2021/2022 tumetoka kutoka hekta 690,000 na mwaka 2024/2025 tumefika zaidi ya hekta 983,000. Zaidi ya miaka mitatu tumeongeza zaidi ya hekta 300,000 kwenye upande wa umwagiliaji, hii ni hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, bado tuna maeneo mengi makubwa na mazuri ambayo yanatufaa kwa ajili ya umwagiliaji. Kule kwangu Chunya tuna maeneo makubwa na mazuri. Walishakuja kufanya utafiti, tunaomba fedha zije ili hawa wananchi waweze kunufaika na maeneo ya umwagiliaji haya ili tuweze kuzalisha chakula kingi cha kutosha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka. Nilimwita Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, atafuatiwa na Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando (Baba Levo) na Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele Villa na Mheshimiwa Kakulu Burchard Kakulu wajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia huu Mpango wa *Professor* Kitila, ninampongeza sana. Ninamshukuru Waziri wa Fedha, ni mtendaji mzuri, ametuonyesha mambo mengi katika taarifa zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuwateua kwa sababu ameona vipaji vyenu vinatumika vizuri kwenye hali hii. Kwa hiyo, tunamshukuru sana kwa kuendelea kuwateua kuwepo hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia mpango huu ulivyo na hakuna chochote kitakachozungumzwa katika mpango kama hatutengenezi maisha bora kwa Watanzania. Nianze tu mimi na jimbo langu. Leo nikienda jimboni hata nikihubiri kilimo bora chenye ufanisi watu hawatanisikia. Nikihubiri ufugaji bora wenye ufanisi watu hawatanisikia; kwa nini? Kwa sababu toka mwaka 2021 mpaka leo kila kinachofanyika kwenye Jimbo la Bunda, tembo wanakula. Yaani leo badala ya kuchunga ng'ombe tunachunga makundi ya tembo, kila kinachofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, leo hata ningehubiria watu kiasi gani, mpango mzuri, mpango nini na uchumi mkubwa wa Jimbo la Bunda ni mazao ya kilimo na mazao ya kibiashara. Tembo anakula yote, anakula mpaka katani, anaangusha na maghala anakula. Sasa wale wa Zanzibar niseme ndovu basi ndiyo tusikie vizuri kwa sababu inawezekana nikisema tembo nisieleweke vizuri. Ndovu wanakula mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa upande wangu, nini kifanyike watu wa Bunda waishi kwenye maisha bora? Ni kuruhusu mpango wa *VIP* wa Grumeti waweke uzio *(fence)* kama

ilivyowekwa Serengeti, kama ilivyo Botswana na South Africa. Tukiwekewa *fence* tutaishi. Maana yake ni kwamba leo, jana na hata juzi nilikuwa ninahangaika na watu wa wanyamapori, Wizara ya Maliasili na Utalii walipe fidia. Kila mwaka ni mamilioni ya hela yanalipwa, siyo kwangu tu na maeneo yote. Sasa, kwa nini kama kuna mpango maalum ambao umefanyiwa utafiti wa kuweka *fence* kwa nini tusikubali huo mpango? Maana yake sisi hatutumii hela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Grumeti Fund* wale wa *VIP* wamekubali kuweka *fence* ili kuzuia pamoja na ng'ombe kwenda huko, lakini tembo kuja huku. Wameweka Serengeti ikaleta tatizo la Kiserikali. Mimi kwangu hoja kubwa ni kwamba Serikali ikubali kuweka *fence*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kabla ya *fence* nini kifanyike? Tunaomba sasa *TANAPA*, *TAWA* na *TFS* waendelee kulinda kwa sababu toka tumeanza kuchukua hizi hela za *TANAPA*, *TAWA* na *TFS* kuzileta Serikalini hali ni mbaya sana. Eti, *TANAPA* wakusanye hela, wawape *TRA* halafu *TRA* wakae huko na Serikali warudishe *TANAPA*. Hivi tembo anasubiri huo mchakato kweli hapo? Tuwe wawazi, *TANAPA* na *TAWA* wanalinda Hifadhi ya Taifa na hifadhi zinazotoa mazao mazuri kwa Tanzania ni tano tu, nyingine 22 hazitoi mazao. Bunge lilishaazimia hapa, tuliazimia, tuwape 51% ya kwao halafu 49% ibaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kilichopo ni kwamba Serikali imetii Azimio la Bunge, lakini badala yake ni kwamba hela zinaenda Serikalini ndiyo zirudi, aah aah! Kwani sisi si wataalam wa fedha? Kwa nini tusiweke mkataba kwenye benki kwamba shilingi milioni moja ikiingia, shilingi 510,000 itakuwa ya *TANAPA*, *TAWA* na *TFS* na shilingi 490,000 iende Serikalini ili moja kwa moja kila mtu anapata chake, kwa nini tunasubiri kurudishwa? Kwa hiyo, kwangu ninataka haya mambo yafanyike ili watu wangu wapate amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nimeona mpango wako, lakini ninajiuliza, hivi Januari, 2027 kutatokea nini? Kama tukio la kwanza kwa Tanzania watoto wa mwaka 2021 darasa la

kwanza na watoto wa mwaka 2022 waliokuja kuingia darasa la kwanza, wale wa darasa la sita. Mwaka 2027 Januari, watoto wa darasa la saba na wa darasa la sita wanaingia kwa pamoja; *almost* 3,000,000 na kitu wanaingia kwa pamoja. Ukigawa hapo tunahitaji karibu madarasa 69,000 na kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua wanafunzi walioingia mwaka huu kwa kutolea mfano, 937,000 maana yake madarasa yanayobaki ni mengi. Tumejiandaa vipi kukabiliana na upungufu wa madarasa na shule za sekondari kwenye mpango huo ambao ni sera mpya? Kwa hiyo, hapo napo tuangalie vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, utekelezaji wa miradi…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Taarifa wapi, Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante ninakushukuru. Ninataka tu kumpa taarifa kaka yangu kwa mchango wake mzuri. Alionyesha kuwa *bitter* kwamba *TANAPA* na Ngorongoro wakikusanya fedha zinaenda. Ninampa taarifa tu kwamba, Bunge la Kumi na Mbili tulifanya marekebisho, sasa hivi *TANAPA*…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Getere, kaa chini wakati unapokea taarifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanakusanya na kuchukua *through retention*. Kwa hiyo siyo kwamba fedha zote zinaenda, wanakusanya na kutumia. Kwa hiyo, kama kuna kero zozote zile za tembo na nini wao watu wana fedha wanaweza wakawa wanalipa *on time*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere unapokea taarifa hiyo?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa si dada utaikataaje hata kama iko vibaya sawa tu, naipokea tu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, utekelezaji wa miradi…

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere kuna taarifa ya pili kutoka kwa Mheshimiwa Profesa Shemdoe

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la darasa la sita na la saba kukutana mwaka 2028 Januari, sisi kama Wizara tumeshatoa maelekezo kwenye bajeti ambayo italetwa kwenye Bunge lako. Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wahakikishe kwenye mafungu yao wanaweka ujenzi wa madarasa ambayo yatatusaidia ku-*accommodate* wale wanafunzi mwaka 2028. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere unaipokea hiyo taarifa.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea taarifa ya Profesa, lakini sina hakika kama mkoa na halmashauri zinaweza kuwa na fedha za kujenga haya madarasa. Sasa kama zinashindwa kulipa 10% ya wanawake ndiyo zitajenga madarasa? Ninadhani tujiandae upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kazi ya kumaliza viporo, niombe Serikali iwe kali kidogo, hamna kitu kinanichukiza kama mradi umepewa fedha halafu haukamiliki na mbaya zaidi sasa akienda Waziri kwenye halmashauri fulani au kwenye mkoa anakutana na mkuu wa mkoa anakutana na mkuu wa wilaya. Wanaenda kwenye Kituo cha Afya Unyari, tumepelekewa milioni 500, hakina jengo la upasuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anaona kabisa hapa kuna tatizo anaanza kuna nini, kuna nini, utasikia sasa minong'ono. mkuu wa mkoa anasema mkuu niachie, mkuu wa wilaya anasema mkuu niachie. Hivi wakuachie ulikuwa wapi? Yaani miaka mitano mradi umekufa wewe waziri anaenda niachie, niachie, tutaachiwa mpaka lini? Ninaomba Mawaziri, sehemu hii ninaona wamekuja kivingine, ninawashukuru sana Mungu awasaidie waendelee kubadilika hivyo hivyo.? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna kuachiwa, kama wewe ulikuwepo mradi umeharibika, chukua *action* hapo hapo. Hii Tanzania tumebaki na maneno mengi mno, kusameheana ni kwingi mno, hakuna hiyo. Sasa hivi ni kupambana na tumeambiwa huko Ulaya, wenzetu walikuwa wanatufadhili fedha hapa nimeona Waziri wa Fedha amesema hapa bilioni 39 haziji, kipindi hiki lazima tuangaliane na hata yale makongamano sijui mihadhara sijui nini ipunguzwe. Sasa leo kila siku Mkuu wa Wilaya yuko Dodoma, Mkurugenzi yuko Dodoma, Mkuu wa Mkoa yuko Dodoma. Wanatumia hela zipi au ni hizi ambazo wananchi wanakusanya kwa viazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tusiwe *online meeting,* kwa nini tusifanye hivyo. Lazima tujibane kipindi hiki, Tanzania ionekane kwamba tunafanya kazi ya maana. Kwa hiyo niombe, kwenye Mradi wa Kituo cha Afya Unyali, kwenye Mradi wa Sekondari ya Tirina, kwenye Mradi wa Sekondari ya Sanzati, kwenye Mradi wa Kituo cha Afya Mihingo Bunda, ile miradi ambayo inakuwepo inakuwepo, tukamalize hiyo miradi ambayo inakuwepo na Barabara ya Sanzati inakwenda Nata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najiuliza, nimeuliza swali siku moja hapa la barabara, Spika aliyekuwepo akaniambia muone, Waziri hapa na Naibu Waziri wamalize. Nikaenda kwa Waziri wa Fedha tukaongea, akasema kwamba miezi hii miwili tutapewa bilioni mbili kwa hiyo barabara, mpaka leo. Hivi sasa kwa nini sisi Wabunge tukisema jambo haliheshimiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niwaambie Wabunge nchi hii tunajenga sisi, Watanzania wametuamini sisi, tukiendelea

na hayo mauoga mauoga hapa, tutashindwa kufanya miradi ya wananchi, pale ambapo mama ametoa hela zake zimekwenda kwenye *site*, tusimamie kikamilifu. Sasa tukijifanya waungwana na kila mwaka tunakuja nusu nusu inasaidia nini sasa. Tunajifanya watakatifu, tukirudi humu tuko 30%, inasaidia nini. Tupambane hela zilizoko huko zifanye kazi. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere ahsante sana kwa mchango wako. Eee, nilimwita Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando (Baba Levo) atafuatiwa na Mheshimiwa Boniventura Kiswaga na wengine niliowataja waendelee kujiandaa.

**MHE. CLAYTON R. CHIPANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii adhimu ili niweze kuchangia mawili matatu kwenye Mpango wa Miaka 50 ya Maendeleo ya Nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniweka hai mpaka leo hii kwa sababu kampeni zangu zilikuwa na heka heka nyingi. Pili, namshukuru Mwenyekiti wangu wa Chama Cha Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kupitisha jina la Clayton Revocatus Chipando (Baba Levo). Watu wengi waliongea lakini sasa hivi nadhani akikaa anaona raha kwa sababu anaona mambo yanayoendelea Jimbo la Kigoma Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, ninawashukuru sana wananchi wa Kigoma Mjini walipiga kura nyingi na walinipa moyo tangu ninazindua kampeni katika Jimbo la Kigoma Mjini. Umati uliokuwa unanifuata nyuma, ni wafuasi ambao walinionesha wazi kwamba tunakupeleka Bungeni. Ninataka niwaahidi kwa uwezo wangu na elimu yangu niliyonayo, hii ndiyo ajira yangu kubwa ya mwisho Ubunge, nitawatumikia kwa nguvu zangu zote kuhakikisha ninakuwa Mbunge bora katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukurani, ninaomba nimpongeze Waziri wangu mzee wangu Mheshimiwa Profesa Kitila. Mheshimiwa Profesa Kitila ni moja kati ya ma-*genius*.

Nilikuwa na Mheshimiwa Profesa Kitila, zamani tulikuwa naye CHADEMA, tulifukuzwa wote kama anakumbuka, tulifanya *press* pale pamoja, kikundi chetu, sasa tuko kwenye chama kikubwa, Chama Cha Mapinduzi. Mungu akujalie sana uendelee kutusaidia kwa mawazo haya ambayo umeyaleta katika mpango huu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka ninaomba nijikite katika upande wa vijana. Nimeona mambo mengi sana yameelezewa namna bora kuweza kuwasaidia vijana katika Mpango huu wa miaka 50 ya Maendeleo ya Nchi yetu ya Tanzania. Vijana hawataki konakona, vijana wanataka hela, ninaomba sana mpango huu upunguze kona kona kwenye namna ya kumfikishia kijana hela, kijana anataka pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawaambia ukweli, wakiangalia mara nyingi sana tunakuwa tunasisitiza hapa vijana wajiajiri, wazee kujiajiri lazima uwe na hela, unajiajirije, ukitaka kujiajiri, ukiniambia mimi wakati niko nje ya Bunge Baba Levo jiajiri, najiajirije labda nifungue biashara yangu, biashara naifungua na nini? Tupunguze masharti ya vijana kuweza kukopa, tunaweka masharti magumu, mtu kama Linex anataka kukopa unamwambia alete hati ya nyumba, Linex ana nyumba? Lazima tuweke masharti ambayo yataendana na vijana tulionao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu amemaliza chuo, ndiyo kwanza anahaha na *documents* zake kutafuta ajira unamwambia jiajiri, anajiajiri kwa mfumo gani, unamwambia bwana tafuta mikopo, anaenda kwenye mikopo, benki zetu tunazijua zina vigezo ambavyo hivyo vigezo vinamtaka awe na mali ambayo ameshika aiweke kama dhamana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafute njia sahihi ya hawa vijana pesa ziwafikie bila njia ngumu wanazopitia. Mimi nitawaambieni ukweli, mimi ni mfano, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akituwekea wasanii pesa kwa ajili ya kukopa, tumeenda kukopa, nimeenda kukopa milioni 100, masharti niliyokutana nayo pale cha kwanza niwe na mali kama gari au nyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikajiuliza kuhusu wasanii wa singeli hivi hawa watatoboa kweli kwenye huu mpango. Kwa tafsiri hiyo, hata hizi pesa ambazo nimeona Waziri Mheshimiwa Makonda amepewa shilingi bilioni mbili, wapunguze masharti ya namna vijana kuzifikia hizo pesa. Wakiwawekea masharti magumu, tenda watachukua wale wasanii ambao tayari wameshakuwa matajiri wana hela na wale wenye vipaji wa chini zile pesa hazitawafikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wanataka pesa bila kona kona na ndiyo maana vijana wengi wanabeti kwa sababu ukibeti unamuua Simba mechi ikiisha unachukua hela yako unaendelea na maisha mengine. Kwa hiyo kwenye hili naomba sana Mheshimiwa Waziri aweke mfumo ambao atawasaidia vijana kupata pesa kwa urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tunazungumzia Mpango wa Miaka 50 ya Maendeleo ya Nchi yetu ya Tanzania, ni lazima tuwazungumzie wafanyabiashara wadogo wadogo. Nitatoa mifano, nimezurura sana. Siku moja nilinunua nguo Uturuki za watoto wangu, mimi nina watoto watano nikawanunulia kila mtoto nguo tatu tatu, zikawa kama 15 hivi nikapitia Dubai nikashuka Dubai nikaa Dubai siku tatu, sikudaiwa wala sikuzuiliwa pale *airport*. Nilivyokuja na zile zile nguo nilivyoshuka nazo *Airport* ya Tanzania, wakaniambia ninatakiwa nizilipie ushuru nguo za watoto wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo lazima tutengeneze, hii ikanipa picha kwamba wafanyabiashara wadogo wadogo kuna namna ambavyo wanafinywa kiasi kwamba hata kile kidogo alichonacho kinaondoka. Mfanyabiashara ana simu mbili, simu tatu mwacheni apite, kama kunaonekana kuna ugumu wa kufuta hizi kodi ndogo ndogo si dhahabu zipo tuuze tu, tupunguze hizi kodi ndogo ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana yazingatiwe haya kwa sababu, kama tunawasaidia wawekezaji wakubwa lazima tuwakumbuke na hawa wawekezaji wadogo wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtu anaweza kwenda na simu tano Dubai akapita bila kuulizwa chochote kwa nini akipita nazo hapa kwetu inakuwa tatizo? Twendeni tukambane sokoni wakati anauza, tupunguze mauzo ya *cash* tuweke katika mfumo, watu watumie kadi, watumie kulipa kwa *digital*, mtaiona hela. Nimeenda China mtu anauza bamia anakupa *Alipay* una-*scan* hela inaingia moja kwa moja kwa Serikali, lakini kiuhalisia kwa mfumo huu wa kuwabana hawa wadogo wadogo watawabana watakufa watatengeneza wakubwa, wakubwa watawanyonya wadogo. Ninaomba sana hilo nalo lizingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huu wa mzee Mheshimiwa Profesa Kitila, nimeuangalia nimeona kabisa sasa ni muda muafaka wa kuitangaza Bandari ya Kigoma kuwa ndiyo kitovu cha biashara kwa Kanda ya Ziwa. Kwa sababu sisi ndiyo tuko karibu na Kongo na Kongo ndiyo nchi pekee yenye watu wengi katika ukanda wetu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kongo bahati nzuri tumepata bahati sijui wana matumbo mazuri wanakula kila kitu ambacho tunakitoa Tanzania tunakipeleka kule. Kwa hiyo, ipo namna ambayo tukiitumia Kigoma, ambayo iko *connected* na Burundi, Kongo na Zambia kuna nafasi kubwa ya nchi yetu kutengeneza pesa nyingi ambazo zitakuja kusaidia kwenye miradi mingine tofauti tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna bandari yetu pia ambayo sasa hivi inaboreshwa pale. Tunaomba sana mzee wangu Mheshimiwa Profesa Kitila waweke mitambo ya kisasa. Sasa hivi pale gari moja kushushwa mzigo yaani unaona wanahaha wale jamaa utafikiri sijui wanafanya kazi gani. Yaani wanatumia *focal lift* lakini wanakuwa kama makuli, tunaomba mitambo ya kisasa iwekwe ili kufupisha muda wa kupakia na kupakua mizigo katika Bandari ya Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine yatengenezwe maghala ambayo yatakuwa na baridi ya kuweza kuhifadhi mizigo, nataka niwaambieni ukweli, kuna baadhi ya mazao ambayo yanapatikana Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi yetu ya Tanzania huwezi kuupata mgebuka wewe, nenda kokote hupati mgebuka, lazima uje pale. Pia tuna chikichi, chikichi ndiyo zao pekee ambalo unaweza kulibadilisha kuwa chochote na nitawaambieni hapa. Chikichi unaweza ukaibadilisha ikawa mawese, ukaibadilisha ikawa mafuta ambayo tunakula tunasema *Korie*, ukabadilisha lile ganda lake likawa meza, ukibadilisha ule muse wa ndani unaweza ukaubadilisha ukawa sabuni, hili ni zao moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mkuu aliyepita mzee wangu Mheshimiwa Majaliwa alikuja Kigoma katika kupambania hili zao, akasema kila mwananchi wa Kigoma Mjini apande mchikichi kwenye nyumba yake nje. Hilo jambo halijatekelezeka kwa sababu hakuna kiwanda ambacho hawa watu wakishapanda hayo mazao kwenye nyumba zao watapeleka wapi? Tutengeneze kiwanda ambacho kitasaidia zao la chikichi liweze kuokoa uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasihi sana wamekuwa ni maneno mengi kuhusiana na chikichi. Tunajua Malaysia na Indonesia wamekuwa wakipambana kuhusiana na chikichi na sasa hivi tunaona maendeleo waliyonayo. Nawasihi sana ndugu zangu wataalam, wamesoma sana tulibadilishe chikichi iwe kama watu wa Geita wanavyotumia dhahabu kwa ajili ya maendeleo ya maji wetu wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote tutayasema kama Kigoma hakuna miundombinu mizuri, ni aibu. Ninajua Mheshimiwa Waziri Mkuu anaenda kesho Kigoma kwenye miaka 49 ya Chama Cha Mapinduzi, wakati anatua na ndege apige jicho chini wakati ndege imeshuka kidogo aone vumbi iliyotapakaa katika Mji wa Kigoma Mjini. Ni aibu kuita Kigoma Mjini wakati 85% ni barabara za vumbi, ni aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini wanatufanyia hivi, kwa sababu kiuhalisia kabisa sisi wakitutumia kama kitovu, hii nchi itapunguza tozo nyingi sana za ajabu ajabu mtaani. Kwa sababu tutaleta pesa, hizo pesa zitasababisha wapunguze tozo nyingi. *TRA* tozo walizonazo mfanyabiashara akilipa tozo zote anafilisika,

hata Bakhresa, kama atalipa zote, zote kwa pamoja, atafilisika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni lazima tuwe na vyanzo ambavyo vitasaidia kuwapunguzia mzigo wafanyabiashara. Nisaidieni Kigoma tuwasaidie kupunguza *gap* lililopo katika bajeti zetu katika Nchi yetu ya Tanzania, watutengenezee barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mawaziri ambao amewaleta sasa hivi ni Mawaziri shupavu, wana *speed* ya kutosha. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Chipando muda wako umekwisha, malizia.

**MHE. CLAYTON R. CHIPANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ndiyo Mbunge pekee ambaye sitegemei kuteuliwa kuwa Waziri kwa sababu ya elimu niliyonayo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninawategemea sana, sina wivu na wao lakini mimi ndiyo kiherehere ambaye nitawachomekea na nitawachongea pale ambapo watafanya vitu vya hovyo kwenye Jimbo la Kigoma Mjini, sitowaacha. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba sana Mawaziri watusaidie Jimbo la Kigoma Mjini tupate barabara, tupunguze vumbi. Mheshimiwa Profesa Shemdoe, mzee wangu ameniahidi na nitakesha kwenye ofisi ya mzee wangu, ninaomba anisaidie barabara bila barabara sitarudi humu ndani na kama hataki nirudi asinipe barabara mzee wangu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Clayton Revocatus Chipando (Baba Levo) ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga atafuatiwa na Mheshimiwa Dickson Lutevele,

Mheshimiwa Kakulu Burchard Kakulu, Mheshimiwa Isaya Moses na Mheshimiwa Mwita Waitara wajiandae.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, kabla sijaanza kuchangia naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunistahilisha, kunirudisha kwenye Bunge hili kwa awamu ya tatu na bado ninaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu wa mwaka 2025/2050 tunahitaji mawazo tulivu ili uweze kutekelezeka. Mipango mingi duniani huandaliwa, hutekelezwa kwa sababu viongozi wenyewe wanakubali mpango huo utekelezeke. Tunaweza tukaandika sana kama huko mbele na viongozi wengine hawajaamua itakuwa ni historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza na kilimo, miaka 10 tumeimba kilimo ni hatua ndogo sana iliyoguswa kwenye umwagiliaji, hivi tuna tatizo gani mabonde ambayo yamefanyiwa usanifu yakiweko na ya Magu. Tukikopa fedha tukawekeza tukaanza kutoza wakulima kile walichokipata kwenye uzalishaji tukalipa hayo madeni tuna tatizo gani Watanzania. Nchi zote zilizofanikiwa hazijasubiri *cash* bajeti kwamba tukusanye ndipo tutekeleze nchi zote duniani zilizofanikiwa zilikopa zikatekeleza mpango zikaanza kulipa. Lazima maendeleo utangulie kwanza halafu uanze kuchukua fedha kutokana na kile ambacho umekiwekeza kulipa hilo deni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niombe, hebu nchi iamue kama deni ni himilivu kama deni lina nafasi, tukope tuwekeze kwenye umwagiliaji ili uchumi jumuishi uweze kupatikana. Mfano tu tunayo mabonde mazuri, lakini kila wananchi wanapolima hali ya hewa ikibadilika hawaivishi, anatupa gharama ya mbegu, anatupa gharama ya vibarua, lakini anaambulia hewa. Atafika kwenye kipato cha dola milioni saba, lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Bunge lazima tuamue na tuweke maazimio kwenye mpango huu ili tuupime vizuri mpango huu kwa sababu tukikusanya mapato yetu ya ndani, hatutaweza

kufikia malengo. Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia waandike historia ya Mpango huu kwa kukubali kukopa ili tuwekeze kwenye umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuhusu mbegu; nchi zote duniani zina mbegu zake mbegu hizi tulizonazo lazima tuzitazame zinatupeleka. Je, zinavumilia magonjwa mfano tu mbegu ya pamba leo imelimwa miaka 12, mwananchi anapulizia zaidi ya mara 15 na mapato hayapati utamshawishije kwenda kulima pamba ambayo kwa eka anapata kilo 200, hazalishi kwa tija? Tutafikiaje lengo la kuzalisha kilo milioni moja bila kuwekeza kwenye mbegu, turudi maabara, sayansi ifanye kazi ili tuweze kuwasaidia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasikiliza Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia kwenye suala hilo la mbegu na namna ya kuwekeza viwanda vya nguo, niombe, Mheshimiwa Babalevo amezungumza hapa sisi Tanzania kama hatutazuia kuingiza mali iliyokamilika kutoka nje, hatuwezi kuwaondoa Watanzania kwenye umaskini. Mazao ya kimkakati yale matano ambayo mojawapo amegusa la mchikichi ukiwa unatoka Congo kupita Rwanda kuja Burundi, Burundi imepiga hatua kwa zao la mchikichi, Burundi inakwenda kutuacha sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaagiza mafuta yote kutoka nje, unafikiri mkulima wa alizeti ambapo Mheshimiwa Naibu spika anatoka kule Babati atauza alizeti kwa bei ya juu? Unafikiri mkulima wa pamba atauza pamba yake kwa bei ya juu? Kwa sababu mbegu zake hizo zina mafuta ya kutosha. Sasa hebu tuweke miaka mitano tumwambie MO ndani ya miaka mitano hutaagiza mafuta, tumwambie Bakeresa ndani ya miaka mitano hutaagiza ngano. Ngano yote ilimwe hapa ili iweze kupunguza fedha za kigeni kwenda nje…

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Musukuma, Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpa taarifa mzungumzaji, anayemzungumzia anaitwa Bakhresa siyo Bakeresa. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiswaga, unaipokea hiyo Taarifa?

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majina yanaweza kuwa hayo hayo mengine ya Kigiriki, mengine ya Kisukuma ni hayo hayo, ninapokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ambayo imejitawala miaka 60 lazima tuweke muda. Bakhresa huyo huyo tumempa shamba la kulima miwa kule Bagamoyo anafanya vizuri tunaamini ndani ya miaka mitano hatutakuwa tena na vibali vya kuagiza sukari. Bakhresa huyo huyo tukimpa kulima ngano kule Njombe au Arusha hataagiza ngano atakuwa mkulima mkubwa na atajenga viwanda na tutapunguza fedha za kigeni kwenda nje, tutauza nje ili kuleta fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna tatizo gani waandika Mpango kuamua jambo hili? Nchi iliyojitawala miaka 60; kama tunakuja humu kufurahisha tu kwamba nimeongea kama kilabu hatuna maana ya kuwa Wabunge wa namna hiyo. Tumestahilishwa na Watanzania kuja hapa ili tuweze kuwasaidia na Watanzania wapige hatua. Kwa hiyo, niombe Bunge hili pamoja na Mpango ndani ya miaka mitano vitu ambavyo vinaweza kulimwa hapa na vikapatikana viwe marufuku vilimwe hapa ili tuweze kuzalisha hapahapa, niombe sana hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nchi kuna vikwazo vingi vya uwekezaji. Nilikuwa ninawasikiliza Wabunge, Mbunge wa Mbeya alizungumza sana jana kuhusu viwanda vya nguo. Pamba tunayolima hapa Tanzania inahitaji fedha dola milioni 300 ili kujenga viwanda angalau vitatu vya kuchakata pamba yetu hapa. Tumezungumza miaka mingi lakini *incentive* zetu tulizonazo zinaweza kusaidia mipango mikubwa hii. Mfano tunapozungumza dola milioni 300, *VAT* 18% ni zaidi ya dola milioni 54. Je, kuna Benki

kwanza hapa Tanzania ambayo inaweza kukopesha dola milioni 300, ni ndoto ya Alinacha. Kwa hiyo, lazima utashi wa Serikali yenyewe iweze kuamua ili viwanda hivi vijengwe na kwenye *incentive VAT* iondolewe kwenye uwekezaji mkubwa kama huu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tatizo letu tulilonalo tunaangalia tu kodi ya msingi halafu unasema hii itakuwa *refund*. Sasa wewe unakopa dola milioni 54 za kulipa *VAT* unaanza kuchajiwa riba halafu *refund* yake hata ikija unapewa ileile ni sawasawa? Kwa sababu hizo dola ninazozungumzia za *VAT* ni uwekezaji mwingine wa kiwanda kingine mbona hawatuelewi tuko kwenye *industry* hii sisi. Mimi ni mwekezaji wa ndani ambaye hata nikipata faida siwezi kwenda kujenga *Canada*. Tuangalie miradi ya wawekezaji wazawa, tuipe kipaumbele, *VAT* ni nini? Huyu mwekezaji akianza *production* anaanza kulipa *VAT*. Kwa nini tunang'ang'ania kodi? Kwa nini tunang'ang'ania Sera za Kijerumani, sera za ki-*Europe*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana kwamba sisi ambao tuko kwenye *industry* hii tunakutana na mambo mengi ambayo ni vikwazo kwa kuendeleza hii Dira ya Mwaka 2025 -Mwaka 2050. Kama hatutaondoa vikwazo tukaweka vitu chochezi vya uwekezaji tutaimba, watakuja na wengine, nchi hii ni yetu tungepata historia tulioko hapa kwamba tumebadilisha sera na sheria zikaendana na Dira hii …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunafanya nini? Ninaunga mkono hoja, lakini tusikilizwe hatuna sababu ya kuwa Waheshimiwa Wabunge kama hatusikilizwi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiswaga, ahsante sana kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Dickson Nathan Lutevele Villa, atafuatiwa na Mheshimiwa Kakulu Burchard Kakulu.

Mheshimiwa Isaya Mngurumi Moses, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King wajiandae.

**MHE. DICKSON N. LUTEVELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia Mpango huu wa 2026 - 2050. Kwanza kabisa ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wetu Profesa kwa kutusomea Mpango ambao kimsingi tuliuelewa umechanganua mambo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba nijikite kwenye eneo moja muhimu ambalo pengine linaweza likawa lina mchango mkubwa sana kwa Taifa letu kwenye Mpango huu ikiwa litafanyika kwa vitendo. Katika usomaji Mpango wa Mheshimiwa Waziri yapo maeneo ambayo yanawiana kabisa na Hotuba ya Mheshimiwa Rais. Eneo hilo mojawapo ni namna tutakavyoliendeleza Taifa letu kutoka kwenye uchumi tulionao hivi sasa kwenda kwenye uchumi wa kati na baadaye uchumi mkubwa zaidi. Katika kufanya hivyo tunajielekeza katika kujenga kongani za viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hilo ukisoma taarifa maeneo ya kongani za viwanda yameainishwa mle, lakini kwenye Mpango inasema tunafikiria kujenga katika kila wilaya. Sasa ninaomba nishauri kwamba mpango huu wa kongani za viwanda usiwe mpango wa maeneo fulani, halafu mawazo yakawa kwamba tunafikiria au tutafikiria kuweka katika kila wilaya. Kwa kuwa huu ni mpango ningeomba tujielekeze katika kuweka kongani za viwanda kwenye kila eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tuweke kwenye kila eneo? Hapa kwenye viwanda kuna eneo pana sana ambalo limeajiri watu ambao hata sasa wanafanya kazi kubwa na pengine hatujawafikia. Kwa mfano, katika nchi yetu hata sasa hivi ukitoka hapo nje unakuta kila baada ya mtaa kuna gereji vijana wanatengeneza magari, vijana wako wanafanya kazi za kuchonga (mafundi seremala) wamo humo, lakini hawa vijana hatujawakusanya sehemu moja na kwa kufanya hivi tunaathiri mambo makubwa mawili. Kwanza, miji yetu inakuwa haina

mpangilio mzuri, lakini jambo la pili tunashindwa kukusanya mapato kwa sababu hawa vijana hatujawaweka sehemu moja na hatujawawekea Mpango mzuri unaotufanya turudi kuangalia maendeleo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wasiwasi wangu ni nini, ukisoma taarifa ya *CAG* kwenye Mpango wa *BBT* inaonesha kabisa kwamba mpango huu ulikuwa umelenga kuajiri vijana 9,724 ulianza na vijana hao, lakini mpaka 2024 kwenye taarifa ya *CAG* ya 2024 inasema vijana waliokuwa wamebakia walikuwa ni vijana 514 tu. Maana yake mpango huu umefeli. Kwenye *conclusion* anasema Wizara ya Kilimo na Wizara ya Umwagiliaji walifeli kwenye mpango huu. Pia, Mpango huu ulikuwa unasema tunakwenda mbele kwa miaka nane *target* yake, lakini ndani ya miaka miwili tayari inaonesha Mpango ulikuwa umefeli kwa sababu vijana 900 na, kwa mwaka mmoja wakashuka mpaka vijana 500 na, hawa vijana 400 na kitu wamekwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni kwamba mpango huu ulikuwa umefeli na sehemu gani ninaweza kusema ulifeli? Kwenye Mpango wa *BBT* yalikuwa yameainishwa maeneo ambayo mpango huo unatekelezwa. Wewe unamtoa kijana Mbinga unamleta atekeleze Mpango wa *BBT* Dodoma, hata mazingira tu yanakataa. Namna ya ufanyaji kazi wa watu wa huku na watu wa kule hayashabihiani, lakini tukiweka kongani za viwanda tutakuwa na faida zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, maeneo mengi katika nchi yetu watu watajiajiri. Leo hii tunajenga vyuo vya *VETA* katika kila wilaya lakini je, tumeshajiuliza hawa vijana tunaowajengea *VETA,* hawa watu wanaoingia *VETA* baada ya kutoka hapo watafanya kazi wapi? Tunasema kwamba mtu akisoma *VETA* atajiajiri. Kujiajiri siyo jambo la kufikirika ni jambo linalotaka mtaji. Kujiajiri siyo jambo la kuamka asubuhi ukasema ninajiajiri ni jambo linalotaka mwendelezo. Hivyo basi, ninaomba kushauri Wizara pamoja na taasisi zinazohusika kwenye haya mambo kwanza kabisa Mpango huu uwe ni wa kila wilaya ili tuwafikie watu wote kwenye nchi nzima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, twende tukajifunze kwa Mataifa yaliyofanikiwa. Nilikuwa ninasoma taarifa ya namna wenzetu walivyofanikiwa, kwa mfano China, 12% ya pato la Taifa la China wanategemea viwanda vidogovidogo ambapo viwanda vidogovidogo vimeajiri takribani watu milioni 60. Idadi ya Watanzania wote imeajiriwa kwenye sekta moja tu Nchini China. Sasa twende maeneo hayo tujifunze. Twende India tujifunze kwa wenzetu waliofanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo mamlaka kwa mfano *TanTrade*; jana mchangiaji mmoja alisema tuwe tunafanya *check and balance* tukipanga mpango hata kama wa mwaka mmoja, jamani tuliwakabidhi hiki mmefika wapi? *TanTrade* atuambie kwa mwaka amepeleka vijana wangapi kupata *exposure?* Ukifuatilia unakuta wanaokwenda huwa ni wale wale, ni wale wale, ni wale wale, vijana walioko kijijini hawana *exposure*. Nguvu wanayo, uwezo wa kufanya kazi wanao, lakini kwa sababu tunakwenda taratibu hawana *exposure*. *TanTrade* chukua vijana 100 peleka China wakajifunze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa mfano, niliomba kwa *TanTrade* mara nyingi sana kwenda nikaangalie tu masuala ya *machines,* lakini nikakosa *private sector* ikanipeleka *Dubai WoodShow*. Wakati niko *WoodShow* nimekutana na masoko ya India, China na maeneo mengine niliporudi nimewapa Watanzania wenzangu masoko na wamefanya *export*. Kwa nini tusifanye haya? Kwa nini tusiwapeleke wale wanaolengwa na Serikali? Badala yake tunapeleka watu wale wale waliofanikiwa wenye viwanda vikubwa, tufikiri kuhusu hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tunafikiria Mpango wa Miaka 50 na kikubwa tunazungumzia viwanda. Tunapozungumzia hivyo viwanda, tuna viwanda ambavyo mpaka sasa vimeajiri watu wengi sana na havifanyi vizuri. Kwenye mpango havijaelezewa. Angalia Viwanda vya Chai kule Lupembe, angalia viwanda vya chai kule Mufindi. Angalia Viwanda vya Kahawa, kwenye Mpango huu tunasema tuna mpango gani wa kuhakikisha viwanda vile vinaendelea kufanya kazi. Kwa sababu katika viwanda vile wako babu zetu walitoa

mashamba kwa ajili ya chai; walitoa mashamba kwa ajili ya kahawa; na walitoa mashamba kwa ajili ya Mikonge. Tunakuja na mpango gani wa kuhakikisha viwanda vile vinaendelea kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia ninaomba sana sana nisisitize kwamba katika mpango huu twende kwanza *field* twende tukawaone vijana. Sasa hivi Serikali imejenga shule kila eneo, imejenga sekondari kila eneo na vijana wanafaulu, lakini wapo ambao hawafaulu kwa *syllabus* na wale vijana wakiingia kwenye ufundi kwenye magereji mafundi wa umeme mafundi wa magari wanafanya vizuri sana kwa sababu ubongo wao bado uko mbichi. Wale vijana kwenye Mpango huu tunawazungumziaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipoangalia tutajikuta tunakwenda na Taifa la wasomi watupu, lakini kuna kundi kubwa nyuma tunaliacha na kundi hilo ndilo linalozalisha. Kwa hiyo, kwenye Mpango usijilengeshe pekee yake kwa waliosoma, tuangalie na wale wanaofeli kwa sababu ni Watanzania na wanashiriki kwenye kuzalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dickson Lutevele Villa, ninakushukuru sana kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Kakulu Burchard Kakulu, Mheshimiwa Isaya Mngurumi Moses atafuatia.

**MHE. KAKULU B. KAKULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninakushukuru kwa kunipa nafasi na ninawapongeza Mawaziri wote wawili waliotuwasilishia taarifa zao. Waziri Profesa Kitila Alexander Mkumbo na Waziri wetu wa Fedha wamefanya mawasilisho muhimu na mazuri sana kwa nchi yetu. Sisi kazi yetu ni kuwashauri namna gani ya kuyaboresha na kuhakikisha kwamba, maoni yaliyopo katika mpango wetu yanatekelezwa, kama tunavyotarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajielekeza kwenye maeneo machache sana, la kwanza ambalo ninataka kuchangia ni hasa katika kugharimia mpango kwa sababu, unaweza ukapanga vizuri, lakini utekelezaji wa mipango hiyo ni kitu kingine. Katikati ya kupanga na kutekeleza ni fedha, bila fedha na rasilimaliwatu, mipango utakuwanayo, lakini matokeo yako kwa sehemu kubwa yatategemea injini inayoitwa pesa. Tunapataje pesa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajielekeza kwenye jambo la kwanza kuhusu maboresho au *reforms* muhimu katika mashirika yetu ya umma. Katika mpango, Mheshimiwa Waziri ametueleza kwamba, matarajio ya Serikali ni kuona sekta ya umma, kupitia mashirika ya umma, inachangia angalau asilimia nane ya matarajio ya rasilimali ili kugharimia mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu kwa sekta, mashirika ya umma peke yake nchi hii yana *assets* zenye thamani ya zaidi ya shilingi trilioni 86.3. Mashirika yenye uwezo mkubwa na mali kubwa kiasi hicho kuchangia kiasi hicho bado ni kidogo. Kwa hiyo, tunahitaji na ninaungana na maono ya Mheshimiwa Waziri ya kufanya maboresho makubwa na *more aggressively* katika mashirika yetu ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapa mfano, hebu tuangalie uwezekano wa mashirika yetu yote yanayojiendesha kibiashara tualike ushiriki kwa sekta binafsi kwenye mashirika hayo badala ya kuendelea kuyashikilia; ufanisi bado upo chini, tija bado iko chini na faida bado iko chini. Tualike ufanisi wa sekta binafsi kupitia masoko yetu ya mitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo, moja, tutapata faida ya kuwaalika Watanzania kushiriki moja kwa moja katika kuyaendesha mashirika yao. Pili, tutaialika sekta yetu ya ndani binafsi kushiriki moja kwa moja katika kumiliki mashirika yetu na kuyaendesha, ili kwanza tupate tija. Pili, tuongeze ufanisi, tuongeze faida na tuongeze ajira. Tatu, kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumesaidia kuchangia utekelezaji wa mpango wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninasisitiza Mheshimiwa Waziri atusaidie ku-*drive radical and fundamental change* katika mashirika yetu ya umma. Ninaamini sana katika ufanisi ulioko katika sekta binafsi. Mashirika yetu ya umma yako yanayofanya kazi vizuri sana kibiashara, lakini naamini yanaweza kufanya mara 10 zaidi, kama tukialika sekta binafsi kushiriki na tukiwaalika wananchi katika kumiliki mashirika yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mifano mizuri, angalau, ya mashirika makubwa mawili. Kwa mfano, *NMB* na *CRDB* miaka 30 iliyopita wakati tunabinafsisha *CRDB* ilikuwa na hali hoi kabisa taabani, leo *quarter* ya nne kwa matokeo yao waliyoyatoa juzi *CRDB* peke yake imepata faida kabla ya kodi shilingi trilioni moja na *NMB* faida yake kabla kodi ni shilingi trilioni 1.13. Hebu tuangalie miaka 30 tu, kizazi kimoja hapo katikati, lakini kampuni mbili tulizoamua kuzibinafsisha leo zinachangia, moja ni kwa sababu, tuna hisa kidogo kwenye hayo mashirika tunapata gawio na pili tunakusanya kodi pale, 30% inaingia *TRA* huku tunapata gawio kwa hiyo, tunapata mara mbili. Kwa hiyo, ninasisitiza kabisa tufanye mabadilko makubwa kwenye mashirika yetu, tusiogope. Tuwaalike sekta binafsi washiriki moja kwa moja, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni Serikali inapata *stress* kubwa sana kutafuta fedha, kukopa na kukusanya kodi, lakini ipo miradi ambayo ina uwezo wa kualika sekta binafsi ikashiriki moja kwa moja kuiendesha. Matumizi ya *PPP* katika kutafuta fedha za kugharamia mpango ni muhimu, tupunguze uwoga, tuamini watu watapata na sisi tutapata. Watatusaidia sisi kupunguza *stress* yetu ya kibajeti na watatusaidia kutekeleza hiyo miradi kwa haraka katika muda tunaotarajia. Sisi tutajielekeza kwenye miradi ambayo tunafikiri ni muhimu, lakini haiwezi kuvutia uwekezaji kutoka sekta binafsi kwa hiyo, ni muhimu sana haya mambo kuyazingatia, kama ambavyo ninasisitiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, kuhusu *carbon credit*, *carbon finance* au tunaita biashara ya kaboni. Kama Wilaya moja tu ya Tanganyika inaweza kupata shilingi bilioni 20 kwa mwaka, hebu fikiria, tuna misitu ambayo ni karibu 55% ya uso

wa ardhi yetu ya nchi nzima. Tukiamua hiyo misitu kuirasimisha, tukaiweka kwenye biashara ya kaboni tuta-*generate* shilingi ngapi, kwa ajili ya kusaidia kutekeleza mpango wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji mambo matatu tu muhimu; la kwanza ni kuihifadhi misitu yetu, la pili ni ku-*certify,* tuitafutia *thirdy party verification,* ikawa *certified,* tukaanza kukusanya fedha na tatu ni kuhakikisha tunaandaa watu wetu wawe na uwezo wa kuifahamu hii sekta vizuri kwa ku-*train* watu wetu katika vyuo mahiri kabisa katika eneo hili. Mambo matatu tu, hela zina-*flow* zenyewe baada ya haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ninakusudia kuchangia ni kuhusu namna ya kufanya mapinduzi ya uchumi wa vijijini. *A more radical rural economy* yetu inahitaji tufanye maamuzi muhimu kuhusu namna tunavyosimamia sekta yetu ya ushirika. Ushirika ninaamini ndiyo nyenzo muhimu sana ya kufanya mapinduzi makubwa sana vijijini sana. Hebu fikiria kwamba, kwa kiwango na idadi ya vyama vya ushirika tulivyonavyo vijijini kila chama cha ushirika kikawa na mashine, angalau kiwanda kidogo cha kuongeza thamani kidogo kwenye mazao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tutakuwa tumeongeza mazao yetu thamani; pili tutazalisha ajira; na tatu tutachechemua uchumi kwenye eneo lile kwa sababu, vile viwanda vitazalisha shughuli nyingine pale; kama kuna mama ntilie atauza chakula, kama kuna mwingine ana-*supply* vipuri ataleta pale, amepata pesa. Kwa hiyo, tutaongeza tija kwenye mazao yetu, tutatengeneza ajira vijijini, tutazuia kwa sehemu fulani ile *rural urban drift* ya vijana wetu wanaotoka vijijini kuja mijini na kwa hiyo, kupunguza *pressure* ya vijana walioko mjini kutafuta ajira kumbe ajira zinaweza kupatikana vijijini kama tukiamua kufanya maamuzi muhimu ya kubadili sekta yetu vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha muhimu sana katika hili ni kuhakikisha ushirika wetu unasimamiwa kwa uadilifu kwa sababu, ubabaishaji ni mwingi sana kwenye vyama vya ushirika wakati mwingine. Kwa hiyo, lazima kusimamia vyama vya ushirika *more*

*aggressively* hasa kwa kuwekeza katika teknolojia ya namna ya kusimamia vyama vyetu vishiriki vizuri zaidi. Kujenga uwezo wa watu wetu ikibidi kutenganisha ushirika wa mazao na ushirika wa fedha, ili ushirika wa fedha usimamiwe tofauti na ushirika mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona nizungumze hayo, lakini kwa kuhitimisha, kama nyongeza kwa wenzangu waliotangulia kuhusu mbegu, bado tuna nafasi ya kufanya vizuri. Shirika letu la *ASA,* wakati fulani tuliwahi kupendekeza JKT itusaidie kuzalisha mbegu. Tukitumia nidhamu tuka-*exploit* nidhamu ya jeshi letu, hasa Shirika letu lile la SUMA-JKT, tunaweza kuzalisha mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbegu hii tani laki mbili na kitu ni kitu kidogo sana, ni uamuzi tu. Ardhi tunayo, watu tunao, watu wenye bidii wapo, ni uamuzi tu. Tufanye maamuzi ya kulifanya Shirika letu la SUMA JKT tuwape uwezo wa kuzalisha hizo mbegu, ili twende kuchochea kilimo chetu, mbegu ni jambo muhimu, mbegu ni usalama wa nchi. Mtu anaweza akaamua kukusababishia njaa kwa kukuletea mbegu mbovu tu, halafu ukatumia pesa nyingi sana kutafuta chakula, watu wako huko wanakufa, watu hawazalishi wana njaa. Kwa hiyo, ni muhimu hili jambo tulipe kipaumbele, ni jambo muhimu sana kama unataka kusababisha mapinduzi makubwa sana kwenye viwanda na kwenye kilimo chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimeona niyasema hayo kwa kuhitimisha kwa sababu, ni masuala muhimu. Kama wenzangu walivyosema mwanzoni, kilimo ndiyo nguzo muhimu sana ya mapinduzi ya uchumi wetu. Tukatae, tusikatae, ndiyo eneo ambalo linaajiri watu wetu wengi sana vijijini. Kama tukifanya mabadiliko kidogo kwa kuweka na kufanya mapinduzi ya viwanda vijijini, kwa kuongeza tija kwenye mazao yetu, kilimo chetu kitasaidia kuchangia pato letu la Taifa na kuzalisha ajira nyingi sana kwa vijana wetu na kwa hiyo, tatizo tunalolia nalo la ajira, tutafika mahali itakuwa ni historia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Ninamalizia kwa kuwashukuru wananchi wangu wapendwa

kabisa wa Jimbo la Mbagala, ninawatakia heri na upendo mwingi sana. Mwenyezi Mungu awabariki sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kakulu kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Isaya Mngurumi Moses, atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara. Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga ajiandae.

**MHE. ISAYA M. MOSES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kuniona. Kwa sababu leo ni mara yangu ya kwanza kusimama, kwanza ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kufika kwenye Bunge hili, chumba hiki Tukufu. Ninashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumshukuru Mwenyekiti wangu wa Chama Cha Mapinduzi, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ninapenda kumpongeza Makamu wa Rais, Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi. Ninapenda pia kumpongeza Rais wa Zanzibar, Dkt. Hussein Mwinyi. Ninampongeza vile vile Spika Wangu, Mussa Azzan Zungu. Ninapenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote waliopata uteuzi, tuna Imani nao na tumeona kazi yenu wanayoifanya, tuna imani tutafika salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwapongeza wananchi wangu wa Jimbo la Kongwa kwa kunichagua kuwa hapa, kwa kweli, sitawaacha. Wamenifanyia vizuri kumchagua Rais wangu kwa kumpa kura nyingi sana, hata alivyopita pale kwenye kampeni watu walijaa sana pale Kibaigwa, mpaka Rais mwenyewe alifurahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, ninapenda sasa kuwashukuru hao Mawaziri wawili kwa kuwasilisha Mpango wao wa Maendeleo. Mpango wa Maendeleo wa Serikali ni mpango ulioshiba, maana mimi ni mdau ninafahamu haya mambo, kazi iliyofanyika ni kubwa na wanastahili pongezi. Kilichobaki ni kusimamia utekelezaji wa huu Mpango wa Maendeleo, ukisimamiwa vizuri tutafika salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru kwa kupanga 70% itatoka kwenye *private sector* na 30% itoke kwenye *public sector*. Huo ni ubunifu na ni mawazo makubwa ya kina profesa. Ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo machache tu ninataka niongezee, hayo tukiyafanya vizuri mpango wetu utakwenda vizuri sana. Kwanza ni kilimo cha umwagiliaji; pili, nitazungumzia ufugaji; tatu nikipata muda nitazungumzia viwanda na mwisho nitazungumzia suala la miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kilimo cha umwagiliaji. Hilo ndiyo utaratibu mzima, ili tufike salama kwenye mipango yetu hii; mpango mfupi, mpango wa kati na mpango mrefu. Kwanza ni lazima tuwe na uhakika wa chakula, Taifa lisipokuwa na chakula lina njaa, siyo Taifa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi tu mmeona hali halisi, mvua imejaribu tu kufanya kidogo watu tukawa na wasiwasi kwamba, tutakwenda wapi. Lazima tuwe na uhakika wa chakula halafu tuwe na ziada, ziada ile sasa ni biashara. Tukifanya hivyo, tutakwenda vizuri, tukiwa na kilimo cha umwagiliaji maana yake ni tutatumia mito yetu vizuri, tutachimba mabwawa, tutachimba visima na tukishafanya hivyo, kilimo kitakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafute mbegu bora za kuweza kuzalisha, maana sasa hivi wakulima wangu na wa sehemu zingine wanapanda mbegu kwa kutumia nafaka, wala siyo mbegu. Ni nafaka wanalima, hizo hizo wanaenda kupanda, lakini tukitumia utaratibu mzuri wa kilimo, ziko mbegu bora za kilimo. Sasa hivi wakulima wengi, hasa kule kwangu Kongwa, Sehemu za Ngomai, Mkoka na Mlali hao watu wanalima ekari moja inatoa magunia matatu, magunia mawili, gunia moja, wakati kuna mbegu bora ya mahindi; ukichukua ile *DK* ngapi sijui, 777 DK, mpaka 93, uwezo wa kuzalisha kwa ekari moja ni magunia 40 mpaka 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukienda kwa utaratibu huu wa kipato kikubwa, yaani tukaamua, kama Serikali sasa, tukaamua

kwamba, sasa kilimo cha umwagiliaji na mbegu bora zitumike tutamtoa mtu, mkulima atabadilika. Hata lile walikuwa wanasema pato la mtu mmoja mmoja, *per capita income* ile Dola 7,000, nina imani tutapita kwa sababu, leo hii nina uhakika pale Soko la Kimataifa la Kibaigwa gunia la kilo 100 linauzwa shilingi laki moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mtu akilima eka moja anapata magunia 40. Wako wakulima kule Ngomai, Mkoka, wanalima, mtu ana ekari 1,000 anapata magunia 1,000; maana yake ni *average* ya eka moja gunia moja. Ukienda kwake utakuta *quantity* ya mahindi imejaa pale utasema huyu ni tajiri, lakini ukiangalia uhalisia kamili huyu mtu anapata gunia moja kwa eka moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukimtengeneza huyu mtu na wale watu wako vizuri mtu mmoja unaweza ukakuta ana ma-*tractor* 10 ya kwake binafsi, yako pale 10. Sasa tukimwezesha kilimo cha umwagiliaji huyu mtu, akatengenezewa mazingira mazuri, maana yake ni kwamba, badala ya kupata magunia 1,000 huyu mtu atapata magunia 40,000 ukizidisha kwa shilingi 100,000 kwa bei ya Kibaigwa ya leo, ambayo mimi juzi nimeuza, huyu mtu wa ekari 1,000 atapata magunia 40,000 ambayo *income* yake itakuwa ni shilingi bilioni nne. Sasa kwa nini asifike huko tunakosema kwenye Dola 7,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama tutawawezesha hawa wakulima vizuri kabisa tutatoka. Tujitahidi sasa tufumbe macho, Serikali tuingize hela kwenye kilimo. Mfano pale Kongwa, maji yako jirani ni kuchimba kidogo tu yanapatikana. Dodoma kwa ujumla hali ya maji ipo vizuri, wakituwezesha; mfano kama pale kwangu nikiwezeshwa mabwawa 10 na visima 12 maana yake ni kwamba, nitamhakikishia Mheshimiwa Profesa nitafika kwenye *per capita income* ya 8,000 sio 7,000. Hebu wajaribu tuone, wafanye majaribio tu, tuamue tufanye eneo ambalo ni la mfano, tuweke mahali, uchumi utapanda sana, tukifanya hivi tutakwenda vizuri. Ninawaomba sana tufanye vitu kwa vitendo tutafika mahali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninazungumzia ufugaji. Kwenye jambo letu hili, Mpango wa Maendeleo, wamezungumzia ufugaji, lakini hawakuingia *in detail.* Wafugaji ni watu muhimu sana na ni wawekezaji wakubwa, hii sekta tukiitumia vizuri, ya wafugaji, tutakwenda mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi nilikuwa ninaongea na Katibu Mkuu wa Chama cha Wafugaji Tanzania, hiyo ni *private sector,* ameniambia tunao mifugo, tukiacha mbuzi na kondoo, ng'ombe milioni 37, hawa tukiwatumia vizuri uchumi huu utakwenda vizuri, ila sasa hawa watu wana shida. Shida ya kwanza ni wana changamoto, maana ukifika wamejipanga wana salamu yao utasikia, ukifika tu pale, wanasalimiana ufugaji maisha yetu, maisha yetu ufugaji kwa hiyo, wanajua kwamba, ufugaji ni maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya kwanza ni ardhi. Ardhi inatakiwa ipimwe, tuwapimie hawa watu ardhi, ili wasiwe wanarukaruka tu. Pili ni maji, hawa watu wana shida ya maji, tuwatengenezee utaratibu wa kupata maji wasiwe wanahamahama. Tatu ni malisho, hawa watu wana shida ya malisho. Kama tutawatengenezea utaratibu mzuri wa malisho hawa watu tutapata kipato kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto yao nyingine ni masoko. Masoko yao kidogo ni magumu. Sasa hivi nilikuwa ninaongea na huyu Katibu Mkuu, Bwana Matayo Daniel ananiambia sasa hivi wanapeleka Comoro, lakini Comoro wana shida ya meli, ile meli ng'ombe wanakufa, lakini wakienda Comoro kilo moja ya nyama kwa hela ya Tanzania ni 30,000/=. Kwa hiyo, tukiwaboreshea watu, tukawatengenezea mazingira mazuri, tutapata *income* ya kutosha na mpango wetu utakwenda vizuri zaidi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. ISAYA M. MOSES:** Namalizia Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Malizia.

**MHE. ISAYA M. MOSES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba suala la miundombinu iko shida pale. Kwenye bajeti hii, tunaenda na iliyopita, Ilani ya Uchaguzi ilituwekea barabara ya kutoka *Kongwa Junction* kwenda *NARCO*, kwenda Hogoro, kwenda Songambele mpaka Zoisa na barabara ya kwenda Zoisa – Kiteto mpaka Arusha. Hiyo ni barabara ya uchumi, ambayo mazao mengi yanatoka kule, lakini sasahivi haizungumzwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo barabara mpaka Mheshimiwa Rais alisimamia mikataba yake, kusaini mikataba, lakini mpaka leo hii haijulikani kinachoendelea. Huko watu wanauliza, hivi Rais inawezekana akasimama akasema ni mikataba ya uongo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaomba Wizara ya Ujenzi wajiandae vizuri. Kama kuna mabadiliko yoyote ninaomba wakasimame kule watetee maana sisi tutakufa. Hiyo barabara inahitajiwa sana kwenye uchumi. Ninawaomba sana hicho kitu. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Isaya Moses, nilimwita Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia mpango wa maendeleo wa nchi yetu. Ninampongeza Rais, kulikuwa na malalamiko namna ya kupanga mipango yetu, ameshaunda Wizara na amempa Profesa Kitila Alexander Mkumbo na Naibu wake pia ameweka Waziri wa Fedha, Balozi mzoefu kwa muda mrefu, pamoja na Watendaji wa Wizara tunawatakia kila la kheri katika kazi hii kubwa ambayo wamepewa ambayo kwa kweli inahitaji kila mtu ashiriki katika mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu haijawahi kuwa na upungufu wa mipango, ninachomwambia Profesa Kitila Mkumbo

yeye ni Profesa, ni mtafiti na Maprofesa wengine waliomo humu na Madaktari na wasomi mbalimbali kuwa, nchi hii haina upungufu wa mipango, shida tuliyonayo ni namna ya kutekeleza mipango tuliyonayo. Ningeshauri Waheshimiwa Wabunge tujielekeze katika maeneo hayo, ukirudi nyuma mipango iliyopangwa katika nchi hii ma-*shelf* huko yamejaa, sasa Bunge hili Rais mwenyewe ana utashi amelileta jambo hili, ameshaunda Wizara, amewapa watu nafasi, tuwasaidia kuwashauri namna ya kwenda mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza vilevile Mheshimiwa Rais kwamba mipango ile ambayo ilikuwa kizungumkuti kwa muda mrefu, Liganga na Mchuchuma, gesi, *SGR* na vitu vingine vingi na viwanja mbalimbali vya ndege ameshatekeleza na vingine vimeanza kufanya kazi. Tunampongeza kwa jambo hilo kubwa sana kwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine niwaambie Watanzania na Wabunge tunapokuwa tunampongeza Rais sisi wengine wanasayansi ni lazima uwe na *facts,* ukiangalia mambo yaliyofanyika, hivi kwa mfano, wenzangu walipata Ubunge, mimi niliutafuta. Nilikatwakatwa huko kote na viongozi wangu wa Wilaya hawanitaki hata bure, Mwenyekiti wa Mkoa na Kamati ya Siasa na Kamati Kuu wakaniteua, nikarudi nikashinda kura za maoni. Nikarudi tena wakanikata tena kule yale majamaa, nimekuja Mkoa na Mama Samia amenirudisha, hivi wanataka nisimpongeze kweli? Haiwezekani! Ukinizuia nisimpongeze Rais utakuwa hunitendei haki, halafu usisahau kwamba nilikuwa Naibu Waziri wa Muungano na Mazingira, Rais akiwa Makamu wa Rais amenituma kazi, kwa hiyo ninamjua vizuri kwa utendaji wake wa kazi na uthubutu. Yapo mambo mazito Mama ameamua ameyafanya hapa, kabisa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mambo haya ambayo vilikuwa ni viporo vya muda mrefu aliwaambia kazi itaendelea na imeendelea. Hivi sasa tuchambue mambo haya namna ya kuzungumza, kama kuna ukweli tuuseme na ukweli utatuweka huru, kama kuna mahali tukosoe na watu wapokee hivyo, twende na Taifa la namna hiyo. Pia msisahau kwamba mimi ni Mjukuu wa

Baba wa Taifa, kwa hiyo hilo ni muhimu sana kuliweka. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitila Mkumbo amesema atawezesha makandarasi wa ndani, hili ni donda ndugu. Pale kutoka Mjini Tarime mpaka Mogabiri, nimewaambia wakakwangue ile inayoitwa lami ubaki udongo watu wajue hakuna lami, kuna udongo pale. Barabara ya kutoka Mogabiri - Nyamwaga - Nyamongo ni kizungumkuti, miaka saba kilomita 25 anadai mpaka leo bilioni 4.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pale Musoma kwa Profesa Muhongo, Makojo – Busekela, ukizungumza habari ya mpango watakuambia barabara. Ukienda Busigwe - Kitaramo - Butiama kama hukutaja barabara hii na fedha ulipe mkandarasi, utaimba hawatakupigia makofi. Ukienda Tarime Mjini nimetaja Mogabiri mpaka kule Tarime Mjini, mkandarasi yupo mpaka mabati yamedondoka, hawatakuelewa na mpango wanataka barabara ilimwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Mwibara, Busambara Mugara wanataka barabara ilimwe. Ukienda Rorya – Utege - Shirati, Chege hawezi kukuelewa bila kuzungumza habari hii. Kwa hiyo Profesa ametaja, nimwambie sasa mwezi wa 11 ukija hapa, pamoja na Mawaziri wengine watueleze hao makandarasi ambao wanadai fedha na miradi ambayo wameshasaini wanalipaje kabla ya kuweka miradi mingine mipya, asiweke kiporo juu ya kiporo, tuambie hizi barabara zingine na miradi mingine ya maji wanaweka mpango gani wa kulipa ndiyo ulete mipango mingine hapa mipya ya kufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu tuwekeze kwenye elimu ya amali. Iwe shule ya msingi akimaliza darasa la saba ana jambo la kufanya, iwe sekondari ana jambo la kufanya, iwe ngazi yoyote ya chuo ana jambo la kufanya, tufanye kama Wachina. Mchina ukimwita aje kufanya kazi ya umeme, akiona shughuli imeisha anakuwa fundi bomba, hujakaa sawa anakuwa fundi cherehani. Tufanye namna hiyo ili tusaidie vinginevyo tutakuwa tunapata lawama kila siku, kwa sababu hatuwezi kuajiri vijana

wote, lakini tuna vyuo, kwa hiyo, tuwekeze maana yake twende kwenye teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetajwa habari ya ajira, nikawa ninajiuliza pamoja na Wizara ya mdogo wangu pale wa vijana. Kwanza juzi wamewaajiri watu hapa, ukiangalia Wabunge walivyokaa humu Bungeni, kila Mkoa una wawakilishi vijana, akinamama na majimbo, kila Mkoa hapa umewakilishwa, tunataka ajira nchi hii iwe na msawazo huu. Wakitoa ajira tuone watu wetu wamepata ajira, wafanye kazi hiyo, ukipitia watu walioajiriwa pale ni kama hatumo maeneo fulani fulani hivi wanasababisha watu kuanza kujadili huyu kapataje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, alete mpango, wanawezaje kutangaza ajira 10,000, twende kwenye uwakilishi wa Majimbo, Mikoa na makabila yote yapo humu ndani, tuombe hilo walifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais amefanya uthubutu mkubwa, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *PAC*, ameshaelekeza walete sheria ya namna ya kupata Watendaji Wakuu wa Taasisi na haya Mashirika ya Umma na kupata Wajumbe wa Bodi, wameleta mapendekezo Kamati ya Bajeti kwamba hata Wakurugenzi kama wanatangaza ajira Mtendaji wa Kata nafasi mbili, wanatangaza watu wanaenda 200 mpaka 500. Kwa nini hizi Halmashauri wasitangaze, 180 ni nyingi sana. Kwa hiyo Wakurugenzi wale wafanye v*etting,* wapewe vigezo, wapewe kazi, hata Makatibu Tawala wale *(DAS)* mpaka *(RAS),* hizi ni taasisi kuna miradi mikubwa ya kiuchumi, kuna viwanda pale, hawa watu wapewe malengo wafanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watenganishe siasa na utumishi wa umma ili twende mbele Profesa anafahamu ninachokizungumza. Walifanya hivyo *London - England* tangu miaka ya 1940, walifanya hivyo Singapore twende kuweka watu kwa vigezo, kwa uwezo, tusiweke mtu kwa sababu ni ndugu yake na Waitara, tulisoma darasa moja, tupimane na wakifanya hivyo hawa vijana ambao wanalalamika wazee kupata uteuzi, hawatalalamika kwa sababu wameweka mambo wazi, wameenda kwenye ushindani

na mtu amekosa nafasi kwa vigezo, hawezi kulaumu. Yule ambaye amepata nafasi tunavyo vigezo kwamba baada ya miezi sita ama mwaka mzima hujafanya kazi ambayo tumeitarajia utaondoka atakuja mtu mwingine, watafanya kazi kwa ushindani na kazi itakuwa nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa hapa tusiongee jambo la utawala bora kwa kujifichaficha, tuongee jambo la utawala bora hadharani na kuna vigezo, watu wameenda shule kuona nini maana ya utawala bora, kwa hiyo tukitaja mambo haya tutaje kwa upana wake na watu wajue tunataka utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano hapa, Profesa amesema kutakuwa na uwazi, kutakuwa na uwajibikaji, hili jambo ni kubwa, kuna utawala wa kisheria, mambo ya demokrasia na vitu vingine. Ushauri wangu hapa ninataka niseme, mpango huu ukiangalia mawazo yaliyokuja ni makubwa yanahitaji kila Waziri aje hapa atuambie yeye anakwama wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ambaye Bunge linatakiwa limhoji limwajibishe atoe majibu sahihi hawezi kuja kuninong'oneza mimi, inatakiwa ikiwezekana Serikali ifanye kazi yake, Bunge lifanye kazi yake, ndiyo utaratibu wa Bunge hili. Kwa hiyo, lazima Wabunge tuzungumze na Mawaziri wa upande wa Serikali, kila mtu afanye kazi iende vizuri, ndiyo mambo ya utawala bora. Tukitaka hoja imekuja hapa iandaliwe vizuri tupate majibu, Mama Samia amejipanga vizuri, ukimsikiliza, mawazo yake, maamuzi yake, viongozi wangeelewa Rais anachokitaka, anataka matokeo, hizi changamoto ziishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi Mbunge kipindi cha tatu humu, nilikuwa ninaangalia hapa kwenye Kanuni za Bunge Kanuni ya 57, 58, 61 - Haki na Madaraka ya Bunge. Nikaangalia mwongozo nikikosea hapa nitaenda kwenye Kamati ya Maadili, ukisoma Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge, nikasoma Ibara ya 100 humu. Sasa kama leo nitazungumza humu Mbunge ninatakiwa nimhoji Waziri, halafu nikimaliza ninaambiwa nitaenda kuhojiwa sehemu nyingine ninataka niseme kwa mazingira

ambayo Bunge letu tumeingia, kwa changamoto tulizopata kwa wananchi wetu, watu wa Tarime Vijijini, wapigakura wangu wanamjua Waitara yukoje, hakuna Waitara wa Jumapili wala Jumatatu wala Jumanne, Waitara ni mmoja siku zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba Bunge hili na Wabunge wameangalia sura za watu waliopo humu ndani, tulikuwa wengi, tupo sasa 30%. Wenzetu wamekuja, kikulacho kinguoni mwako. Kila mtu afanye kazi ya wananchi kwenye Bunge hili na Serikali iende ijipange vizuri, wakiwasilisha hoja wafanye kama anavyofanya Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo! Mbona Waziri Kitila watu hawalalamiki? Analeta hoja za kitaalam ameenda amejifungia, sasa mpango huu tungetamani, watu wanasema ni Mpango wa Maji, Maji, Maji, Waziri kijana Aweso aje atuambie yeye anakwama wapi katika Wizara yake tumsaidie kama ni kubadilisha sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu wa kilimo aje atuambie malalamiko ya wafugaji na wakulima kila mwaka tunazungumza hapa, watu wanauana, leo hii unaleta mpango wa Serikali tuoneshe namna ambavyo wakulima watalima kwa mpango, namna ambavyo wafugaji watafuga kwa mpango na bila ugomvi kuwe na amani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge wa Tarime vijijini nina shida ninapiga hapa mwaka huu ni awamu ya pili kwa Jimbo la Tarime Vijijini, Jimbo la Ukonga ilikuwa awamu ya kwanza, ninazungumza malalamiko ya Hifadhi ya Serengeti kuhusu habari ya mipaka tu! Ng'ombe wanatekwa, watu wanapotea pale. Ndugu zangu! hapa ninapozungumza Karakatonga kuna watu watano hawapo. Sasa ukiniambia mambo mengine!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda Bunge lifanye kazi yake, Serikali ifanye kazi yake na Mahakama ifanye kazi yake, kama ambavyo tukienda Mahakamani tunanyenyekea na Serikali wakija hapa tuzungumze kama Mhimili, tufanye kazi ya wananchi. Rais atalindwa kwa wivu mkubwa, yeye ameshamaliza kazi yake kama kuna mtu amepata fursa ya kumsaidia na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba tunajua anaweza kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninasoma watu wa Singapore walifanikiwa kwa namna gani, ni *meritocracy,* tufanye kazi kwa uwezo wa mtu, tufanye *proper placement* kwenye maeneo, tufanye kazi ya mapinduzi, huu mpango huu ukiusoma vizuri ni mpango wa kimapinduzi. Hatuwezi kujadili mzaha mzaha hapa, hatuwezi kupiga piga makofi, tumuunge mkono Rais, tutunge sheria za kufunga watu, ukienda ukaiba tukwambie umeiba, *you are in for it*, ukidanganya tukwambie umedanganya *you are in for it,* tusilete blaa blaa, hili Bunge Watanzania wanatutegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, ahsante kwa hayo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waitara kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, simwoni, basi tutaendelea na mchangiaji anayefuata na atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho Mheshimiwa Ali Nasoro Omar King

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, lakini majina yangu hasa sahihi ni Ali Hassan Omar King.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Ali Hassan Omar King.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kupata hii nafasi, pia ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka hai na kunijalia siku ya leo kusimama katika Bunge hili Tukufu kuweza kuandika mipango au kutoa ushauri na maoni juu ya uandikaji wa mipango ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Mbunge aliyesimama hapa, wengi miongoni mwao walikuwa wanaonesha wasiwasi juu ya utekelezaji wa mipango hii au mpango huu, mwisho amesimama Mheshimiwa Waitara naye pia ameonesha wasiwasi juu ya utekelezaji wa mpango huu. Kamati ilishauri na mimi ninaongezea kushauri, kwa nini tusiweke sheria ya kutekeleza huu mpango?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunapopitisha bajeti tunakuwa tuna *The Appropriation Act* na tunakuja tunaihoji Serikali juu ya utekelezaji, tunakuja hapa baada ya miezi sita kwa mujibu wa sheria ya bajeti tunakuja kufanya, kama kunafanyika *mid-review* basi Serikali inatupa habari kwamba kitu gani kimefanyika. Kwa hiyo, ninaunga mkono kwanza wazo hilo la Kamati, lakini ninatia mkono zaidi kwamba huu mpango basi tugeuze iwe sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nichangie katika ugharamiaji wa mpango, katika ugharamiaji huo tumesema kwamba sekta binafsi itachangia 70%, nilitamani zaidi Wabunge tungejadili huko kwenye hizo 70%, niseme tu Serikali wajiandae kuwa na vivutio vizuri kwa sekta binafsi za ndani na nje ili mpango huu utekelezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa ushauri huo tu sitaki kwenda mbali katika hizi 70%, sekta ya umma ambapo Serikali yenyewe itagharamia mpango huu kwa 22%, lakini ugharamiaji mzima wa mpango ni sawasawa na dola trilioni 3.6 *approximately*. Sasa nitachangia juu ya uchangiaji wa Serikali katika mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huu Waziri amesema kuwa Tanzania kupitia Benki Kuu tutaendelea kununua dhahabu, sasa nami hapa hapa katika kugharamia mpango huu tunaweza kupitia hii kwenye kugharamia dhahabu tukapata fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mpango huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhahabu huwa tunaitumia kuweka *reserve (federal reserve)* ya nchi, kwa hiyo inatusaidia *sometimes percentages* tunayoamua kuiweka inatusaidia kuingiza katika *reserve* kwa sababu Serikali yetu au Benki Kuu huwa inafanya *portfolio* ambayo wenyewe wanaita *strategic reserve allocation*. Inawezekana wakaweka katika Dola asilimia fulani, katika *Euro* asilimia fulani, katika *Yuan* asilimia fulani na katika dhahabu tumeweka asilimia fulani. Tumeanza kuweka kwenye dhahabu ambayo ndiyo ninaizungumzia asilimia tano,

lakini tukawa tunaendelea tunaanza kuweka 10% na huenda tukazidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoweka vizuri tukizidi kwenye *reserve,* yale matumizi yetu ya miezi minne ambayo sasa hivi tuna miezi 4.9 tunapata kuwa na *special drawing rise* kubwa ambayo *supplementary* au ziada ya kile kilichowekwa tunapata kukopa kitu ambacho kinaitwa *concessional loans*. Mikopo ambayo pengine unaweza ukaipata hata chini ya asilimia moja hiyo ni *financing* ya kwanza, ni kwa sababu tumeweka dhahabu, hiyo *ni financing* ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Financing* ya pili, tunaweza tukaweka hiyo dhahabu ambayo ziada yake dhahabu hiyo ambayo tukiisha kuweka tunaweza ikiwa nyingi, tunaweza tu tukasema kwamba tuweke dhamana tukapata fedha kwa kuweka ile dhamana, fedha zile zinaweza zikaja kwenye miradi na huu utaratibu siyo wa kigeni, siyo mgeni duniani utaratibu huu, utaratibu huu upo na uko katika mfumo wa *international bullion system*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wanaojua waangalie wataona, sasa tukiweka dhamana dhahabu zetu katika kiwango ambacho kinakubalika tutapata fedha. Jambo la tatu, tunaweza tukaweka dhahabu nyingi na kiwango kile ambacho kitakachozidi tunao uwezo wa kuziuza dhahabu zile, au tunao uwezo wa kuweka dhamana tukanunua *bond* ya Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *bond* ya Marekani sasa hivi ya miaka miwili, sasa imefikia asilimia 3.5. Asilimia 3.5 ni kiwango kikubwa wakati fedha zako ziko palepale zitakuja kutekeleza hii miradi. Pia katika kuweka dhamana wanaku-*charge* asilimia mbili, utakapokuwa-*charged* asilimia mbili kwa dhamana ina maana ukipata 3.5, 1.5 ni faida na fedha zako ziko palepale, lakini umepata faida. Kwa hiyo, kila tukiweka dhahabu kwa wingi tunapata faida zaidi pia kiwango cha dhahabu kinachozidi tunaweza hata tukauza halafu tukanunua tena, si tunayo wenyewe hii? Kwa kuwa, tunayo wenyewe leo kitu chako kikikusaidia inakuwa nongwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze ndugu zangu, kuna mtu mmoja kule kwetu, jina lake anaitwa Mbu, Baba yake anaitwa Mbu na Babu yake Mbu, kiufupi ukimtaja majina yake yote anaitwa Mbu Mbu Mbu, alijaribu kujadili mambo haya! Huyo Mbu Mbu Mbu alitaka kujaribu mambo haya, kwa hiyo hawezi kuelewa. Huu utaratibu upo duniani unatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije katika ushauri wangu katika sehemu nyingine, ushauri wa Kamati *page* namba 13 walisema kwamba Serikali iimarishe matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kukusanya mapato ya kodi na yasiyo ya kodi; lakini wakaeleza kwamba *TRA* aliomba bilioni 480 kwa ajili ya kuimarisha mifumo. *TRA* amepewa bilioni 120 ambayo ni sawa 25% kwa ajili ya kuimarisha mifumo. Ina maana hii mifumo inayotumika imeboreshwa kwa 25% bado kwa 75%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishauri Serikali kwamba hebu watoe na hizo shilingi bilioni 360 ili tupate mfumo kamili; kwa sababu kati ya mifumo ilipoimarishwa mfumo mmoja ulioimarishwa ulikuwa huu ni wa *IDRAS* ambao unashughulikia mapato ya ndani. Mfumo huu umerekebishwa kwa 25% bado ziko *modules* ambazo zinatakiwa ziingizwe katika mfumo huu ili uweze kufanya kazi kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walipotumia fedha hizo 25% pia walirekebisha mfumo ya *TANCIS,* lakini bado ziko *modules* zinahitajika ndani ya mfumo huu ili mfumo huu uweze kwenda sawa; na kwa sababu inashindikana hata kufanya *comparability,* kwa sababu Mfumo wa *TANCIS* tunatumia kwa *East Africa.* Sisi hatuwezi kuona ule ulinganifu kama wanavyofanya watu wetu wengine. Huwezi kujua kama umepigwa au umepiga wewe. Tukiuboresha mfumo huu unaweza ukaja ukatufanyia mambo mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tuna mfumo hapa unaitwa *ETS (Electronic Tax Stamps)* ambao ulikuwa *vender* wake ni *SICPA*. Mfumo huu ilikuwa tayari uwe umekwishakabidhiwa Serikalini. Mwaka 2017 wakati mfumo huu anapewa *SCPA* ilikuwa a-*run* kwa muda wa miaka mitatu arithishe elimu kwa watu wetu ili

uweze kufanya kazi. Sasa hivi bado tunahangaika na kumlipa *vender,* bado mfumo huu sisi hatujauchukua tunaanzisha na mifumo mingine. Kwa nini mfumo huu usije huku? Ambapo *serving* yake tutatekelezea miradi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe tunakosa mapato kutokana na maeneo tofauti katika nchi katika mipaka. Upande wa nchi jirani wanazo *scanners,* lakini ukija kwa upande wetu hakuna *scanners.* Watu wamefanya *research* wamepita Horohoro hakuna *scanners,* wamepita Holili hakuna *scanner,* Tunduma ipo lakini foleni kubwa. Kwa hiyo, inahitajika *scanner* ziwe nyingi. Pia Namanga kulikuwa bado hakuna *scanner* na kama itakuwa imechukuliwa ni ndani ya wiki mbili hizi. Niiombe Serikali iangalie utaratibu wa kukusanya mapato. Tukiweka *scanners* ina maana kwamba mapato yetu hayataweza kuondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine tupime ardhi. Tunayo ardhi nzuri sana. Tutakapopima na kutoa hati tutapokea pango la ardhi. Makisio yanasema tuna uwezo wa kupata trilioni mbili kwa mwaka kwa sababu ya kodi ya ardhi tu. Sasa kwa nini hili Serikali hatuingii tukafanya hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo ardhi peke yake; tumetoa mfano, Mji wa Mtumba ule pale.  Ninauchukulia ule ni mji wa mfano. Kila kitu chake kimepimwa. Barabara ziko pale. Kila kitu kiko pale majengo yamekaa ukipita unaona raha. Hivyo katika mpango wetu huu wa miaka 25 kutoka 2025 mpaka 2050 tutakaa kwenye makazi hayahaya Mbagala na kwingine huko? Tutakuwa hivi hivi?  Ninaomba Mheshimiwa Waziri atuelezee na mpango wa makazi. Tupime ardhi lakini na mpango wa makazi uwepo. Kama hatutakuwa na mpango wa makazi kwamba hii itakuwa siyo nchi inayokua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilizungumzie, tunakua kwa kasi kiteknolojia na kila sekta imetajwa huku inatakiwa ikue; na kwa kuwa kila sekta inatakiwa ikue ina maana tunahitaji elimu ya ufundi. Tunahitaji kuwa na *skills* ili tuwe na kilimo kizuri. Kila mmoja aliyelalamika hapa kuhusiana na mbegu zile ni *skills*. Watu waliolalamika hapa kutokana na

viwanda, tunakosa *skills*. Tumesema kwamba *foreign direct investment* itakuwa 57%. Watakuja watu wa nje lakini je; *raw materials* tutakuwa nayo, sawa; lakini watakaoajiriwa pale ni akina nani? Kama wasipoajiriwa watu wenye *skills* ina maana kwamba tutapoteza na huu uchumi wetu pato lile tutaingia wasiwasi kulipata. Ninazungumzia kwenye *skills,* mfano China watu wanafuata *skills, raw materials* zipo, ukitaka za viwanda zipo, ukitaka za kilimo zipo, lakini wanafuata *skills. Skills* zinazopatikana pale ndiyo maana wanakuwa wako *competitive* katika dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimechukua muda wako mwingi unisamehe, lakini huu ni ushauri. Huu mpango unawezekana kabisa kutekelezeka na unatekelezeka, *GDP* iliyokusudiwa inapatikana, *per capita* inapatikana. Ikiwa tutawekeza kwenye ujuzi tuwekeze mapema maana ni wa miaka 25. Kwa hiyo, tusije kuwekeza mwaka wa mwisho. Tuwekeze mwanzo; tukiwekeza mwanzo *productivity* itakuwa ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa King. Waheshimiwa Wabunge huyo ndiye alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa jioni hii ya leo. Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

*(Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Tumemaliza michango ya leo; kwa hiyo, kabla ya kuahirisha Bunge kuna matangazo machache. La kwanza, Waheshimiwa Wabunge wote wanakumbushwa kuwa Ofisi ya Uhamiaji watakuwepo katika viwanja vya Bunge kwa ajili ya kutoa huduma ya hati za kusafiria *(passport)* kwa Waheshimiwa Wabunge pamoja na watumishi. Zoezi hili litaanza kesho tarehe 4 Februari, 2026, katika ukumbi namba 9 ulioko jengo la utawala *ground floor.* Waheshimiwa Wabunge, mnaombwa kufika na nyaraka zifuatazo: -

Kwa Waheshimiwa wenye *passport:-*

(a) Picha moja;
(b) Barua ya ofisi ya utambulisho; na
(c) Kitambulisho cha Ubunge.

Kwa Waheshimiwa wasiokuwa na *passport:-*

(a) Barua ya ofisi ya utambulisho;
(b) Kitambulisho cha Ubunge;
(c) Cheti cha kuzaliwa; na
(d) Picha moja.

Waheshimiwa Wabunge, ili kurahisisha zoezi hili mnaombwa mfike na vishikwambi vyenu kwenye ofisi hiyo.

Pili, ni kukumbushana tu; tulipofika tulipewa begi na kulikuwa na Kanuni - kitabu cha *blue,* Waheshimiwa mwendelee kukipitia. Jambo ambalo linajitokeza, siyo mara nyingi, ni Wabunge kukatisha kati ya Kiti na Msemaji.

Waheshimiwa Wabunge, tuna *description* ya kulisema, lakini halileti picha nzuri kwa Mbunge ambaye atakuwa anaambiwa kwamba kaa chini. Kwa hiyo, tuwaombe sana zipitieni Kanuni, Kanuni ya 76(3)(a), (b) mpaka (c) zinaweka hayo masharti. Sharti lingine ni kutopita mbele ya Siwa au pembeni ya Siwa isipokuwa pale ambapo umeruhusiwa kwa mujibu wa taratibu zetu. Kama umeitwa kuja kuongea hapa au msafara unapita na vitu kama hivyo. Kwa hiyo, tuwaombe tuendelee kuzifuatilia hizo Kanuni zetu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo matangazo machache, ninaahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.48 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 4 Februari, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*